# MGAO MPYA WA KAZI ZA MWANAUME KATIKA HADITHI FUPI ZA KISWAHILI

**NA**

**PENNINAH SOFIA NZONG'A**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A) KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**NOVEMBA 2020**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

Sahihi ..................  Tarehe...16/11/2020...

PENNINAH SOFIA NZONG'A

C50/CE/26018/2011

Tasnifu hii imetolewa kwa Chuo Kikuu cha Kenyatta kwa idhini yetu kama wasimamizi.

Sahihi ..................  Tarehe...16-11-2020...

DKT. RICHARD M. WAFULA

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

Sahihi..................  Tarehe ...16 NOV 2020...

DKT. MIRIAM K. OSORE

IDARA YA KISWAHILI

CHUO KIKUU CHA KENYATTA

## TABARUKU

Kwa marehemu mama yangu Damaris kwa kunipa motisha wa kusoma. Mungu akuweke pema peponi. Kwa mume wangu Peter, wanangu Kennedy, Lilian na Collins kwa kuvumilia nilipokuwa masomoni.

# SHUKRANI

Shukrani za dhati kwa Maulana kwa kunijalia na kunikirimia neema, uzima wa mwili na hekima hadi nikaweza kukamilisha kazi hii.

Pia, nawashukuru kwa udhati wa moyo wasimamizi wangu Dkt. Richard Wafula na Dkt. Miriam Osore. Uongozi wenu wa busara na ushauri wenu wenye uvumilivu ulinifaa katika utafiti huu. Nashukuru kwa kunivumilia kuanzia mwanzo hadi nikafikia tamati mwa kazi hii. Mungu awazidishie maarifa, hekima, upendo na uvumilivu wa kuwaongoza wanafunzi wengine.

Shukrani kwa wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika kwa kunielekeza katika masomo yangu na pia kunipa mwongozo nilipokuwa nikitetea pendekezo la utafiti huu. Mungu awabariki sana.

Wanafunzi wenzangu, Phoebe, Peninnah, Ndunge, Kennedy, Lucy, Kamanja, Makandi na Janet shukrani kwa kunipa motisha katika masomo na kushirikiana nami katika mijadala yote ambayo kwa kweli ilinijenga na kupanua akili yangu. Safari hii ilikuwa ndefu lakini kwa ushauri wenu nimeweza kuikamilisha salama. Asanteni.

Marehemu mama yangu, nakushukuru sana kwa bidii zako katika masomo yangu. Ulinihimiza kusoma kwa bidii hadi kufikia kilele. Ingawa hujawa hapa kushuhudia mazao ya ushauri wako na jitihada zako, najua popote ulipo unashangilia nami.

Mwisho, shukrani za dhati kwa mume wangu mpendwa Peter Mbugua na watoto wangu Kennedy, Lilian na Collins kwa kunifaa kwa hali na mali wakati wa masomo yangu. Mlivumilia upweke nilipokuwa masomoni. Mungu awabariki.

## MAELEZO YA ISTILAHI MUHIMU

| | |
|---|---|
| Mgao mpya wa kazi za mwanaume – | Hii ni kazi ambayo mwanaume anatekeleza Sasa kinyume na kazi yake ya kimapokeo. |
| Masuala ibuka- | Istilahi hii inatokana na maneno mawili; suala na ibuka. Neno suala lina maana ya kimsingi ya jambo linalohitaji kujadiliwa na kukatiwa shauri. Nalo neno ibuka linamaanisha kufika mahali bila kutarajiwa. Masuala ibuka katika utafiti huu yanamaanisha mambo ambayo yamejitokeza katika jamii na hayakuwepo tangu jadi. |
| Mfumo wa kuumeni- | Mfumo wa kijamii, kisiasa na kiuchumi unaohakikisha uhifadhi na udumishaji wa mamlaka ya mwanaume katika nyanja zote za maisha. |
| Tasnifu- | Hali asili ya kitu/kitu kisichokuwa kamilifu. |
| Tabaini- | Kukinzana kwa tasnifu. |
| Kusanisi- | Zao la migongano ya tasnifu na tabaini. |
| Uana- | utambulisho wa wanawake na wanaume kwa mujibu wa jamii husika. |

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| FWWC - | Fourth World Women Conference |
| JM - | Jumuia ya Madola |
| TTWCW - | The Third World Conference on Women |
| Uk - | Ukurasa |
| UM - | Umoja wa Mataifa |
| WCIWY - | World Conference of International Women's Year |
| WCUND- | World Conference of the United Nations Decade |

## IKISIRI

Utafiti huu ulidhamiria kuainisha, kueleza na kuchanganua mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili**.** Diwani za *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004) ambayo imehaririwa na Wamitila, *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007) ambayo imehaririwa na Walibora na Mohamed, *na Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* (2011) ambayo imehaririwa na Sanja zilichanganuliwa. Diwani hizi ziliteuliwa kimaksudi kwa sababu hadithi zilizoteuliwa kutoka kwenye diwani hizi zimesawiri wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi. Pia ni za kisasa na zinashughulikia masuala ibuka katika jamii kama ulivyo mgao mpya wa kazi za mwanaume. Hadithi nne kutoka kwa diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* hadithi tatu kutoka kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* na hadithi tatu kutoka kwenye diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* ziliteuliwa kimakusudi. Hadithi ambazo zina wanaume ambao wanafanya kazi ambazo awali zilichukuliwa kuwa za wanawake ziliteuliwa. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uana na nadharia ya upembuzi. Nadharia hizi mbili kwa pamoja zilionyesha jinsi majukumu ya kiuana yamekuwa yakijengwa na jinsi yamebadilika kulingana na mfumo wa jamii yenye kusisitiza usawa wa kijinsia. Nadharia ya uana ina misingi yake katika usomi wa kijinsia na imejikita katika utanzu wa sosiolojia kuanzia mwaka wa 1950. Nadharia hii inashikilia kuwa majukumu ya kiuana hubandikwa na kulazimishwa kupitia ushawishi wa kijamii. Nadharia hii ilitufaa kuonyesha jinsi jamii ilijenga majukumu ya mwanaume na kuyapitisha kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Nadharia ya upembuzi inahusishwa na Hegel. Nadharia hii inashikilia kuwa, kila kitu kimeundwa kwa hali mbili kinzani, kila kitu kinapita na kina kikomo kwa kipindi cha wakati kinachopatikana. Nadharia hii ilitufaa kuonyesha ukinzano baina ya mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume na mgao mpya wa kazi zake katika hadithi fupi teule kama utanzu wa kisasa unaoshughulikia masuala ibuka. Utafiti huu ni wa kimaelezo kwa sababu data yake inapatikana katika maandishi na hauhusishi takwimu. Mbinu ya uchanganuzi matini ilitumiwa kuchanganua hadithi zilizoteuliwa na matokeo kuwasilishwa kwa njia ya kimaelezo. Kama yalivyokuwa matarajio ya utafiti huu, wanaume katika hadithi zilizoteuliwa wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume kama vile kupika, kuosha nguo, kuosha vyombo na kushirikiana na wanawake kulima na kutoa ushauri katika familia zao.

## ABSTRACT

This study sought to identify, describe and analyze new male roles in selected Kiswahili short stories from *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine (2004)* edited by Wamitila, *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine (*2007) edited by Walibora and Mohamed and *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* (2011) edited by Sanja. The short stories for analysis were purposively selected. They depict male characters who have accepted roles that were traditionally viewed as feminine. They are also contemporary in that they show emerging issues in society. Four stories from *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, three from *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*, and three from *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* were analyzed. Only stories with male characters who have taken up roles which were traditionally viewed as feminine were analyzed. Content analysis was used to evaluate the selected stories and present the findings of the study. This study was guided by Gender Theory and Dialectic Theory. This is because, the two theories together describe how gender roles have been constructed by the society in which the authors live and how they have changed according to contemporary society that emphasizes on gender equality. Gender theory has its roots in gender studies and it is sociological. It upholds that gender roles are constructed and forced through cultural influence. The theory assisted the researcher show how society constructed male roles and passed certain gendered characteristics from one generation to another. Dialectic theory has its roots in Hegel and it is based on the principle of contradictions. It says that everything is composed of two opposing forces and that everything is passing and has an end at a given period of time. This theory enabled the researcher show the conflict of the traditional male roles and the emerging male roles in today's society. Analysis of data was guided by the tenets of Gender and Dialectic theories. The study was qualitative because the data was in the form of words. Content analysis was used to analyze the selected stories. Presentation of data was done descriptively. From the study, it emerged that male characters in the stories have taken up the new male roles like cooking, washing clothes and taking advices and instructions from women.

## YALIYOMO

Ungamo …………………………………………………………………… ii

Tabaruku ………………………………………………………………… iii

Shukrani ……………………………………………………………….. iv

Maelezo ya Istilahi ……………………………………………………… . v

Vifupisho ………………………………………………………………..vi

Ikisiri ……………………………………………………………………vii

Yaliyomo ………………………………………………………………… ix

SURA YA KWANZA

1.0 Usuli ……………………………………………………………… 1

1.1 Suala la Utafiti ………………………………………………….. 5

1.2 Maswali ya Utafiti ………………………………………………….. 6

1.3 Malengo ya Utafiti ………………………………………………… 6

1.4 Sababu za Kuchagua Mada ……………………………………… 7

1.5 Upeo na Mipaka …………………………………………………… 11

1.6 Misingi ya Nadharia…..…………………………………………. .. 12

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu Mada ………………………………….. 26

1.8.0 Mbinu za Utafiti……………………………………………………………….33

1.8.1 Muundo wa Utafiti…………………………………………………………….33

1.8.2 Uteuzi wa Sampuli………………….…………………………………….34

1.8.3 Ukusanyaji wa Data…………………………………………………………… 35

1.8.4 Uchanganuzi wa Data…………………………………………………………..36

1.8.5 Uwasilishaji wa Matokeo……………………………………………………… 37

1.9 Hitimisho………………………………………………………………………..37

SURA YA PILI

2.0 Utangulizi………………………………………………………………….. 38

2.1 Mgao wa Kazi za Mwanaume katika Hadithi Fupi Teule…………….. 44

2.2 Mgao wa Kazi za Mwanaume kinyume cha Mgao wa Kitamaduni….. 44

2.3 Mgao wa Kazi za Mwanaume kwa kuzingatia Ushirikiano…………. 67

2.4 Hitimisho……………………………………………………………………..80

SURA YA TATU

Sifa za Wanaume Wanaochukua Mgao Mpya wa Kazi

3.0 Utangulizi ……………………………………………………………… 83

3.1 Ni wasomi…………………………………………………………….. 84

3.2 Watambuzi wa Mantiki ya Mgao Mpya wa Kazi za Mwanaume……… 88

3.3 Wakubalifu …………………………………………………………….. 91

3.4 Waadilifu ……………………………………………………………….. 93

3.5 Wenye Mapenzi ya Dhati …………………………………………… 98

3.6 Wanyenyekevu ……………………………………………………….. 100

3.7 Waliopata Uzindushi wa Kiuchumi ………………………………… 103

3.8 Wenye Mwamko wa Usawa wa Kijinsia……………………………… 107

3.9 Hitimisho …………………………………………………………… 111

SURA YA NNE

Athari za Mgao Mpya wa Kazi za Mwanaume kwa Mhusika Mwanaume

4.0 Utangulizi ……………………………………………………………… 113

4.1 Huongeza Mapenzi…………………………………………………… 114

4.2 Huleta Ushirikiano baina ya Mwanaume na Mwanamke …………… 116

4.3 Husababisha Utoshelevu wa Moyoni ……………………………….. . .119

4 .4 Huleta Ufanisi katika Maisha ya Mwanaume ………………………… 125

4.5 Humfanya Mwanaume Kujihisi kuwa wa Maana katika Familia yake.... 128

4.6 Hufaidika …………………………………………………………… 129

4.7 Husababisha Mikinzano……………………………………………… 131

4.8 Hitimisho …………………………………………………………… 134

SURA YA TANO

Mhutasari, Matokeo, Mchango na Mpendekezo

5.0 Utangulizi ………………………………………………………….. 138

5.1 Muhtasari…………………………………………………………….. 140

5.2 Matokeo ya Utafiti…………………………………………………… 142

5.3 Mchango wa Utafiti ………………………………………………… 147

5.4 Mapendekezo ………………………………………………………. 147

Marejeleo…………………………………………………………………...150

# SURA YA KWANZA

## Utangulizi wa Utafiti

### 1. 0 Usuli

Utafiti huu umebainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Mgao mpya wa kazi za mwanaume ni suala ambalo lina historia ndefu na linajikita katika nadharia ya uana. Kulingana na Merriam Webster (2003) mgao wa kazi ni utaratibu wa kugawia mtu au kundi la watu kazi mahususi. Mgao mpya wa kazi za mwanaume katika utafiti huu ni wajibu ambao mwanaume anatekeleza sasa kinyume na wajibu wake kimapokeo kama vile kupika, kuosha nguo na kulea watoto. Kazi hizi zilitengewa wanawake katika jamii nyingi za Kiafrika ambazo ziligawa kazi kwa kuegemea mfumo wa kuumeni.

Ndungo (1998) anasema kuwa mfumo wa kuumeni ulimpa mwanaume nafasi ya kwanza katika nyanja zote za maisha. Aidha, Osore (2008) na Gitau (2005) wakimnukuu Masinjila (1992) wanasema kuwa mfumo wa kuumeni ni mfumo wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ambao huhakikisha, huhifadhi na kuendeleza mamlaka ya mwanaume katika nyanja zote za maisha. Mgao wa kazi katika jamii za Kiafrika na kazi za kifasihi ulijikita katika mfumo huu.

Gitau (2005), anasema kuwa majukumu ya mwanaume yaliundwa na jamii zinazoendelea kubadilika kwa kuegemea misingi ya kijinsia. Misingi hii ilitumiwa katika mgao wa kazi ya kila mwanajamii. Kwa mujibu wa Adler (1993),

wasichana hufunzwa kutilia maanani majukumu ya kijamii na hutarajiwa kukaa nyumbani huku wakijifunza majukumu ya jikoni kama vile kupika, kutafuta kuni, kuchota maji na kusuka nywele. Misingi hii huwapa wasichana majukumu ambayo hayachangii moja kwa moja katika utafutaji wa riziki; hayakuambatana na malipo na hivyo yalionekana kuwa ya hadhi ya chini yakilinganishwa na ya wanaume. Benjamin (1976) anasema kuwa majukumu ya kiuana hubandikwa na kulazimishwa kupitia ushawishi wa kijamii. Jamii ya Waswahili kama jamii zingine za Kiafrika iliyabainisha majukumu ya kila jinsia tangu utotoni. Wanaume walikuwa na jukumu la kuwa kichwa cha familia na kukimu mahitaji yao (Ndungo, 1998). Mgao huu wa kazi ndio mgao wa kitamaduni ambao ulitumiwa na wasanii katika kuwasawiri wahusika wa kifasihi hasa kabla ya mwamko wa usawa wa kijinsia.

Jamii za Kiafrika wanamokulia wasanii mbalimbali zimepitia mabadiliko mengi yakiwemo ya kihistoria na mahusiano katika familia. Mabadiliko haya yalitarajiwa kudhihirika katika kazi za wasanii hao kama vile mgao wa kazi za mhusika mwanaume katika hadithi fupi. Eagly na Kite (1987) wanasema kuwa athari ya majukumu ya kiuana ni ukariri wa tabia na mielekeo inayochukuliwa kuwa kawaida. Aidha, Eagly na wengine (2004) wanasema kuwa majukumu na vielelezo kaririwa vyote ni kaida na matarajio ya jamii. Kwa hivyo, mgao wa kazi za kiuna ni michakato ya jamii na hutarajiwa kutekelezwa kama ulivyoumbwa.

Utekelezaji wa kazi hizi unaweza kuzua kutoelewana wakati mtu hapendezwi na mgao wa kazi za jinsia yake na hivyo basi anafanya kinyume. Hali hii huzua mkinzano wa ndani kwa ndani na kusababisha utafutaji wa suluhu mwafaka. Mwanaume kama zao la jamii na mhusika wa kifasihi anatarajiwa kutekeleza kazi zake kwa jinsi ambavyo zitaafiki mabadiliko yaliyopo katika jamii kihistoria na kiuchumi. Hadithi fupi teule kama utanzu unaoendelea kukua unatarajiwa kushughulikia masuala ibuka katika jamii inayopitia mabadiliko kama ulivyo mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Katika miaka ya karibuni, kumekuwa na mikataba mbalimbali inayotetea usawa wa kijinsia kupitia kwa mashirika mbalimbali. Mikutano mbalimbali ya kimataifa imefanyika kuanzia mwaka wa 1975 hadi 1995 kutetea haki za wanawake na kuhimiza usawa wa kijinsia katika nyanja zote za maisha. Mikutano hii ni: *World Conference of the International Women's Year* 1975, *World Conference of the United Nations Decade: Equality (*1980), *The Third World Conference on Women* (1985) na *Fourth World Women Conference (1995).* Mikutano hii inakisiwa kuwa imesababisha mabadiliko ya falsafa za watu kuhusu mgao wa kazi. Spence na Hahn (1997) wanasema kuwa majukumu ya kiuana yanabadilika na imani za wanajamii sasa zimekuwa za kisasa huku wakichuja baadhi ya tamaduni zikiwemo za mgao wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi.

Mgao mpya wa kazi za mwanaume umekuwa suala ibuka ambalo limezaliwa na mabadiliko ya kiuchumi, kihistoria na falsafa za watu. Aidha, Gitau (2005)

anasema kuwa mabadiliko ya kiuchumi yaliyotokea baada ya majilio ya enzi ya ukoloni katika jamii za Kiafrika yamebadilisha majukumu na hadhi ya wanawake. Sasa, wamekuwa na wajibu wa kuikimu na kuitunza familia sawia na wanaume. Waandishi wa hadithi fupi za Kiswahili wanachora mambo halisi katika jamii kisanaa ambapo mgao wa kazi za mwanaume umechukua mwelekeo tofauti na wa kitamaduni. Diwani za *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* (2007), *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* (2004) na *Mwavyaji Wa Roho na Hadithi Nyingine* (2011) zilichanganuliwa ili kudhihirisha haya.

Kama ilivyotajwa hapo awali, majukumu ya mwanamume yalijengwa kwa misingi ya mfumo wa kuumeni katika jamii za Kiafrika. Ndungo (1998) anasema kuwa huu ni mfumo wa uongozi wa kiume ambapo mwanaume ndiye kiongozi wa familia. Mwanaume alipewa nafasi ya kwanza katika nyanja zote za jamii. Kazi alizopewa zilionekana kama zenye hadhi kuliko za mwanamke. Jamii nyingi za Kiafrika zina mfumo unaompa mwanaume nguvu dhidi ya mwanamke katika nyanja zote za maisha kama vile kiuchumi, kisiasa na pia katika ugawaji wa majukumu (Kimani, 2003). Mgao wa kazi za mwanaume umepitia mabadiliko mengi kutokana na mabadiliko ambayo jamii imepitia na kuyafanya yawe suala ibuka ambalo linahitaji kutafitiwa.

Utafiti huu umebaini kuwa “kichwa” kama jukumu la kimsingi la mwanaume kimetwaliwa na mwanamke. Wanawake katika hadithi zilizoteuliwa sasa wamechukua jukumu la kuwa kichwa na kutoa amri na ushauri katika familia zao

na kusababisha ukinzano wa mgao wa kitamaduni na mpya wa kazi za mwanaume. Mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule ndicho kichocheo cha utafiti wetu.

### 1.1 Suala la Utafiti

Utafiti huu umeainisha, kueleza na kuchanganua mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi za Kiswahili kutoka kwa diwani za *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine (2004), Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine(2007)* na *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine(2011*). Mgao mpya wa kazi za mwanaume ni wajibu ambao mwanaume anatekeleza tofauti na wajibu wake wa kimapokeo. Mgao wa kimapokeo ni kama vile kuwa kichwa cha familia na ule mpya ni kama vile kupika na kuosha nguo. Mgao huu umekuwa ukijengwa kwa misingi ya mfumo wa kuumeni unaompa mwanaume mamlaka zaidi kuliko mwanamke. Mgao huu wa kazi za mwanaume umepitia mabadiliko mengi kutokana na mabadiliko ambayo jamii imepitia kiuchumi, kisiasa, kihistoria na kiitikadi. Mgao mpya wa kazi za mwanaume ni baadhi ya masuala ibuka katika jamii kwa sababu umebadilika ili kuafiki mifumo ya uzalishaji mali katika jamii hasa ile inayotilia maanani usawa wa kijinsia.

Utafiti huu umechunguza mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa mikusanyiko iliyoteuliwa na sifa za wanaume ambao wameuchukua. Pia, umebainisha athari za kuuchukua mgao mpya wa kazi kwa mhusika mwanaume.

### 1.2 Maswali ya Utafiti

**(i**) Ni mgao upi mpya wa kazi za mwanaume umesawiriwa katika hadithi fupi za diwani za *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine na Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine?*

(ii) Wanaume wanaochukua mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili wana sifa gani?

(iii) Mgao mpya wa kazi za mwanaume una athari gani kwa mhusika mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili?

### 1.3 Malengo ya Utafiti.

Utafiti huu ulikusudia kutimiza malengo yafuatayo;

*(i)* Kubainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi za Kiswahili kwenye diwani za *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine, Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine na Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine.*

(ii) Kuchanganua sifa za wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili na tajriba ambazo zimewafanya kuuchukua.

(iii) Kuchunguza athari za kuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa mhusika mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili.

## 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Kazi hii ililenga kubainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi za Kiswahili. Mada hii ilichaguliwa kwa kuzingatia kuwa, suala la mgao mpya wa kazi za mwanaume ni muhimu katika uandishi wa hadithi fupi kwa sababu ni mojawapo ya matendo ya mhusika katika fasihi. Mhusika ni kipengele muhimu cha fani katika kazi ya kifasihi na usawiri wake unahitaji kuchunguzwa ili kubaini kazi anazotenda katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Utafiti huu unashikilia kuwa ingawa majukumu ya mwanamume yamebadilika ili kuafiki usawa wa kijinsia, kuna haja ya kuonyesha mipaka ya utekelezaji wa mgao wa kazi za kila mwanajamii ili kusuluhisha migogoro inayohusu ni nani anapaswa kufanya nini. Tulichanganua hadithi fupi teule kutoka katika diwani tatu teule ili kubainisha jinsi wasanii wake wanavyoliangazia suala la mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Sababu za kuchagua diwani hizi ni kuwa baadhi ya waandishi wake ni chipukizi ambao wamechangamkia kuangazia masuala ibuka katika jamii kama vile mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi za Kiswahili. Aidha, ni wasomi ambao wamepevuka na kubadili mitazamo yao kuhusu suala la usawa wa kijinsia hasa ugawaji wa kazi katika familia. Hii ina maana kuwa wamekombolewa kimawazo na wanaweza kusawiri wahusika wa kiume wanaofanya kazi ambazo awali zilichukuliwa kuwa za kike. Waandishi hawa wamedhihirisha kuwa kazi ya mwanaume imebadilika kwa kutwaliwa na mwanamke.

Kadhalika, diwani hizi tatu zimechaguliwa kwa sababu zimechapishwa katika kipindi cha miaka ya elfu mbili. Hiki ni kipindi ambacho utanzu wa hadithi fupi umeanza kushughulikiwa kwa kina. Pia, falsafa za watu kuhusu mgao wa kazi zimebadilika kutokana na mikataba kuhusu usawa wa kijinsia na haki za wanawake. Spence na Hahn (1997) wanasema kuwa sasa imani za wanajamii zimekuwa za kisasa na kuchuja baadhi ya tamaduni. Kulingana na kauli hii ya Spence na Hahn (1997) tamaduni za mgao wa kazi za mwanaume zimechujwa na baadhi ya wanaume kuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Utanzu wa hadithi fupi ni mwafaka wa kuwasilisha mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa sababu ni utanzu wa kisasa kama asemavyo Mukopi (2005). Utanzu huu unashughulikia mambo ya kisasa kama vile masuala ibuka katika jamii miongoni mwa masuala mengine. Pia, ni utanzu ambao matukio yake yamejengeka katika misingi ya maisha ya kila siku. Aidha, McOnyango (2006) anasema kuwa utanzu wa hadithi fupi umepata umahiri wake katika fasihi ya Kiswahili katika miaka ya karibuni na haujashughulikiwa vya kutosha na wasanii wa fasihi. Kwa sababu hii, utafiti huu uliushughulikia mgao mpya wa kazi za mwanamume kwa kuegemea utanzu huu ili kuongeza tahakiki za hadithi fupi za Kiswahili na kuujenga utanzu huu.

Isitoshe, utanzu huu tofauti na ushairi andishi huwasilishwa kwa lugha ya nathari na kuufanya kueleweka kwa urahisi. Waandishi wa hadithi fupi za kisasa wanapata kichocheo cha utunzi kutokana na hali halisi ya masuala katika jamii.

Jamii za Kiafrika zimepitia mabadiliko mengi katika mbinu zao za kuzalisha mali kutokana na athari za kigeni. Scanzoni (1979) anasema kuwa shirika la *Women Liberation Movement of 1960* lilibadili tamaduni za awali za kugawa kazi za wanaume na wanawake. Mabadiliko haya yamesababisha mabadiliko katika nyadhifa ambazo mwanamke anatekeleza kwani sasa mwanamke anashiriki kazi ya kukimu familia ambayo awali ilikuwa ya mwanaume.

Goldberg (1976) anasema kuwa mwanaume sasa hatambui jukumu lake kwani mwanamke pia amekuwa mkimu familia. Hii ina maana kuwa mabadiliko ambayo yametokea katika mgao wa kazi ili kuafiki usawa wa kijinsia yameleta utata. Hii ni kwa sababu yale mwanaume alikuwa akifanya, hata mwanamke anayafanya na kwa hivyo mipaka ya mgao wa kazi za mwanaume si wazi. Utafiti huu ulikusudia kubainisha mgao wa kazi za mwanaume ambazo zimetwaliwa na wanawake na pia athari za mgao huo mpya wa kazi za mwanaume.

Kimani (2003) anasema kuwa kutokana na juhudi za wanawake kujikomboa, kumezuka visa vya wanaume kudhulumiwa na wanawake katika maisha halisi kama vile utekelezaji wa majukumu yake katika familia. Mgao wa kazi mpya za mwanaume ni mojawapo ya masuala ibuka ambayo yanahitaji kuangaziwa kwa kina katika utanzu huu wa hadithi fupi za Kiswahili.

Utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa kwa tafiti ambazo zimeshughulikia masuala ya wanawake. Umebainisha usawiri wa mwanaume ambaye anafanya kazi ambazo zinaafiki usawa wa kijinsia. Utawawezesha wasomi wa fasihi andishi

hususan hadithi fupi za Kiswahili kutambua sifa za wanaume wanaopokea mgao mpya wa kazi.  Isitoshe, utaongeza tahakiki ambazo zimeshughulikia masuala ya kijinsia katika fasihi ya Kiswahili.  Aidha, Utahamasisha waandishi kufanikisha sifa ya usasa ya hadithi fupi kwa kusawiri wanaume zaidi wanaobadilishana kazi na wanawake.

Mgao mpya wa kazi za mwanaume ukibainishwa, kuelezwa na kuchanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti utaleta mwongozo mwafaka kwa wasomi wa fasihi andishi ya Kiswahili katika kuangazia mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume. Kazi atakazopewa mwanaume katika hadithi fupi zitaafiki matakwa ya usawa wa jinsia.  Utafiti huu ulikusudia kuchunguza jinsi waandishi wa hadithi fupi teule wanavyoliangazia suala la mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Usomi katika eneo la jinsia umeendelea na kufikia sasa kuna tafiti nyingi za kifasihi ambazo zimeangazia suala la kijinsia kama vile Ndungo (1998), Gitau (2005) na Elishopher (2013) lakini hakuna hata mmoja umeshughulikia uainishaji wa mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi.  Utafiti huu umeainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule.  Kama tulivyosema hapo awali, kutokana na msisitizo wa usawa wa kijinsia wanawake sasa wanashiriki majukumu ya viwandani sawia na wanaume jambo ambalo limechochea mtafiti kuuchanganua mgao mpya wa kazi za mwanaume katika mwamko wa usawa.

### 1.5 Upeo na Mipaka

Utafiti huu ulibainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Katika kuitalii mada hii, mtafiti alichambua diwani tatu za hadithi fupi: *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine, Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* na *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Diwani hizi zimechapishwa katika kipindi cha miaka ya elfu mbili. Hiki ni kipindi ambacho utanzu huu umeanza kushughulikiwa kwa kina.

Mtafiti alichagua hadithi tatu kimaksudi kutoka katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine.* Hadithi za "Dr. Strese" ya (Sheila Ali Ryanga), "Uganga wa Pete" ya (Ayubu Mukhwana) na "Macheo Mengine" ya (Kitula King'ei) zilichanganuliwa. Katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, hadithi nne zilichaguliwa. Hadithi ya "Mke Wangu" ya (Muhammed Said Abdulla), "Kikaza" ya (Robert Oduori), "Ndoa ya Samani" ya (Omar Babu) na "Maeko" ya (Mohamed Khelef) zilihakikiwa. Kutoka kwenye diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* hadithi tatu ziliteuliwa. Hadithi ya "Kachukua Hatua Nyingine" ya (K. W. Wamitila), "Mayai Waziri wa Maradhi" ya (E. Kezilahabi) na "Fumbo la Mwana" ya (Sinjiri Mukuba) ziliteuliwa. Kwa jumla, mtafiti alihakiki hadithi kumi. Hadithi zilizoteuliwa ni zile ambazo zimeonyesha mgao mpya wa kazi za mwanaume.

### 1.6. 0 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uana na nadharia ya upembuzi. Hii ni kwa sababu nadharia hizi kwa pamoja ziliweza kuonyesha jinsi mgao wa kazi za kiuana umekuwa ukijengwa na jinsi umebadilika kulingana na mfumo wa jamii yenye kusisitiza usawa wa kijinsia.

### 1.6.1 Nadharia ya Uana

Nadharia hii ina misingi yake katika taaluma ya usomi wa kijinsia. Imejikita katika sosiolojia ya jinsia utanzu wa sosiolojia kuanzia mwaka wa 1950. Money (1955) ndiye aliasisi istilahi "majukumu ya kiuana". Hata hivyo, kazi yake ilichapishwa mwaka wa 1994. Kwa maoni yake, majukumu ya kiuana ni istilahi ambayo hutumiwa kuonyesha mambo yote ambayo mtu husema au hufanya ili kujidhihirisha kuwa na hulka za kiume au za kike. Money alikuwa anajaribu kuonyesha tofauti kati ya biolojia na uana na uana kama jukumu. Maana yake haikuendelea mpaka miaka ya sabini wakati nadharia ya ufeministi iliendeleza dhana ya uana na kuonyesha tofauti kati ya maumbile ya kiuna na ujenzi wa jamii wa mke au mume.

Benjamin (1976) anasema kuwa majukumu ya kiuana ni tabia na misimamo au mielekeo ambayo mwanaume au mwanamke anatarajiwa kudhihirisha kulingana na hali zao za kijinsia. Akitumia mfano wa Marekani alisema kuwa, katika miongo kadha iliyopita, Wamarekani wamepiga hatua kubwa kwa kukubali na kurekebisha mielekeo yao kuhusu mitazamo mipya ya majukumu ya kiuana. Idadi ya

wanawake katika maeneo ya kufanya kazi imeongezeka huko Marekani na kuwafanya washiriki katika utafutaji riziki. Aidha, wazazi ndio wanzilishi wa athari ya majukumu tarajiwa ya jinsia ya watoto wao kwa sababu ndio walimu wa kwanza.

Baadhi ya wazazi wameshikilia maana ya kitamaduni kuhusu mwanaume na mwanamke na majukumu na shughuli zinazohusika na jinsia hizo. Wanawashughulikia na kuwatunza wasichana na wavulana kwa njia tofauti tangu wakiwa wachanga. Kuna uwezekano wa kutambua urembo wa msichana na mafanikio ya mvulana. Kwa mfano, kumwambia msichana kuwa anapendeza kwa nguo aliyovaa mara kwa mara kunaweza kumchorea taswira kuwa anapongezwa kwa sura wala si yale anayoweza kufanya.

Aidha, wazazi wengi huwahimiza wavulana kuwa wakali na wenye fujo kinyume kwa hivyo, mvulana anakua akijua kuwa anapaswa kuwa mwenye nguvu huku akifanya kazi zinazohitaji nguvu za misuli. Mabadiliko yakitokea katika historia ya jamii hasa katika harakati za uzalishaji mali, huathiri familia, kazi, shule na kila mwanajamii katika utekelezaji wa majukumu yake. Kwa sababu hii, mgao wa kazi za kila mwanajamii unatarajiwa kubadilika ili kuafiki usawa wa kijinsia. Utafiti ulihitajika ili kubaini ikiwa watunzi wa Kiafrika wanaangazia mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume.

Foucault (1978) alichangia pakubwa nadharia hii ya uana. Katika kazi yake '*History of Sexuality'*, alichunguza nadharia tete ya ukandamizaji na kusema kuwa

mataifa ya ughaibuni yalikandamiza ujinsia kuanzia karne ya kumi na saba hadi katikati mwa karne ya ishirini. Alisema kuwa, hii ni nadharia tete ya kinjozi kwa sababu mihadhara juu ya ujinsia ilienea katika kipindi hiki. Anaendelea kusema kuwa wasomi walianza kuchunguza ujinsia kisayansi. Kazi zake zilisadia katika kueleza jinsi uana na jinsia hufanya kazi.

Bem (1981) pia alichangia ukuaji wa nadharia hii kupitia kwa kazi yake kwenye '*Gender schema Theory'*. Alikuwa akielezea jinsi watu hupata majukumu ya kiuana, tabia na mienendo ya kiume na kiuke, kuyadumisha na kuyarithisha kwa wanajamii wengine. Pia, alifafanua jinsi watu hutumia uana kama kiini cha mipangilio katika miondoko ya maisha. Kielelezo hiki kimejikita katika nadharia ya ujifunzaji wa kijamii na nadharia tambuzi ya upataji wa majukumu ya uana. Alikusudia kupima jinsi watu binafsi huafiki majukumu ya kiuana kulingana na upekee wao kama wanaume au wanawake. Kwa hivyo, mtu hutengeneza na kusafisha ujumbe na kudhibiti tabia zao kulingana na fasili ya uuke na uume kwa mujibu wa tamaduni zao.

Butler (1990) katika kazi yake ya kuumbua jinsia anashikilia kuwa "mwanamke"si jambo la kawaida bali hujengeka kupitia urudufu wa mifanyiko ya kijinsia. Hii ina maana kuwa mwanamke na yale ambayo anafanya ni mambo ambayo yanaundwa na jamii anamokulia kupitia kwa ushawishi wa tamaduni na desturi za jamii. Kila mwanajamii anatarajiwa kudhihirisha tabia fulani na kutekeleza majukumu mbalimbali ambayo yametengewa jinsia yake na jamii yake ili kuafiki jinsia hiyo.

Kwa mfano, mwanaume alihitajika kulinda familia na kuichumia. Wanawake nao walihitajika kushiriki majukumu kama vile kupika, kutunza watoto na mume. Jamii huwa imemfunga kila mwanajamii katika utekelezaji wa kaida mbalimbali mgao wa kazi za kiuana ukiwemo. Mwanaume ambaye hajajitenga na jamii yake, amewekewa matarajio katika utekelezaji wa majukumu yake katika jamii mahsusi ambayo ni lazima ayatimize ikiwa ataafiki kaida za jamii yake kama mwanaume.

Fenistermaker (2002) anashikilia kuwa majukumu ya jinsia fulani hujenga taswira kuwa tofauti za kijinsia hujidhihirisha kama kiungo muhimu cha tabia za kijinsia. Majukumu ya mwanaume yanatarajiwa kudhihirisha tabia za kiume kulingana na jamii ya mhusika. Hii ina maana kuwa jinsi jamii inavyoendelea kukua kiuchumi, kihistoria, kitamaduni na kubadilisha mielekeo yake kuhusu uana, ndivyo mgao wa kazi wa kila jinsia unavyochukua mwelekeo tofauti. Jamii ya sasa inatilia mkazo usawa wa kijinsia na kwa sababu hii utafiti ulihitajika ili kudhihirisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika jamii ya sasa katika utanzu wa hadithi fupi.

Parsons (2004) aliunda muundo wa mfumo wa familia asili wa miaka ya 1995 uliopendelewa na jamii nyingi wakati huo. Alilinganisha mielekeo na mitazamo ya jamii kuhusu majukumu ya kiuana kwa undani. Pia, alifafanua mipaka ya majukumu ya kiuana. Muundo A, unaeleza jumla ya tofauti baina ya majukumu ya kike na ya kiume huku Muundo B ukielezea uvunjaji wa majukumu ya kiuana.

Mifano iliyotolewa imejikita katika tamaduni za Marekani.

**Mielekeo na Mitazamo ya Watu kuhusu Majukumu ya Kiuana**

| | **Muundo A** – tofauti za majukumu ya kiuana | **Muundo B** – mwingiliano wa majukumu ya kiuna |
|---|---|---|
| Elimu | Elimu mahsusi ya kijinsia-matarajio ya juu ya kitaaluma yalipewa wanaume na kutiliwa mkazo kama jambo muhimu kwao | Elimu bia, shule bia na masomo sawa kwa jinsia zote kisha uwezo sawa wa kimasomo na ujuzi kwa wanaume na kwa wanawake. |
| Taaluma | Kazi ya kitaaluma si jambo la kimsingi la mwanamke. Kazi na ukuaji wa kitaaluma huchukuliwa kama si jambo la maana kwa mwanamke. | Kazi na utaalamu ni muhimu kama ilivyo kwa mwanaume. Nafasi sawa ya kitaaluma ni muhimu kwa jinsia zote mbili. |
| Majukumu ya nyumbani | Kutunza nyumba na kulea watoto ni majukumu ya kimsingi ya mwanamke. Kuhusika kwa wanaume katika majukumu haya hakuhitajiki sana. | Kazi zote za nyumbani hufanywa na mume na mke katika familia. Hugawa shughuli za nyumbani bila kuzingatia jinsia. |
| Maamuzi katika familia | Iwapo kutatokea utata na | Hakuna mhusika katika |

| | | |
|---|---|---|
| | tofauti, mwanaume ndiye hutoa uamuzi wa mwisho. Kwa mfano, kuchagua mahali pa kuishi, shule za watoto na kuhusu vitu vya kununua nyumbani. | familia amepewa kipaumbele kutoa suluhisho na maamuzi katika familia, hadhi na nguvu hudumishwa tofauti zikizidi. |
| Ulezi wa watoto na elimu | Wanawake ndio hufanya malezi kwa kiwango cha juu, huwaelimisha watoto na kuwatunza kwa kila njia. | Wanaume na wanawake hugawa majukumu kwa kuzingatia usawa. |

Tafsiri yetu (2015)

Kutokana na mawazo ya Benjamin na mchoro huu wa Parsons, mtafiti anaweza kuorodhesha mihimili ifuatayo ya nadharia ya uana.

**Mihimili ya Nadharia ya Uana**

Mihimili ifuatayo ya nadharia ya uana iliongoza utafiti wetu;

(i) Mtu hazaliwi mke au mume lakini hufanywa kuwa hivyo na jamii anamokulia.

Mhimili huu ulitumika kuonyesha jinsi jamii inavyomkuza mwanaume kuanzia utotoni hadi anapoelewa anayopaswa kutekeleza kama mwanaume.

(ii) Majukumu ya kiuana ni mkururo wa matarajio ambayo mwanaume au mwanamke anapaswa kutekeleza katika jamii.

Mhimili huu ulitumiwa kubainisha kaida mbalimbali ambazo jamii anamokulia mwanaume zimemwekea katika kutekeleza kazi yake.

(iii) Majukumu ya kiuana hubandikwa na kulazimishwa kupitia ushawishi wa kijamii.

Mhimili huu ulibainisha mgao wa kazi ya kimapokeo ya mwanaume na jinsi ambavyo inakisiwa kumuathiri kama inavyojitokeza katika hadithi fupi teule.

(iv) Wazazi ndio waanzilishi wa athari ya majukumu matarajiwa ya jinsia ya watoto wao.

Mhimili huu ulitumiwa kuonyesha jinsi ambavyo mgao wa kazi za mwanaume umejengwa kuanzia mtoto anapokuwa mchanga na kupitishwa katika utu uzima. Nadharia ya uana ilifaa katika utafiti huu kuonyesha ujenzi na upokezi wa mgao wa kazi za kiuana zikiwemo za mwanaume. Nadharia hii haiwezi kuonyesha mabadiliko na mikinzano iliyopo baina ya mgao wa kazi za kimapokeo za mwanaume na mgao mpya katika hadithi fupi za Kiswahili. Nadharia ya upembuzi ilifidia pengo hili kwa kufafanua mikinzano hii.

### 1.6.2 Nadharia ya Upembuzi

Kwa mujibu wa kamusi ya Merriam Webster (2003), upembuzi ni utaratibu wa Hegel wa mabadiliko ambayo dhana au suluhu lake hupitia na hudumishwa na kusuluhishwa na mikinzano yake. Ni majadiliano ya hatua kwa hatua au ufafanuzi wa dhana yenye mikinzano ili kusuluhisha mikinzano hiyo. Neno upembuzi lina

asili yake katika Ugiriki wa Kale na lilipewa umahiri wake na Plato katika mijadala ya Kistoiki. Nadharia hii hutilia mkazo mikinzano baina ya watu au makundi mawili yenye mitazamo tofauti na ambayo yangetaka kudhihirisha ukweli wa jambo kupitia mijadala yenye mashiko. Hegel ambaye alikuwa mwanafalsafa wa Kijerumani katika karne ya kumi na tisa, aliona upembuzi kama ambao unahusu tasnifu na kusanisi. Alisema kuwa kitu cha kwanza kisichokuwa kikamilifu huitwa tasnifu.

Tasnifu ni hali asili ya kitu au jambo fulani kama vile mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Tasnifu hii haijakamilika wala haijajitosheleza. Hali hii huzalisha mikinzano ya ndani kwa ndani. Kukinzana kwa tasnifu huitwa tabaini. Migongano baina ya tasnifu na tabaini huzalisha kusanisi ambako hutokea mapema zaidi katika maendeleo ya kitu kinachozungumziwa na hivyo si kamilifu na hujiibukia mgogoro mwingine wa ndani kwa ndani ambao ni aina mpya ya tabaini.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa mgongano wa tasnifu na tabaini huendelea mpaka hali kamilifu na ya dhahania ya kitu ambayo ndiyo kamilifu kuliko zote inapopatikana. Mgao wa kazi za mwanaume ambao haujakamilika na hivyo kusanisi, hujenga tasnifu mpya tena. Hii tasnifu bado haijitoshelezi na huibua mgogoro mwingine wa ndani kwa ndani ambao ni aina mpya ya tabaini. Mwingiliano wa tasnifu na tabaini huzalisha kusanisi kwingine. Utafiti huu ulichunguza mgao huu wa kazi za mwanaume katika utanzu wa hadithi fupi ili

kusuluhisha migongano ya ndani kwa ndani ya mgao wa kazi za mwanaume katika jamii za Kiafrika zinazosisitiza usawa wa jinsia ambapo tofauti za kitabaka pia zinanuiwa kupunguzwa.

Katika mwaka wa 1847, Marx na Engels walitumia mawazo ya Hegel kuipa nadharia yao ya ukomunisti mashiko. Kazi hii ilichapishwa mwaka wa 1848. Kazi hii ina machapisho mengine ambayo yamechapishwa hivi karibuni. Chapisho ambalo limerejelewa katika utafiti ni la mwaka wa 2020. Kulingana na Marx (1873), tabaka la jamii hutoweka na lingine kuchipuka kwa sababu ya mapambano yanayotokea kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Marx anaendelea kusema kuwa kinachoendesha historia ni mapambano ya kitabaka baina ya wanyonyaji na wanyonywa. Kwa hivyo, inabidi kuwa na mapinduzi katika mifumo ya uzalishaji mali. Kazi ya Marx ya 1873 ndio kazi asili lakini imechapishwa mara nyingi kutoka mwaka wa 1873 hadi sasa. Chapisho ambalo limerejelewa katika sehemu ya marejeleo ni la 2004.

Mfumo wa kuumeni ulichangia katika uundaji wa matabaka kwa sababu ulimpa mwanamume nguvu zaidi kuliko mwanamke. Engels (1972) anasema kuwa jamii za kwanza za binadamu zilikuwa sahili, zilikusanya matunda, mizizi na kuwinda wanyama. Majukumu kati ya wanaume na wanawake yalitegemea umri na jinsia. Wanawake walichukua majukumu ya kinyumbani nao wanaume wakachukua majukumu ya kuchumia familia. Majukumu haya yalimfanya mwanamke

kunyenyekea na kumuona mwanamume kama mungu wake. Haya ni matabaka mawili yanayokinzana.

Baxter na Montgomery (1998) waliendeleza nadharia hii. Wanaamini kuwa nguvu zinazokinzana zimo na ndizo msingi wa uhusiano wowote wa kibinafsi na kuwa mikinzano baina ya nguvu zinazopingana huwa haina mwisho na haina suluhu bayana na la kudumu. Walitambua misingi miwili ya upembuzi ambayo ni ukinzano na utaratibu wa mambo. Ukinzano ni ushindani wa vitu viwili kama vile mgao wa kitamaduni na mgao mpya wa kazi za mwanaume. Msingi wa pili ni utaratibu wa mambo unaoshikilia kuwa upembuzi unaendelea na unakua. Wanaendelea kusema kuwa majukumu ya kiuana ni kitu kinachobadilika na husababisha mume na mke kufanya kazi pamoja.

Kwa mujibu wa Woods (1997), upembuzi ni madai kuwa kuna asili ya nguvu ambazo zina msukumo unaokinzana au upembuzi ni jinsi tunavyoathirika na kitu na kukipokea. Pia anasema kuwa ukinzano ni kugongana, kupingana au kushindana kwa vitu viwili. Mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili unaweza kudhihirisha hali ya upembuzi. Baada ya neno “usawa” kupigiwa debe katika jamii, lilipokelewa na kueleweka kwa njia tofauti. Usawa huu umesambaa hadi katika kazi za malipo ambapo hata wanawake wanashiriki katika kazi hizi na hivyo kuwa wakimu wa familia. Mabadiliko ya kiuchumi kama vile kuwapa wanawake nafasi sawa na wanaume katika kazi mbalimbali ili kuonyesha usawa yanaleta ukinzano hasa pale ambapo mtu

anahitajika kutekeleza majukumu ambayo awali yalidhaniwa kuwa ya jinsia tofauti.

Anderson (2002.350) anasema kuwa upembuzi huchunguza jinsi uhusiano hujengeka kutoka kwa nguvu mbili zinazokinzana. Pia huchunguza jinsi ambavyo wanaowasiliana hutetea jumla ya mambo yanayoendelea kubadilika kila mara kutokana na maendeleo na mikinzano ya ndani kwa ndani ya jamii kiuchumi, kihistoria na kisiasa.

Wamitila (2002) anasema kuwa tendo la kwanza la kihistoria ni kutafuta njia za kuyakidhi mahitaji ya kimsingi. Ili kufanikiwa, wanadamu hujiunga pamoja na kuunda umoja ili kuimarisha ubora na wepesi wa kuizalisha mali ya kukidhi mahitaji yao. Historia huendelea kutokana na mfulululizo-safu wa mkinzano wa mawazo. Matokeo ya mkinzano huo ni kuzuka kwa hatua nyingine mpya ya kihistoria ambayo ndiyo msingi wa upembuzi wa kiyakinifu. Mawazo ya wanawake kuhusu mgao wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi za Kiswahili yanazua mkinzano wa ndani kwa ndani ambao ndio kichocheo cha utafiti huu.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa Marx alimpa binadamu tumaini la kung'oa mizizi yote ya unyonyaji na unyanyasaji na kujenga ulimwengu wa kijonzi usiokuwa na madhila. Jamii ya sasa inatilia mkazo usawa wa kijinsia na utendakazi sawa wa wanajamii wote. Kazi za wahakiki wa kiufeministi kama vile Woolf, Simone na Wollstonecraft zilikuwa na mchango mkubwa katika kuanzisha harakati za ukombozi wa mwanamke. Walipigania usawa ambapo mwanamke

anachukua nafasi sawa na mwanaume katika jamii. Kupitia udurusu wa kina inaelekea kuwa, sasa mwanamke anachangia katika kukimu familia jambo ambalo awali lilikuwa likifanywa na mwanaume.

Fasili zote za upembuzi zinatilia mkazo mambo sawa muhimu: nguvu zinazokinzana na jinsi ambavyo watu wanaathirika nazo. Usomaji wa upembuzi unaweza kusaidia waandishi wa hadithi fupi za Kiswahili kusawiri wahusika wa kiume ambao wanatekeleza kazi zao mpya kama jambo la kawaida. Kama asemavyo Woods (1997), nadharia ya upembuzi inachukulia mabadiliko kama jambo la kawaida na linalopatikana kila mara katika uhusiano wowote kama vile mgao wa kazi za kiuana. Humwezesha mtu kuyachukulia mabadiliko kwa njia chanya na kushughulikia mikinzano au migogoro kwa mtazamo bora.

Lengo la fikra za upembuzi ni kusuluhisha mikinzano kirazini na hatimaye kutafuta ukweli. Kusuluhisha mambo kirazini ni kuzua mjadala na kuthibitisha ukweli wa kauli kulingana na mantiki. Njia moja ni kuonyesha kuwa tasnifu husababisha mkinzano na kulazimisha kusanisi. Njia nyingine ni kuzua dhanio la kutosheleza kwa tasnifu na tabaini na kwa njia hii kuleta mkinzano mwingine wa ndani kwa ndani. Mkinzano huu huzalisha kusanisi kwingine ambako huzua aina nyingine ya tabaini.

Kutokana na mawazo ya Hegel tunaweza kuorodhesha mihimili mitatu ya nadharia hii itakayosaidia katika utafiti huu.

**Mihimili ya Nadharia ya Upembuzi**

Mihimili mitatu ifuatayo ya nadharia hii ilitufaa katika utafiti wetu:

(i) Kila kitu kinapita na kina kikomo kinachopatikana kipindi fulani cha wakati. Katika mpito wa wakati kitu fulani hubadilika na kuwa kingine kinachohusiana nacho. Kitu kipya huzuka ambacho ni kikamilifu kuliko cha asili. Hali hii ya ukinzani huendelea hadi kitu kikamilifu zaidi kinapopatikana.

Mhimili huu ulifafanua mgao wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Mtafiti alivisoma vitabu vya diwani za hadithi fupi zilizoteuliwa na machapisho mengine ili kubainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili kama utanzu unaoshughulikia masuala ibuka katika jamii kama ulivyo mgao wa kazi za mwanaume.

(ii) Kila kitu kimeundwa kwa hali mbili kinzani.

Mgao wa kazi za kiuana kwa jumla umeundwa kwa hali ambayo inaashiria mikinzano katika utekelezaji wake. Ikiwa mgao wa kazi za mwanaume ambaye anapatikana katika jamii ambayo imepitia mabadiliko mengi hasa kiuchumi unachukua mkondo mwingine ili kuakisi mabadiliko katika jamii, kuna uwezekano kuwa utekelezaji wa mgao huu katika jamii ya kisasa utakinzana na matarajio ya jamii yake.

(iii) Mabadiliko ya hatua kwa hatua husababisha mikinzano na kufikia ukamilifu wake wakati nguvu moja hushinda nguvu kinzani na kusababisha mabadiliko kamilifu.

Mhimili huu ulitumika kuchunguza hatua ambazo mgao wa kazi za mwanaume zilikisiwa kupitia ili kuendana na zile za mwanamke. Pia ulitumika kutambua mikinzano katika utekelezaji wa kazi za mwanaume katika jamii za kisasa.

Nadharia ya upembuzi ilitufaa katika kuonyesha mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume katika utanzu wa hadithi fupi teule za Kiswahili kama utanzu wa kisasa unaoshughulikia masuala ibuka kama vile mgao mpya wa kazi za mwanaume.

### 1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Hadithi fupi za Kiswahili ni utanzu wa fasihi andishi ambao umekua kuanzia Karne ya ishirini kama asemavyo Mbuthia (2010). Kufikia miaka ya 1960 hadithi fupi za Kiswahili zilianza kutokeza magazetini hasa katika nchi ya Tanzania. Kukua kwake kunadhihirika kupitia mikusanyiko mingi ya hadithi zinazopatikana kote Afrika Mashariki hasa katika maeneo ambamo Kiswahili huzungumzwa (MCOnyango, 2006). Hawa wameshughulikia ukuaji wa hadithi fupi hadi kufikia kuitwa hadithi fupi za kisasa. Tafiti hizi zilitufaa kuonyesha utanzu wa hadithi fupi kama utanzu mwafaka wa kuwasilisha mgao mpya wa kazi za mwanaume kama suala ibuka katika jamii. Tafiti hizi zinatofautiana na utafiti huu kwa sababu zimejifunga katika utoaji wa maelezo kuhusu ukuaji wa hadithi fupi bali utafiti wetu umeshughulikia mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi teule za Kiswahili.

Gitau (2005) alishughulikia unyanyasaji dhidi ya mwanaume katika utanzu wa tamthilia na riwaya. Alidhamiria kuainisha namna mbalimbali za unyanyasaji huo kwa kuchanganua waandishi wa kike na wa kiume wa tamthilia na riwaya. Alitumia nadharia ya umuundo-utekelezi. Utafiti wake ulikuwa wa kimaelezo na ulifanyiwa maktabani. Matokeo ya utafiti wake ni kuwa wanaume hukabiliwa na unyanyasaji wa kutukanwa na wake zao kwa kushindwa kutekeleza majukumu ya kukimu familia na kuilinda. Pia, alipata kuwa wanaume wengi hukimbia majukumu yao na kuwaachia wanawake majukumu yote ya malezi ya watoto.

Wengine huingilia ulevi wakitegemea wake zao wawalishe na kuwatunza kwa njia zote jambo ambalo huleta mfarakano.

Utafiti wa Gitau (2005) umeshughulikia suala la unyanyasaji dhidi ya wanaume katika riwaya na tamthlia za Kiswahili. Unatofautiana na wetu kwa sababu tumeshughulikia mgao mpya wa kazi za mwanaume katika utanzu wa hadithi fupi za Kiswahili. Aidha, nadharia yake ni umuundo - utekelezi nasi tumetumia nadharia ya uana na nadharia ya upembuzi. Mawazo ya Gitau yalitusaidia kutilia mkazo mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume ambapo baadhi ya kazi hizi zimetwaliwa na mwanamke. Pia, utafiti wetu umeshughulikia suala la kijinsia kama ulivyo wa Gitau.

Sanja (2011) anashikilia kuwa, malighafi ya hadithi fupi sawia na tanzu zingine ni jamii. Hadithi fupi kwa hivyo zinazungumzia mambo ambayo yamechotwa katika jamii na husemwa kisanaa. Sanja alikuwa akitoa maana ya hadithi fupi katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine.* Jamii za Kiafrika zimeujenga mgao wa kazi za kila mwanajamii kwa kuegemea mfumo wa kuumeni. Hata hivyo, jamii hizi zimepitia mabadiliko katika utendakazi wake ambapo mgao wa kazi za wanajamii mbalimbali unaelekea kushabihiana kutokana na mfumo wa viwandani kuchukua nafasi kubwa katika jamii za Kiafrika. Sasa, wanaume na wanawake wanashiriki katika kazi za kulipwa. Mgao wa kazi za mwanaume unakisiwa kuwa umebadilika. Kwa sababu hii, hadithi fupi za Kiswahili kama utanzu wa kisasa zinachota maudhui kama haya kutoka kwa jamii

halisi na kuyawasilisha kisanaa.

Connell (1987) alifanya utafiti kuchunguza kama kuna uhusiano baina ya biyolojia na majukumu ya kiuana. Alitumia nadhraria ya majukumu ya uana. Alibainisha kuwa nadharia ya majukumu ya uana na mwingiliano wa kijamii husababisha mabadiliko ya kisiasa; ikiwa mwingiliano wa kijamii na tajriba kandamizi zinaweza kubadilisha utaratibu, basi zinaweza kubadilisha tabia za wanaume na wanawake.

Matokeo ya utafiti wa Connell (1987) ni kuwa hakuna uhusiano baina ya biolojia na majukumu ya uana. Pia, wanawake na wanaume kujikita kwa taaluma sawa, madaraka na kazi sawa kunaashiria kuwa jinsia aliyozaliwa nayo mtu haina uhusiano wa moja kwa moja na uwezo wa mtu. Ingawa kuna tofauti katika maumbile ya jinsia tofauti kama vile nguvu za kimwili, uwezo wa kufanya majukumu mbalimbali hujikita kwa uwezo unaohitajika kufanya jukumu fulani ambalo limepewa jinsia mahsusi. Utafiti huu unatofautiana na wetu kwa sababu tumetumia nadharia mbili tofauti na yake. Utafiti wake ulishughulikia suala la uana kama vile wetu ingawa mada zilizoshughulikiwa ni tofauti.

Osore (2008) katika tasnifu ya uzamifu alifanya utafiti kuhusu kinaya katika riwaya za Euphrase Kezilahabi na Said Ahmed Mohamed. Alitumia nadharia ya tahakiki usemi (critical discourse analysis). Matokeo ya utafiti wake ni kuwa kutoka utotoni mafunzo katika jamii yalijikita katika uana. Wanaume walichukuliwa kuwa ‘Kichwa’ cha familia. Walipewa majukumu ya kutimiza

mahitaji ya wake na watoto wao. Ili kutimiza haya, walijihusisha na kilimo na uvuvi. Majukumu ya wanawake yalikuwa ya kufagia boma, kupika, kuosha vyombo na nguo na kufuma mikeka. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu unashughulikia maudhui ya kinaya kwa kutumia nadharia ya tahakiki usemi huku utafiti wetu ukibainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa kutumia nadharia ya uana na nadharia ya upembuzi. Matokeo ya utafiti wa Osore yalitufaa kuangalia upya majukumu ya mwanaume kama alivyopendekeza.

Scanzoni (1979) katika kazi yake *Strategies for Changing Male Family Roles* anasema kuwa katika miaka ya hamsini usomi wa familia ulijikita katika tamaduni mbili ambazo zilichukulia majukumu ya wanawake na wanaume kama ambayo hayawezi kubadilika. Kazi yake ilikusudia kuangazia hatua tatu ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kuleta mabadiliko katika majukumu ya familia ya mwanaume. Hatua ya kwanza aliita uungwana ambapo mtu hutenda mambo kwa manufaa ya wengine. Mwanaume anabadili majukumu yake kwa sababu ni haki, adilifu na sahihi. Anashiriki katika majukumu ili kuleta ufanisi katika familia.

Hatua ya pili ni mbinu ya upendeleo au ubinafsi. Katika hatua hii wanaume hubadili majukumu yao kwa sababu watafaidika kutokana na mabadiliko hayo. Kwa mfano, mwanamke anapochukua jukumu la kukimu familia atamuauni mwanaume jukumu hili zito na kufanikisha ufanisi wa familia. Hatua ya tatu ni kupitia majadiliano. Kwenye hatua hii, mwanaume na mwanamke hujadiliana kuhusu mabadiliko katika majukumu yao.

Utafiti wa Scanzoni unahusiana na wetu kwa sababu unashughulikia majukumu ya mwanaume kama ulivyo wetu. Unatofautiana na wetu kwa kuwa, wake unatambua mbinu za kuyabadilisha majukumu ya familia ya mwanaume huku wetu ukibainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume, kuchanganua sifa za wanaume wanaochukua mgao mpya wa kazi na kuchunguza athari za kuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili.

Wilbon na Simpson (2009) walichunguza historia na utamaduni wa jukumu la kutunza watoto. Walikusudia kuwasaidia wanawake kuwahusisha wanaume katika jukumu la kutunza watoto na kuyarithisha kwa wasichana na wavulana wao. Wilbon na Simpson wanashikilia kuwa kupitia kwa ufasili barabara wa kitu, kitu hicho hupata maana yake na umahiri. Hivi ni kusema kuwa, jinsi jamii inavyofasili na kutoa maana ya kitu fulani, kitu hicho hupata maana kulingana na muktadha husika. Walisisitiza utoaji wa maana mpya ya majukumu ya mwanaume. Mawazo haya yalitusadidia katika ufafanuzi wa mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume.

Utafiti wa hivi karibuni wa Dunleavy (2007) katika *A Woman's Nation Changes Everything* alichunguza ongezeko la wanawake viwandani. Anatueleza kuwa sasa mpaka asilimia 48% ya wafanyikazi wa Marekani ni akina mama. Pia anaeleza kuwa familia ambazo zina mwanamke kama mchumaji wa kimsingi ziliongezeka kutoka asilimia 4.1 hadi zaidi ya asilimia 7 kutoka mwaka wa 1970 – 2000 na mpaka sasa zinaendelea kuongezeka. Aidha, thuluthi moja ya wanawake hupata

mapato makubwa kuliko waume zao. Wanashiriki katika kuyakimu mahitaji ya jamii au wao ndio hutegemewa hasa na familia zao kuwapa mkate wa kila siku katika jamii nyingi. Utafiti huu ulitusaidia kuonyesha mabadiliko ya jukumu la kukimu familia kama jukumu asili la mwanaume. Utafiti huu ni tofauti na wetu kwa sababu ulishughulikia ongezeko la wafanyi kazi wa kike katika jamii za Marekani huku wetu ukiainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Kibutu (2013) alifanya utafiti kuhusu "Maudhui ya Mitindo ya Lugha inayotumiwa kuwasilisha mafunzo ya kukuza vijana katika misingi ya kiuana". Utafiti wake uliongozwa na nadharia ya semeotiki. Anasema kuwa, wanaume walitarajiwa kutekeleza majukumu ya kuwinga, kutoa uamuzi, na masurufu na kuleta chakula. Jamii zinaweza kupitia mabadiliko mengi mpaka kuyalazimu majukumu ya kiuana kubadilika kwa kiwango kikubwa. Kibutu alitumia nadharia ya semeotiki katika utafiti wake na kutambua majukumu ya kitamaduni ya mwanaume lakini utafiti wetu umetumia nadharia ya uana na nadharia ya upembuzi kuainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa kuegemea utanzu wa hadithi fupi.

Mgao mpya wa kazi za mwanaume uliainishwa, kuelezwa na kuchanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti ili kuleta mwongozo mwafaka kwa wasomi wakereketwa wa fasihi andishi ya Kiswahili katika kuliangazia suala zima la mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume. Ugawaji wa nyadhifa mbalimbali katika hadithi fupi za Kiswahili utachukua mwelekeo mpya wa kuafiki matakwa

ya usawa wa kijinsia. Good na Wood (1995) wanasema kuwa mara nyingi majukumu haya na nyadhifa hazigawanywi kwa misingi sawa ya kijinsia na hii ndio sababu wanaume na wanawake hunga'ang'ana kuhusu ni majukumu yapi na tabia gani zinakubalika kuafiki mwanaume au mwanamke.

Nadharia ya uana na nadharia ya upembuzi zilifaa katika kubainisha ujenzi wa kitamaduni wa mgao wa kazi za mwanaume na mabadiliko ambayo mgao huu ulikisiwa kuwa umepitia kutokana na mabadiliko katika jamii anamoishi mwanaume. Utanzu wa hadithi fupi teule za Kiswahili ulitufaa kuangazia mgao mpya wa kazi za mwanaume kama suala ibuka kwani ni utanzu wa kisasa ambao huyashughulikia masuala ibuka katika jamii.

### 1.8.0 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii ilishughulikia muundo wa utafiti, uteuzi wa sampuli, ukusanyaji wa data, uchanganuzi na uwasilishaji wa data.

### 1.8.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa aina ya kimaelezo. Mugenda (1999) anasema kuwa utafiti wa kimaelezo hutafuta uelewaji wa tabia za binadamu na sababu ambazo hutawala tabia hizo na hauhusishi takwimu lakini data huwa katika mfumo wa maandishi. Tabia za binadamu kama utekelezaji wa mgao mpya wa kazi za mwanaume zinaweza kuelezewa vizuri kwa kutumia utafiti wa kimaelezo. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani; maktaba ya Chuo Kikuu cha Kenyatta na cha Nairobi. Maktabani, mtafiti alisoma maelezo ya kimsingi kuhusu masuala ya nadharia, hadithi fupi, uchanganuzi na tafiti kuhusu mgao wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili.

Pia, mtafiti alisoma tasnifu, vitabu, majarida, mtandao na makala mbalimbali yenye data hiyo. Isitoshe, alisoma na kuhakiki kazi za watunzi wa hadithi fupi ziliozoteuliwa ili kuainisha mgao wa kazi za mwanaume. Haya yalitufaa katika utafiti huu katika kujenga hoja za mtafiti kwa upande wa nadharia, mbinu za kukusanya data, uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti.

### 1.8.2 Uteuzi wa Sampuli

Uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimakusudi. Sampuli ya kimaksudi ilitumiwa kwa sababu maalum za kitafiti na kiuchunguzi za mtafiti. Mugenda (2013) anasema kuwa, uteuzi wa sampuli kimaksudi ni mbinu ambayo humruhusu mtafiti kuchagua sampuli itakayompa data anayohitaji kulingana na malengo ya utafiti wake. Sampuli iliyochaguliwa ni hadithi ambazo zimeangazia suala la mgao mpya wa kazi za mwanaume. Vitabu vilivyolengwa ni diwani za hadithi fupi ambazo zimechapishwa kuanzia mwaka wa 2000-2013. Hiki ni kipindi ambacho utanzu wa hadithi fupi umeshughulikiwa kwa kina ukilinganishwa na kipindi cha miaka ya tisini.

Pia, katika kipindi hiki cha 2000-2013, falsafa za watu kuhusu mgao wa kazi zimechukua mwelekeo tofauti kutokana na mikataba ya usawa wa kijinsia na haki za wanawake. Mtafiti alisoma hadithi zote kwa kuangalia wahusika wa kiume wote. Baadaye alichagua wahusika wa kiume wanaofanya kazi za kike kama vile kupika na kufua nguo. Hadithi ambazo zimesawiri wahusika wa kiume wanaofanya kazi hizi za kike ziliteuliwa kutoka kwenye diwani tatu zilizoteuliwa. Hadithi nne kutoka kwenye diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* tatu kutoka kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* na tatu kutoka kwenye diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* ziliteuliwa.

### 1.8.3 Ukusanyaji wa Data

Data ambayo ni mgao mpya wa kazi za mwanaume ilikusanywa kutoka kwa diwani tatu zilizoteuliwa. Kutoka katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine,* hadithi za "Dr. Strese" ya (Sheila Ali Ryanga), "Uganga wa Pete" ya (Ayubu Mukhwana) na "Macheo Mengine" ya (Kitula King'ei) zilisomwa. Katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, hadithi nne zilichaguliwa. Hadithi ya "Mke Wangu" ya (Muhammed Said Abdulla), "Kikaza" ya (Robert Oduori), "Ndoa ya Samani" ya (Omar Babu) na "Maeko" ya (Mohamed Khelef) zilihakikiwa. Kutoka kwenye diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* hadithi tatu ziliteuliwa. Hadithi ya "Kachukua Hatua Nyingine" ya (K. W. Wamitila), "Mayai Waziri wa Maradhi" ya (E. Kezilahabi) na "Fumbo la Mwana" ya (Sinjiri Mukuba) zilisomwa. Kwa jumla, hadithi kumi zilisomwa kwa kina ili kupata mgao mpya wa kazi za mwanaume. Katika kila diwani, mtafiti alisoma hadithi zote na hatimaye akateua zile ambazo zinaonyesha mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Aidha, alibainisha na kuainisha mgao wa kazi za mwanaume ambao umebadilika. Hadithi ambazo zilidhirisha mgao mpya wa kazi za mwanaume zilisomwa huku kazi ambazo ziliashiria mabadiliko zikiorodheshwa na kupangwa ili kuchanganuliwa. Kadhalika, alichanganua sifa za wanaume ambao wanauchukua mgao mpya wa kazi na kuchunguza athari za mgao huu kwa mhusika mwanaume.

Magazeti, majuzuu, tasnifu mbalimbali na vitabu vingine ambavyo vinagusia mada hii pia vilisomwa.

### 1.8.4 Uchanganuzi wa Data

Mgao mpya wa kazi za mwanaume kutokana na usomaji wa vitabu teule ulichanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini. Carney (1969) anasema kuwa uchanganuzi matini ni mbinu ya utafiti ambapo mtafiti hupanga data kulingana na mada fulani ya utafiti. Mada hizi hujumuisha mambo ambayo yamo ndani ya matini na ambayo mtafiti anaweza kubainisha maana yake kutokana na matini yanayoshughulikiwa. Mtafiti hugawa mada katika vijisehemu vidogo vidogo vinavyoweza kufasiriwa kwa urahisi. Wamitila (2008) anasema kuwa kufasiri kunahusisha kitendo cha kuchunguza na kueleza maana ya mwandishi au maana ya kazi ya kifasihi.

Mtafiti aliainisha mgao wa kazi za mwanaume zilizobadilika na kuzipanga kwa utaratibu ili kuonyesha jinsi ambavyo hadithi teule zimeuangazia. Uchanganuzi uliongozwa na maswali na malengo ya utafiti kuonyesha namna mgao wa kazi mpya za mwanaume unavyoangaziwa katika kazi za kisasa za fasihi. Mihimili ya nadharia ya uana na nadharia ya upembuzi ziliongoza utafiti huu kwa kuzingatia hadithi fupi teule. Matokeo ya uchanganuzi yameandikwa kinathari.

### 1.8.5 Uwasilishaji wa Data

Baada ya data kukusanywa na kuchanganuliwa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini, iliwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Mtafiti alibainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule kwa njia ya maelezo. Pia, sifa za wanaume wanaochukua mgao mpya wa kazi zilichanganulia kwa njia ya maelezo. Hatimaye, athari za kuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume zilichunguzwa na kuwasilishwa kwa maelezo.

### 1.8.6 Hitimisho

Sura hii imejadili mambo ya kimsingi ya utafiti yakiwemo usuli, suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti. Sura ya pili imeshughulikia kazi anazofanya mhusika wa kiume kwa kuegemea hadithi teule kutoka kwenye diwani zilizoteuliwa.

# SURA YA PILI

## Mgao Mpya wa Kazi za Mwanaume Katika Hadithi Fupi Teule

### 2.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilijenga msingi wa utafiti huu kwa kuangazia usuli na suala la utafiti, maswali na malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka, misingi ya nadharia, yaliyoandikwa kuhusu mada na mbinu za utafiti.

Lengo la sura hii ya pili ni kubainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za diwani za *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* na *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine.* Sura hii imefafanua mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi zilizoteuliwa kimakusudi kutoka kwenye diwani tatu zilizoteuliwa. Mgao mpya wa kazi za mwanaume katika utafiti huu unarejelea kazi ambazo mwanaume anatekeleza sasa kinyume na kazi zake za kitamaduni. Kazi hizi ni kama vile kupika, kuosha nguo na kulea watoto. Kibutu (2013) anasema kuwa wanaume walitarajiwa kutekeleza majukumu ya kutoa uamuzi na kuleta chakula katika familia zao. Kulingana na kauli hii ya Kibutu, kazi ya kufanya uamuzi na kukimu mahitaji ya familia ni kazi asili ya mwanaume.

Gitau (2005) anasema kuwa majukumu ya mwanaume yaliundwa na jamii zinazoendelea kubadilika kwa kuegemea misingi ya kijinsia. Misingi hii ilitumiwa katika mgao wa kazi za kila mwanajamii. Kulingana na kauli hii ya Gitau (2005),

jamii za Kiafrika zinaendelea kubadilika ili kuafiki usawa wa kijinsia. Kwa hivyo, jinsi mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa yanavyotokea katika jamii za Kiafrika ndivyo kazi wanazofanya zinavyobadilika ili kuoana na usawa wa kijinsia. Hii ina maana kuwa mwanaume anaweza kufanya kazi ambazo awali zilichukuliwa kuwa za kike na mwanamke kufanya kazi zilizochukuliwa kuwa za kiume ili kuafiki usawa wa kijinsia.

Mtafiti ameonyesha jinsi suala la mgao mpya wa kazi za mwanaume limeshughulikiwa na waandishi wa hadithi zilizoteuliwa. Data ambayo imechanganuliwa katika sura hii ni mgao wa kazi za mwanaume kwa msingi wa ushirikiano na mwanamke kwa kuzingatia usawa wa kijinsia. TUKI (2013) wanasema kuwa ushirikiano ni hali ya kuungana na kusaidiana katika jambo; uelewano, changamano, tangamano, fungamano. Katika utafiti huu ushirikiano ni hali ya mwanaume na mwanamke kuungana na kusaidiana kufanya kazi ambazo kitamaduni zilifanywa na jinsia moja hasa ya kiume. Pia tulichanganua mgao wa kazi unaonyesha kuwa yale mwanaume anayofanya sasa ni kinyume na yale alikuwa akifanya zamani.

Mbinu ya uchanganuzi matini ilitumiwa kuchanganua data katika utafiti huu. Kama ilivyosemwa awali katika utafiti huu, Carney (1969) anasema kuwa uchanganuzi matini ni mbinu ya utafiti ambapo mtafiti hupanga data kulingana na mada fulani ya utafiti. Mada hizi hujumuisha mambo ambayo yamo ndani ya matini na ambayo mtafiti anaweza kubainisha maana yake kutokana na matini

yanayoshughulikiwa. Mtafiti hugawa mada katika vijisehemu vidogo vidogo vinavyoweza kufasiliwa kwa urahisi. Mgao mpya wa kazi za mwanaume uligawa katika vijisehemu vidogo vidogo vyenye uhusiano fulani. Kisha mtafiti aliorodhesha kazi zote anazofanya mwanaume kutoka kwenye diwani za hadithi fupi anazoshughulikia kwa kuegemea vijisehemu hivyo.

Mgao mpya wa kazi za mwanaume ulibainishwa katika vijisehemu viwili. Katika kijisehemu cha kwanza mgao wa kazi za mwanaume ambao unaonyesha kuwa mwanaume na mwanamke wanashirikiana katika ugawaji na utendaji wa kazi hizo ulishughulikiwa. Katika kijisehemu hiki, mtafiti alijadili mgao mpya wa kazi za mwanaume ambapo mwanaume anafanya kazi mbalimbali sasa kwa kushirikiana na mwanamke kinyume na ilivyokuwa katika mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Ushirikiaono katika ugawaji wa kazi za mwanaume unaashiria ukinzano baina ya mgao mpya wa kazi za mwanaume na mgao wa kitamaduni kwa sababu yale anayofanya mwanaume ni tofauti na yale aliyoyafaya awali. Aidha, mtafiti alijadili kila kazi kwa kuchukua mifano kutoka kwenye hadithi zilizoteuliwa kimaksudi. Wahusika wanaofanya kazi hizi ambazo zimechukua mkondo mpya kutoka kwenye hadithi zenye data hiyo waliangaziwa kwa kina.

Katika kijisehemu cha pili mgao wa kazi za mwanaume ambao unaonyesha kuwa yale anayoyafanya mwanaume ni kinyume na kazi zake katika mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume ulishughulikiwa. Mtafiti alizichukua kazi ambazo zilionyesha kuwa yale anayoyafanya mwanaume ni kinyume na yale

aliyokuwa akiyafanya katika mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Kazi hizi zilifafanuliwa kwa kuchota mifano kutoka kwenye hadithi zinazoangazia kazi hizi. Hata hivyo, kuna aina moja ya kazi ambayo ilijitokeza katika vijisehemu vyote viwili. Kazi hii ni ile ya kushauri. Kazi hii ilijitokeza katika kazi ambazo mwanaume anafanya kwa kushirikana na mwanamke na pia kazi ambazo mwanaume anafanya kinyume na mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume.

Parson (2004) anasema kuwa katika mgao wa awali wa kazi, kazi za kitaaluma zilifanywa na wanaume. Wanawake hawakuhusika katika kazi za kitaaluma kama walivyohusika wanaume. Kazi za wanawake zilikuwa kutunza nyumba, kulea watoto na kufanya kazi zote za nyumbani. Kwa hivyo, wanawake ndio waliofanya malezi ya watoto na kuwafunza mambo mbalimbali huku wanaume wakitoa uamuzi katika masuala tata kwenye familia. Parson (2004) anaendelea kusema kuwa katika mgao mpya wa kazi za mwanaume, wanaume na wanawake wanapata elimu bia na uwezo sawa wa kimasomo na ujuzi katika kazi za kitaaluma. Kwa hivyo, usawa unaojidhihirisha katika upataji elimu na ujuzi wa kazi unatarajiwa pia katika mgao wa kazi.

Parson anaeleza kuwa kazi zote za nyumbani katika mgao mpya wa kazi za mwanaume hufanywa na mwanaume na mwanamke bila kuzingatia jinsia. Pia, kila mhusika awe mwanaume au mwanamke anahusika katika kutoa suluhisho na maamuzi kwenye familia. Parson katika maelezo yake anasema kuwa wanawake na wanaume hugawa kazi kwa kuzingatia usawa. Kwa hivyo kazi zote zinafanywa

na wanaume na wanawake bila kubagua. Kwa mujibu wa kauli hii ya Parson (2004) tunaweza kusema kuwa mwanaume sasa anafanya kazi ambazo awali zilichukuliwa kuwa za kike. Wanawake pia wanashiriki kazi ambazo zilichukuliwa kuwa za wanaume.

Perry na Crouter (1990) wanasema kuwa wanaume na wake zao wanafanya bidii kusawazisha jukumu la kuwa mkimu familia wanapofanya kazi za nyumbani. Wanaendelea kusema kuwa, kwa miaka kumi na mitano iliyopita, kumekuwa na ongezeko kubwa la wanawake walioolewa kwenye viwanda wakifanya kazi za ajira. Kutokana na ongezeko la wanawake kwenye viwanda, idadi ya wanawake wanaoshiriki jukumu la kukimu familia imeongezeka. Haya yamesababisha mabadiliko katika kazi ya kukimu familia ambayo tulilitambua awali kama kazi ya kitamaduni ya mwanaume. Kutokana na mabadiliko ya kazi za kiuchumi zinazoegemea jinsia, tunajiuliza; wanaume wameuchukua mgao wa kazi mpya? Ili kufanikisha kazi hii, mtafiti aliangalia hadithi mbalimbali ambazo zimesawiri wanaume wanaofanya kazi ambazo zinaafiki mgao mpya wa kazi za mwanaume. Hadithi ambazo zilihakikiwa zilionyesha wanaume ambao wanafanya kazi ambazo awali zilifanywa na wanawake.

Masinde (2003: 32) anasema kuwa mtunzi wa fasihi sawa na fasihi yenyewe, ni zao la mazingira maalum katika kipindi maalum cha historia ya jamii. Kipindi cha wakati cha msanii huathiri jinsi anavyouona na kuusawiri ulimwengu wake. Hii ina maana kuwa msanii husawiri wahusika ambao wanafanya yale yanayoendana

na mazingira yanayomzunguka kwa wakati fulani maalum. Kipindi ambacho waandishi wa hadithi zilizoteuliwa wameaandika kazi zao ni kipindi ambacho kimeshuhudia mikataba mingi kuhusu suala la usawa wa jinsia na utetezi wa haki za wanawake.

Kama tulivyotaja katika ukurusa wa tatu, kumekuwa na mikataba ambayo ni mazao ya mikutano mbalimbali ya kimataifa iliyofanywa kutetea haki za mwanamke na usawa wa kijinsia. Mikutano hii ni pamoja na WCIWY 1975, WCUND*: Equality (*1980), TTWCW (1985) na FWWC *(1995).* Maafikiano ya mikutano hii ni kuwa na usawa wa kijinsia katika nyanja mbalimbali za maisha. Kutokana na mikataba hii, taswira ya unyanyapaa wa wanawake imebadilika kwani sasa wanafanya kazi zenye hadhi sawa na wanaume.

King'ei (2000: xv) anasema kuwa maudhui ya fasihi yoyote huzalika kutokana na hali ya jamii ilivyo kwa wakati wake. Hivyo, mabadiliko yanapotokea katika nyanja zote za maisha hayakosi kamwe kuwaathiri watunzi. Athari hizo ndizo zinazowapa hamu ya kuumba wahusika wa kifasihi wanaoonyesha mabadiliko haya. Adler (1993) anasema kuwa wasichana hufunzwa kutilia maanani majukumu ya kijamii na hutarajiwa kujifunza majukumu ya jikoni kama vile kupika na kutafuta kuni. Kwa hivyo, kazi ya kupika ni kazi ya kitamaduni ya mwanamke. Wahusika ambao wameuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi zilizoteuliwa wanadhihirisha athari za kiwakati katika kazi za

watunzi.  Kipindi cha wakati ambacho kimehusishwa katika utafiti huu ni cha mwamko wa usawa wa kijinsia hasa mgao wa kazi za mwanaume.

### 2.1 Mgao wa Kazi za Mwanaume katika Hadithi Fupi Teule

Katika sehemu hii, mtafiti amebainisha mgao wa kazi mpya za mwanaume katika hadithi fupi teule.  Haya yamejitokeza katika vitengo viwili.  Katika kitengo cha kwanza, mtafiti alishughulikia mgao wa kazi za mwanaume ambao ni kinyume na mgao wa kitamaduni.  Kazi ambazo wanaume wanafanya kinyume na ilivyokuwa katika mgao wa kitamaduni zimejadiliwa pamoja huku mifano mwafaka kutoka kwenye hadithi zilizoteuliwa ikitolewa.  Kitengo cha pili kimeshughulikia mgao wa kazi za mwanaume kwa kuzingatia ushirikiano. Mgao wa kazi za mwanaume ambao unabainisha mabadiliko kwa kushirikiana na wanawake kufanya baadhi ya kazi ulishugulikiwa katika sehemu hii.  Utafiti huu umeshughulikia mgao wa kazi za mwanaume kinyume na mgao wa kitamaduni kwanza.

### 2.2 Mgao wa Kazi za Mwanaume Kinyume cha Mgao wa Kitamaduni

Kwenye sehemu hii, mtafiti alibainisha mgao wa kazi za mwanaume ambao ni kinyume cha mgao wa kitamaduni.  Kwa mujibu wa Engels (1972) jamii za kwanza zilikuwa sahili, zilikusanya matunda, mzizi na kuwinda wanyama. Majukumu kati ya wanawake na wanaume yalitegemea umri na jinsia. Wanawake walichukua kazi za kinyumbani nao wanaume wakachukua kazi za kuchumia familia.  kazi za kinyumbani katika muktadha huu ni kama vile kupika, kuosha nguo na kunadhifisha boma.

Kadhalika, kazi za kuchumia familia ni kazi ambazo zinaleta mapato yanayoweza kukimu mahitaji ya familia. Kazi hizi ni kama vile kufanya biashara na kazi ya kilimo. Jamii nyingi za Kiafrika ziligawa kazi kulingana na jinsia ya kila mwanajamii huku kila mwanajamii akifunzwa kazi anazotarajiwa kutekeleza tangu utotoni kama alivyosema Kimani (2003). Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa mgao wa kazi za kila jinsia ulibainishwa tangu utotoni.

Salim (1978) anasema kuwa katika familia asili ya Waswahili wanawake walitumia wakati wao pale nyumbani wakifanya kazi za nyumbani. Mgao wao wa kazi ulikuwa ni kunadhifisha boma, kupika, kusiaga nafaka, kusuka nywele na kufuma mikeka. Mwanaume ndiye aliyekuwa kichwa cha familia huku akiwa na jukumu la kukimu mahitaji ya kimsimgi ya mke na watoto wake na kufanya uamuzi katika familia yake. Huu ni mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanamke na mwanaume.

Brittan (1997) anasema kuwa majukumu ya kiuana hayapatikani nje ya historia na utamaduni wa jamii husika. Kwa hivyo, uanaume na uanauke unaweza kufasiliwa upya. Hivi ni kusema kuwa mgao wa kazi wa kila mwanajamii unaweza kufasiliwa upya kadiri jamii inavyobadilika kiuchumi na kisiasa. Mashirika kama vile shirika la umoja wa kimataifa yamechangia utetezi wa usawa wa kijinsia kupitia kwa mikutano kama vile, *WCIWY 1975*, *WCUND: Equality (1980), TTWCW* (1985) na *FWWC (1995).* Mikutano hii ilikubaliana usawa wa kijinsia utekelezwe katika nyanja zote za maisha. Kutokana na makubaliono haya mgao

wa kazi za mwanaume umebadilika kwa sababu mwanaume anafanya kazi zilizokuwa za mwanamke. Usawa ndio unaotawala katika utekelezaji wa majukumu ya kila mwanajamii. Kutokana na mabadiliko ya kisiasa na kiuchumi mwanaume sasa anafanya kazi ambazo ni kinyume cha mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Imejitokeza katika hadithi tulizoteua kuwa kazi zifuatazo anazofanya mwanaume ni kinyume cha mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume.

### 2.2.1 Kazi ya Kushauri

Kushauri ni dhana inayotokana na neno "shauri". Kulingana na *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* toleo la tatu, neno shauri linamaanisha kutoa maoni, rai au nasaha. Shauri ni jambo aghalabu linalohitaji kuzungumzwa au kujadiliwa. Kushauri katika utafiti huu ni kutoa mwelekeo kuhusu jinsi ya kufanya jambo fulani. Kimani (2003) anasema kuwa mwanamke hakuwa na uwezo wa kutoa maoni wala kueleza hisia zake kuhusu jambo lolote katika familia. Angefanya hivyo angechukuliwa kuwa mtovu wa nidhamu. Kauli hii inamaanisha kuwa mwelekeo kuhusu jinsi ya kufanya mambo mbalimbali katika familia ulitolewa na mwanaume huku mwanamke akibaki kuwa mtu wa kufuata yale ameelekezwa afanye.

Katika jamii nyingi za Kiafrika hasa ile ya Waswahili uamuzi na ushauri ulifanywa na mwanaume. Jamii hizi zilifuata mfumo wa kuumeni. Masinjila (1997) anasema kuwa mfumo wa kuumeni ni mfumo wa kijamii, kisiasa na

kiuchumi ambao huhakikisha, huhifadhi na kuendeleza mamlaka ya mwanaume katika nyanja zote za maisha. Katika kuhifadhi na kudumisha mamlaka ya mwanaume mfumo wa kuumeni humpa mwanaume jukumu la kutoa uamuzi kuhusu masuala nyeti katika familia yake. Hii ni kwa sababu yeye ndiye kiongozi au kichwa cha familia yake.

Scanzoni (1979) anasema kuwa mwanaume hubadili majukumu yake kwa sababu atafaidika kutokana na mabadiliko hayo. Hii ina maana kuwa mwanaume anaweza kukubali mgao mpya wa kazi kwa sababu mgao huo unamletea faida fulani katika maisha yake na familia yake. Mwanaume anapoamua kufanya kazi ambazo tumetambua kuwa za kike anaweza kuwa ametathmini na kuona kuwa kuna faida katika kufanya kazi hizo. Kazi ya kushauri kama jukumu la kitamaduni la mwanaume ni kazi nzito ambayo huhitaji busara ili kutoa ushauri mwema.

Kazi hii ya kushauri yaonekana kuwa awali iliegemea mfumo wa ubabedume. Kwa mujibu wa Wamitila (2003) ubabedume ni mfumo wa kijamii ambao unamtukukuza mwanaume huku ukimdhalilisha au kumdunisha mwanamke. Mfumo huu ulizichukulia amali za kiume na mawazo yao kama kaida za kufuatwa katika jamii nzima. Kutokana na maelezo haya, mawazo ya mwanaume ndiyo yaliyofuatwa na mwanamke katika familia yao. Mwanamke pia hudhalilishwa na mwanaume anapojaribu kudumisha mamlaka yake. Katika mfumo wa ubabedume, ushauri ulitolewa na mwanaume.

Kwa mujibu wa Parson (2004) kazi ya kushauri sasa inafanywa na wanaume na wanawake kwa ajili ya ufanisi wa familia. Mwanaume na mwanamke wanashauriana kuhusu mwelekeo watakaochukua ili kuifanikisha familia yao. Aidha, mwanaume anaomba ushauri wa mkewe katika masuala nyeti na mazito ambayo peke yake hawezi. Mwanaume kama huyu hufanya hivyo baada ya kutathmini na kupata kuwa mgao mpya wa kazi unamletea faida na ufanisi katika maisha yake.

Tulitambua katika hadithi ya "Uganga wa Pete", inayopatikana kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* kuwa kazi ya kuwa mshauri katika familia imetwaliwa na mwanamke huku mwanaume akitegemea ushauri wa mkewe. Maskini ambaye ni mhusika wa kiume katika hadithi hii mwanzoni alijitokeza kama mwanaume ambaye ameshikilia ubabedume.

Mwanzoni mwa hadithi ya "Uganga wa Pete" Maskini alikuwa akimchapa mkewe kama inavyodhihirika katika hadithi. "Mimi siendi nawe, nimechoka kupigwa kama ngoma usiku!" (uk 102). Maneno haya ya mke wa Maskini yanathibitisha kuwa mwanaume huyu awali alikuwa akimpiga mkewe. Kitendo cha kumchapa mke kinaweza kuchochewa na mfumo huo wa ubabedume unaomfanya mwanaume kujihisi kuwa bora zaidi na mwenye mamlaka yote katika familia. Maskini anaonekana kubadilika na kutua ubabedume hadithi inapoendelea. Tunaweza kusema kuwa mabadiliko haya yalichochewa na mabadiliko ya kiuchumi ambapo mwanamke pia anashiriki katika utafutaji riziki na kusaidia

katika kukimu familia.  Katika hadithi hii pia tunajulishwa kuwa Maskini alitegemea kipato duni cha mkewe kwa sababu yeye mwenyewe hakuwa na kazi ya ujira.

Maskini anaomba ushauri kwa mkewe kuhusu jinsi ya kutatua matatizo yaliyomkumba na ambayo yeye mwenyewe ameshindwa kutatua.  Pia, anaonekana kunyenyekea kwa mkewe ili aweze kumshauri vilivyo.  Hili la mwanaume kuomba mkewe ushauri kwa unyenyekevu halikuwa katika mgao wa kimapokeo wa kazi za mwanaume bali linajikita katika mgao mpya wa kazi za mwanaume. Mkewe Maskini alimshauri kila mara na hivyo kumuokoa kutoka hatarini. Maskini anapoitwa na mfalme ili amshauri ilipokuwa pete ya Malkia, aliogopa sana na kuamua kwenda kumuomba mkewe ushauri.  Inasadifu kuwa wakati pete ilipokuwa ikimezwa na jogoo, mkewe Maskini alikuwa nyumbani kwa mfalme na pia alishuhudia kisa hicho.  Kauli ifuatayo inadhihirisha kuwa jukumu la kushauri limetwaliwa na mwanamke:

> Kwa hivyo akamshauri mumewe asitie shaka. Akamweleza namna alivyomwona jogoo mwekundu na mkubwa kuliko wote pale nyumbani pa mfalme akiimeza pete husika.  Kwa kumweleza mumewe hivi, tatizo lake likawa limetatuliwa.(uk 102).

Maneno ambayo tumenukuu hapo juu yanaonyesha kuwa ushauri wa mke wa Maskini ulimfaa mumewe katika kukitegua kitendawili cha pete ya Malkia.  Baada ya Maskini kusaidiwa na mkewe kutatua suala hilo nyeti ambalo lilimkabili, alipata sifa nzuri kwa mfalme kama mganga hodari.

Pia katika hadithi hii, majambazi waliweza kupora mali ya mfalme.  Baada ya uporaji huu mfalme alimwita Maskini ili aseme vilipofichwa vitu vilivyoibwa kwani mfalme aliamini kuwa Maskini alikuwa mganga hodari.  Kazi hii ilikuwa gumu kwake Maskini ndiposa akaamua kwenda kuomba ushauri kwa mkewe. Kwake, mkewe alikuwa mtatuzi wa masuala sugu na ambayo yalimlemea yeye. Jambo hili linathibitika kupitia kwa usemi ufuatao;

> Mfalme akaamua kumwita tena Maskini ili aje aseme vile vilivyoibwa vimefichwa wapi.  Jukumu hili lilikuwa gumu na zito na lilimfadhaisha sana Maskini.  Hakujua kama ajitoe vipi.  Kwa mara nyingine, akaomba arudi nyumbani kwake mpaka keshoye kwa kujidai kuwa mambo yake yeye hufanya usiku…  Kule kufika nyumbani aliomba ushauri kutoka kwa mkewe (uk 104.)

Dondoo la hapo juu linadhihirisha kuwa mwanaume sasa anashauriwa na mwanamke kwenye masuala mazito mazito kama alivyoshauriwa Maskini na mkewe.  Pia linadhihirisha kuwa hakuna mhusika katika familia ambaye anapewa kipaumbele kutoa suluhisho na maamuzi kwenye masuala nyeti.  Kazi hii ya kutoa ushauri na kufanya maamuzi katika familia ilikuwa ya mwanaume kabla ya majilio ya ukoloni na elimu rasmi hasa katika familia za Waswahili kama tulivyosema hapo awali.  Mwanaume sasa anamheshimu mkewe na kushirikiana naye katika shughuli zote likiwemo suala la kufanya uamuzi.

Kupitia usimulizi wa babu katika hadithi hiyo ya “Uganga wa Pete”, mwandishi anamsihi mwanaume kumheshimu mkewe na kushirikiana naye maana ni ubavu wake tangu ngano za kale. Katika Bibilia Takatifu kitabu cha mwanzo sura ya pili na mstari wa 21-23 Mungu alimfanya Adamu kulala usingizi mnono na kutoa

ubavu mmoja kisha Mungu akamtengeneza mwanamke kutoka kwenye ubavu huo hatimaye, alimpeleka mwanamke huyo kwa Adamu. Adamu naye akasema, "Huu ni mfupa wa mifupa yangu na nyama ya nyama zangu, ataitwa mwanamke kwa sababu alitolewa kwa mwanaume." Maelezo haya yanaupa usimulizi wa Babu mashiko kwamba mwanaume na mwanamke wanakamilishana na kwa hivyo wanapaswa kufanya mambo yao pamoja huku mwanaume akimchukulia mwanamke kama sehemu yake. Kwa mujibu wa usimulizi huo wa babu, kazi hii ya kushauri sasa inafanywa na mwanamke huku akitoa ushauri wenye busara na wa kumfaidi mwanaume.

Parson (2004) akifafanua mipaka ya majukumu ya kiuana kama tulivyoonyesha katika sura ya kwanza, alisema kuwa kwenye muundo wa familia ya awali, kazi ya kushauri ilifanywa na mwanaume. Yeye ndiye aliyekuwa akitoa uamuzi wa mwisho huku mwanamke akifuata uamuzi na ushauri wa mumewe. Lakini katika mfumo wa kisasa ambao Parson alionyesha, kazi ya kushauri ilifanywa na mwanaume na mwanamke kwa pamoja. Akifafanua kauli hii, Parson alisema kuwa hakuna mhusika katika familia anapewa kipaumbele kutoa suluhisho na maamuzi katika familia. Kwa hivyo, kila mmoja awe mwanaume au mwanamke anaweza kuelekeza mwenzake jinsi ya kutatua suala fulani katika familia yao.

Elishopher (2013) anasema kuwa mashirika kama vile Umoja wa Kimataifa yamekuwa yakitetea usawa katika jamii. Matokeo yake yamekuwa wanawake wengi kujiunga na kazi za malipo. *Beijing Declaration and Platform for Action*

*1995 Chap. IV Article 82* ilinuia kupunguza tofauti baina ya wanawake na wanaume. Walisisitiza wanawake wahusishwe katika kufanya maamuzi muhimu katika jamii na wapewe nafasi za kazi sawa na wanaume.

Kwa mujibu wa Foucault (1978) usomi wa kijinsia ulienea kuanzia karne ya kumi na saba hadi katikati mwa karne ya ishirini. Kipindi hiki kimeshuhudia mikataba mingi kuhusu suala la usawa wa kijinsia na utetezi wa haki za wanawake. Mikataba hii ni mazao ya mikutano kama vile *WClWY* 1975, *WCUND: Equality (*1980), *TTWCW* (1985) na *FWWC (1995).* Maafikiano ya mikutano hii ni kuwa na usawa wa kijinsia katika nyanja zote za maisha. Hii ina maana kuwa, usawa unapaswa kuzingatiwa katika shughuli zote za kila mwanajamii ukiwemo mgao wa kazi mpya za mwaname.

Kama inavyjitokeza hapa, tunaweza kusema kuwa wanaume ambao wamesoma na kuzinduka katika masuala ya usawa wa kijinsia, wanachukua mgao mpya wa kazi kwa njia chanya. Wanawasikiza wake zao na kuchukua ushauri wenye busara na manufaa kutoka kwao. Kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* katika hadithi ya “Dr. Strese”, mwanamke ndiye anayetoa ushauri katika masuala nyeti huku mwanaume akiufuata na kufaidika nao. Mwandishi anadhihirisha haya kupitia kwenye dondoo lifuatalo; “Daktari Strese aliweza kumsikiza mkewe na kurekebisha maisha yake. Alipunguza ulevi na kurudia juhudi kazini kwake” (uk.50). Inabainika katika dondoo hili kuwa mkewe Daktari

Strese alimpa ushauri nasaha na kumwezesha kupunguza ulevi ambao awali ulikuwa umemlemea na kuathiri afya yake.

Daktari Strese kuchukua ushauri wa mkewe ni jambo ambalo linadhihirisha mabadaliko hasa ikizingatiwa kuwa amesoma na ukweli kuwa jamii nyingi za Waafrika hawakusikiza wake zao wala kuchukua ushauri kutoka kwao. Katika hadithi hii, mwandishi ameweka wazi usomi wa Daktari Strese anaposema, "Strese alikuwa amemaliza shule ya upili na hata kuingia chuo kikuu alikosemea kazi ya udaktari." (Uk.43-44)

Mwandishi wa hadithi hii ya "Dr. Strese" pia amesawiri wahusika ambao wameshika jadi za mgao wa kazi za mwanaume. Hamnazo ambaye ni mhusika wa kike na dada ya Daktari Strese alishika na kufuata imani za jadi za mgao wa kazi za mwanaume. Kwake kazi ya mwanaume ni kukimu mahitaji ya mke kama alivyomuona babake akifanya. Mwanamke huyu alikuwa amesoma na kufuzu katika daraja la P1. Kwa mujibu wa hadithi hii, cheo hicho kiliheshimika katika miaka ya sabini. Hamnazo alikuwa amepata ujira lakini kutokana na imani yake ya kijadi, alitarajia kuwa mumewe angekimu mahitaji ya familia yake huku hela zake akizitumia kwa faida yake mwenyewe. Kwa upande mwingine mumewe Hamnazo ambaye pia ni msomi na mwalimu mkuu wa shule ya upili, hakutarajia kwamba mshahara wake ndio ambao ungetimiza mahitaji yao wote wawili. Kwa mujibu wa maelezo haya, mgao mpya wa kazi za mwanaume unakinzana na mgao

wa kazi wa kitamaduni kwa sababu mgao mpya wa kazi unaonyesha kuwa mwanamke pia anapaswa kukimu mahitaji ya familia kama afanyavyo mwanaume.

Mumewe Hamnazo amezinduliwa na elimu na kukaribisha mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume. kwake kazi ya kukimu familia inafanywa kwa ushirikiano na mwanamke hasa pale mwanamke pia anafanya kazi ya ujira au biashara. Ukweli wa kauli hii unadhihirika kutokana na usimulizi wa mwandishi: "Kwa sababu Hamnazo alikuwa mwalimu wa shule ya msingi, mumewe naye, hakutarajia kwamba hela yake pekee ndiyo ambayo ingewatekelezea mahitaji yao wote wawili" ( uk 42)

Kadhalika, mwandishi wa hadithi ya "Dr. Strese" ameonyesha mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume kwa sababu ameangazia pande mbili za Daktari Strese. Awali katika hadithi hii Daktari Strese alishikilia jadi za mgao wa kazi za mwanaume. Aliamini kuwa mtoto wa kwanza wa kiume ndiye anayechukua jukumu la kuwa kiongozi wa familia. Jukumu hili liliandamana na kazi ya kukimu familia na kutoa mwelekeo katika familia. Ryanga, mwandishi wa hadithi hii anaiita kazi hii "kufaa kofia ya baba." Baba alifanya kazi ya kukimu familia yake pamoja na makinda wao. Kwa hivyo, Daktari Strese aliamini kuwa kazi ambazo baba yake alizifanya alipaswa kuzifanya yeye kama mwana wa kwanza wa kiume:

> Strese alipoanza kazi tu, ilimbidi achukue majukumu ya babake pale nyumbani. Aliazimia kutotafuta nyumba yake binafsi katika eneo lilokuwa karibu na sipitali, bali abaki pale kwao ili asaidie. Babake alifurahia hili na kutiwa moyo na busara ya mwanawe (uk 44.)

Kutokana na maelezo ambayo mtafiti ametoa, mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume umebadilika na kuchukua mkondo mpya. Daktari Strese na mumewe Hamnazo wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume. Daktari Strese aliweza kuweka kando imani yake kuhusu mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume na kuchukua ushauri wa mkewe ambao ulimfaidi. Mume wa Hamnazo naye alishikilia kuwa kazi ya kukimu familia sasa inapaswa kufanywa na mwanamke na mwanaume kwa ushirikiano ili kuleta ufanisi na maendeleo katika familia.

Katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*, hadithi ya "Macheo Mengine", baadhi ya wanaume ambao hawajasoma na kupata elimu ya Kizungu wangali wanashikilia tamaduni zao hasa kuhusu mwanaume kuwa mwenye nyumba. Mwanaume huyu hufanya uamuzi na kutoa ushauri kuhusu masuala nyeti yanayoikumba familia yake. Mzee Majaliwa, mhusika wa kiume katika hadithi hii angali anashikilia mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Katika mgao huu mwanaume ndiye kichwa cha familia. Kwa mujibu wa hadithi hii kuwa kichwa cha familia kuliambatana na kuwa"mwenye nyumba." Maana ya kauli hii ni kuwa mwanaume ndiye aliyekuwa msemaji katika familia. Pia ndiye aliyetoa mwelekeo utakaofuatwa na familia yake hasa katika kutatua masuala nyeti. Aidha kauli hii inaashiria ubabedume ambao humtukuza mwanaume na kumpa mamlaka juu ya mwanamke.

Kama tulivyosema katika sura ya kwanza, mfumo wa ubabedume huzichukulia amali za kiume na mawazo yao kama kaida za kufuatia katika jamii nzima. Kwa kuwa wanaume katika mfumo huu wametukuzwa, kila mwanajamii hujionea fahari mwana wa kiume kama anavyoonyesha mwandish wa hadithi ya “Macheo Mengine” kupitia kwa mhusika wa kiume kwa jina Sikujua: “Fahari ya mwanaume ni mtu kupata angalau mtoto mmoja wa kiume” (Uk. 29).

Pia, mwanaume hakupaswa kuwa na hisia za huruma, masikitiko, imani, woga na hofu. Mwanaume angekuwa na hisia hizi, angechukuliwa kuwa mnyonge. Hizi ni kaida ambazo zilifuatwa na kila mwanajamii ili kuafiki uanaume katika jamii yake. Ni kwa msingi huu ambapo mzee Majaliwa alimrejelea Sikujua kama “mwenye nyumba.” Sikujua alipaswa kufanya uamuzi wa njia na mahali pa kumwangamizia mwanawe ambaye alizaliwa na ulemavu. Tukizingatia kuwa, kuwa kichwa cha famila pia kunafungamana na kuilinda familia dhidi ya hatari zote, tunatarajia Sikujua kumlinda mwanawe asiangamizwe. Jambo hili linaoneka kuwa gumu kwa Sikujua kama inavyojitokeza kwenye nukuu lifuatalo:

> Naelewa kwamba lazima auawe kabla ya siku ya kumi tangu kuzaliwa kwake. Kuhusu mahali, wakati na mbinu ya kumuulia mwanangu sijafanya uamuzi wa mwisho. Kama ujuavyo, sio rahisi kamwe kwangu kufanya uamuzi huu japo natambua sina njia ya kuikwepa mila hii yetu ya jadi (uk 31).

Nukuu la hapo juu linadhihirisha kuwa Sikujua ambaye ni mwanaume amelemewa na jukumu hili la kutoa mwelekeo. Alipaswa kutoa mwelekeo watakaofuata yeye

na mkewe kutatua suala nyeti kuhusu usalama wa mwana wao ambaye alizaliwa na ulemavu.

Hata hivyo, baadhi ya wanaume wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume. Kwa Mfano, jukumu la kuamua katika boma linatekelezwa na mwanamke ambaye ametwaa kazi ya kukata kauli katika masuala nyeti yanayoikumba familia yao. Mwakwetu, mhusika wa kike na mkewe Sikujua anamshauri mumewe watafute msaada wa sheria dhidi ya mwana wao aliyepangiwa kifo kwa ajili ya kuzaliwa na ulemavu. Sikujua anashindwa kufanya uamuzi wa busara na badala yake mkewe anafanya uamuzi huo wa kumuokoa mtoto wao wa kiume kutokana na uhasama wa wanakijiji. Sikujua kama kichwa cha familia na mwenye nyumba, alipaswa kutoa suluhu la kumuokoa mwana wao wa kiume kutokana na mpango wa wazee wa kutekeleza mila na desturi zao. Mila za jamii yao kama asemavyo Majaliwa ni kuwa mwana anapozaliwa na ulemavu angeangamizwa kwa sababu alileta nuksi kwenye familia na kufunga tumbo la uzazi la mwanamke.

Katika hadithi hii, badala ya mwanaume kushika usukani kamili wa kuiendesha na kuilinda familia yake, mkewe ndiye anayeshughulika huku mwanaume akishiriki kutii yale mkewe anamwambia. Tunayoyazungumzia hapa yanadhihirika kwenye usemi wa Mwakwetu: "Lazima tutafute msaada wa sheria. Kila kiumbe licha ya maumbile yake, ni muhimu na ana haki sawa na wenzake katika jamii" (uk 36). Usemi huu unatubainishia kuwa suala ambalo lilikuwa nyeti katika familia hii

linatatuliwa kutokana na ushauri wa Mwakwetu kwa mumewe kuwa wanaweza kupata msaada wa sheria kumlinda mwana wao.

Mwandishi anasema kuwa haya ni macheo mapya. Kwa mujibu wa TUKI (2013) macheo ni wakati jua linapochomoza au mapambazuko. Katika muktadha wa hadithi hii dhana "macheo" inaashiria kipindi kipya. Hiki ni kipindi ambacho wanajamii wamepata mafunzo ya katiba mpya na kufahamu kuwa wanaweza kutafuta ulinzi wa sheria dhidi ya mila na desturi za kinyama kama vile mauaji ya watoto walemavu. Mwandishi akinukuu katiba kifungu 26(1-4) anasema,

> Vifungu nambari 3 na 2 vinasisitiza kwamba mtu yeyote hawezi kunyimwa haki ya kuishi ambayo huanzia pale mtoto anapokuwa tumboni mwa mamaye. Ni uwezo wa sheria tu unaoweza kumnyima mtu mhalifu haki ya kuishi. Isitoshe, kifungu namba 1 kinatilia mkazo kuwa kila mtu ana haki ya kuishi (uk 34-35).

Baxter na Montgomery (1998) wanasema kuwa majukumu ya kiuana ni kitu kinachobadilika na husababisha mume na mke kufanya kazi pamoja. Kama inavyojitokeza kwenye maneno yaliyonukuliwa hapo juu, mafunzo ya katiba mpya yamemzindua Mwakwetu ambaye alimshawishi mumewe kuchukua ushauri wake kuokoa mwana wao asiuliwe na Wajadi. Mwanaume sasa anaunga mkono uamuzi wa mkewe na kuamua kushirikiana naye kutatua suala la kuangamizwa kwa mtoto wao mlemavu. Haya ni mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume kwa sababu katika mgao wa kitamaduni mwanaume ndiye aliyekuwa na uwezo wa kuelekeza huku mwanamke akifuata bila pingamizi. Ili kuipa kauli hii mashiko,

Sikujua anamwambia mkewe; “Ni macheo mengine mapya” kisha wanashikana mikono kuendelea na safari (uk.36). Maana ya usemi huu wa Sikujua ni kwamba hiki ni kipindi kingine kipya ambapo amefahamu haki za walemavu na uwezo wa katiba mpya wa kulinda kila mwanajamii. Pia ametambua umuhimu wa ushirikiano katika kutatua maswali nyeti yanayoikumba familia.

### 2.2.2 Kazi ya Ulinzi

Ulinzi ni neno linalotokana na kitenzi linda. Kwa mujibu wa Ahmed na wengine (2013), linda ni kuangalia ili kuepusha na madhara ama hasara; weka salama; chunga. Katika utafiti huu, ulinzi ni mikakati ambayo inawekwa ili kuhakikisha usalama wa familia. Buttler (1990) anasema kuwa mwanaume alihitajika kulinda familia na kuichumia huku wanawake wakihitajika kushiriki majukumu ya nyumbani kama vile kupika, kutunza watoto na mume. Kulingana na usemi wa Buttler, ulinzi ni kazi asili ya mwanaume. Mwanamke na watoto walitarajia kuwa mwanaume angewalinda dhidi ya hatari zozote.

Katika hadithi ya “Macheo Mengine”, kazi ya kulinda familia inafanywa na mwanamke. Mwakwetu, mkewe Sikujua alizaa mtoto mlemavu ambaye kulingana na desturi za familia yao alipaswa kuuliwa. Baraza la wazee lilipoamua kumuua mtoto huyo, Sikujua alikuwa na changamoto kubwa kumlinda mwanawe. Alipolemewa kumlinda, Mwakwetu aliamua kumlinda kwa kutumia sheria za nchi katika katiba mpya. Katiba mpya tunayorejelea hapa ni ile ambayo imeangaziwa

na mwandishi wa hadithi ya "Macheo Mengine". Katika mafunzo ya katiba tunafahamishwa kuwa kuna sheria za kuwalinda watu wote.

Wakufunzi wa katiba hii mpya wanasema, "Kifungu cha namba 1 kinatilia mkazo kuwa kila mtu ana haki ya kuishi" (uk.35). Hii ina maana kuwa walemavu wamepewa ulinzi wa kikatiba na kwa hivyo hakuna mtu anayepaswa kukatiza maisha yao. Mafunzo hayo ya katiba mpya ndiyo yaliyomzindua Mwakwetu na kumpa ujasiri wa kumlinda mwanawe asiangamizwe na Wajadi. Ingawa kazi hii ilikabiliwa na changamoto nyingi, Mwakwetu alidhihirisha kuwa si lazima mtu kutumia nguvu za misuli ili kuitekeleza. Kupitia sheria za nchi yao, Mwakwetu alifaulu kumlinda mwanawe kutokana na uhasama wa baraza la wazee.

Scanzoni (1979) anasema kuwa kazi za mwanaume hubadilika kulingana na mabadiliko ya kazi za mwanamke. Kazi ya mwanamke imebadilika kwa sababu sasa anatoa ulinzi wa familia yake kwa kutumia sheria kwenye katiba mpya. Uzindushi wa katiba alioupata Mwakwetu ulimwezesha kumshawishi mumewe kushirikiana naye katika kumlinda mwanawe. Kutokana na ufafanuzi wa kazi hii ya ulinzi, tunaweza kusema kuwa kazi hii imebadilika kwa sababu changamoto za kazi hii zinatatuliwa na mwanamke huku akimshawishi mumewe kuunga mikakati yake ya kutekeleza kazi hii.

### 2.2.3 Kazi ya Upishi

Salim (1978:11) anasema kuwa katika familia ya Waswahili, wanawake walitumia muda wao mwingi katika mazingira ya nyumbani huku wakifanya kazi za

nyumbani. Kazi hizi zilijumuisha kufagia, kupika, kuosha vyombo, nguo, kusaga unga, kusuka nywele na kufuma mikeka. Salim alionyesha jukumu la kupika kama jukumu asili la mwanamke katika familia za Waswahili. Mawazo haya ya Salim yamejikita katika nadharia ya uana kwa sababu yanazungumzia masuala ya kijinsia ambayo yamo katika nadharia hii ya uana. Mgao wa kazi za mwanaume pia umo katika nadharia hii. Tukizingatia usemi wa Salim tunaweza kusema kuwa kazi ya kupika ni kazi ya kitamaduni ya mwanamke na inapofanywa na mwanaume inaashiria mabadiliko. Mawazo haya yalisaidia mtafiti kudhihirisha kuwa kazi ya kupika imebadilika kwani baadhi ya wanaume wanashiriki kazi hii kinyume na ilivyokuwa awali.

Nadharia ya upembuzi inashikilia kuwa kila kitu kinapita na kina kikomo kinachopatikana kipindi fulani cha wakati. Marx (1873) anasema kuwa tabaka la jamii hutoweka na lingine kuchipuka kwa sababu ya mapambano yanayotokea kati ya tabaka tawala na tabaka tawaliwa. Katika jamii zilizotawaliwa na mfumo wa kuumeni, mwanaume alipewa nguvu zaidi kuliko mwanamke. Mgao wa kazi uliegemea mfumo tawala huku ukimpa mwanaume kazi zinazoashiria utawala dhidi ya mwanamke.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa Marx alimpa binadamu tumaini la kung’oa mizizi yote ya unyonyaji na unyanyasaji na kujenga ulimwengu wa kinjozi usiokuwa na madhila. Jamii ya sasa inatilia mkazo usawa wa kijinsia na utendakazi sawa wa wanajamii wote. Kazi za wahakiki wa kifeministi kama vile

Woolf, Simone De Beavoir na Wollstonecraft zilichangia katika kuanzisha harakati za ukombozi wa mwanamke. Walipigania usawa ambapo mwanamke anachukua nafasi sawa na mwanaume katika jamii. Mapambano haya ndiyo yalizaa mgao mpya wa kazi za mwanaume kama vile kazi ya kupika.

Kazi ya kupika ambayo awali ilikuwa kazi asili ya mwanamke sasa inaonekana kubadilika kutokana na ushawishi wa elimu rasmi. Kurian (2007) anasema kuwa ongezeko la usajili wa watu katika mfumo wa elimu rasmi umefanya mfumo wa ushawishi wa kijamii wa wanawake na wanaume kuwa dhaifu. Uwafiki wa kazi za kitamaduni za kiuana sasa umepungua kutokana na ongezeko la usomi wa elimu rasmi. Mgao wa kazi za mwanaume na mwanamke umebadilika kwa sababu mwanaume anafanya kazi ambazo kitamaduni zilikuwa za mwanamke kama vile kupika. Wahusika wa kiume katika baadhi ya hadithi wameichangamkia kazi hii. Wamegundua kuwa kitu muhimu cha kufuata si utamaduni wa kibabedume bali ni nguvu hela za kuendeleza maisha. Wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume wameshawishiwia na elimu kwamba mwanaume pia anaweza kufanya kazi ambazo katika mfumo wa kibabedume zimekuwa zikifanywa na wanawake.

Nguvu hela katika utafiti huu ni uwezo anaopata mtu kutokana na upataji wa hela za kuendeleza maisha yake. Uchumi unaweza kutengeneza kazi ambazo watu mbalimbali wanafanya. Kwa mfano, Mapanya katika hadithi ya "Mke Wangu" anashiriki kazi ya upishi kama kazi yake rasmi inayompa mapato na hela za

matumizi yake ya kimsingi. Kwa hivyo, mwanaume huyu amechukulia kazi hii kama nguvu hela inayomwezesha kukimu mahitaji yake.

Isitoshe, katika hadithi ya “Maeko” Hamduni ambaye ni mhusika wa kiume alifanya kazi ya upishi katika hoteli. Wanaume kwa hivyo, wanafanya kazi ya kupika ili wapate riziki na hatimaye wanapata ujuzi na kuwa wapishi hodari. Hamduni aliifanya kazi hii kwa ustadi mkubwa hata pale nyumbani kwake alipokuwa akimpikia mkewe. Keith na Brubaker (1979) wakimnukuu Lipman (1969), wanasema kuwa wanaume walijihisi kuwa wa maana na wenye umuhimu wanaposhiriki kazi za nyumbani na pia husisitiza mapenzi katika uhusiano. Jamila alifurahia upishi wa Hamduni, mumewe ambao ulikuwa bora zaidi:

> Hamduni aliwasha buli la umeme akateleka chai nzito ya maziwa, akaoka jiko la makaa na kutayarisha supu ya pweza na penye jiko la utambi akaanga mayai… hii haikuwa kazi ngumu kwake, hasa ukitilia maanani uzoefu wake aliokuwa nao kama mpishi wa hoteli (uk.55).

Maneno ambayo tumenukuu hapo juu yanaonyesha kuwa Hamduni alikuwa mpishi bora kutokana na uzoefu wake wa kazi hii kwenye hoteli. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa wanaume sasa wanafanya kazi ya upishi kwa hiari yao. Pia wanafanya kazi hii kama njia mojawapo ya kupata riziki na pia kusadia pale nyumbani. Vilevile, ilibainika kuwa wanaume wanaweza kutekeleza kazi hii kwa ustadi mkubwa. Katika usimulizi wa hadithi ya “Maeko” tulifahamishwa kuwa upishi wa Hamduni ulimfurahisha mkewe sana na kumfanya kula zaidi.

Wahusika wengine kama vile Ukombozi katika hadithi ya "Mayai Waziri wa Maradhi", wanafanya kazi hii ya upishi. Ukombozi anapika chai pale nyumbani kwao. Ukombozi ni mtoto wa kiume, mwanawe Bwana Mayai Waziri wa Maradhi. Ukombozi anapofanya kazi ya upishi anakuwa kielelezo wanaume ambao wamekubali mgao mpya wa kazi za mwanaume. Hii ni kwa sababu kazi hii ni kazi ya kitamaduni ya mwanamke kama tulivyosema hapo nyuma. Kazi ya upishi inapofanywa na mwanaume, huonyesha mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume.

### 2.2.4 Kazi ya Kuosha Nguo

Engels (1972) anasema kuwa majukumu kati ya wanawake na wanaume yalitegemea umri na jinsia. Wanawake walichukua kazi za kinyumbani huku wanaume wakichukua kazi ya kuchumia familia. kazi za kinyumbani katika muktadha huu ni kupika, kuosha vyombo, kuosha nguo na kunadhifisha boma. Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa mgao wa kazi za kila jinsia ulibainishwa tangu utotoni. Kazi ya kuosha nguo ambayo tunafafanua hapa ni kazi ya kitamaduni ya mwanamke.

Mwandishi wa hadithi ya "Mke Wangu" amesawiri mhusika wa kike kwa jina Aziza. Aziza ameshika jadi za mgao wa kazi kwa sababu kwake kazi ya kuosha nguo inapaswa kufanywa na mwanamke. Kama inavyojitokeza katika hadithi hii Mapanya ndiye aliyeajiriwa kuwapikia, kuwaoshea nguo na vyombo pale nnyumbani. Aziza anaonekana kukerwa na jambo hilo kwa sababu angali

anashikilia mgao wa kimapokeo wa kazi.  Mwanamke huyu alitaka kufanya kazi hizo kwa sababu yeye kama mwanamke anafaa kuzifanya.  Aziza anasema, “Nguo zangu sitaki mtu anifulie, wala vyombo sitaki kuoshewa” (uk 5).  Hata hivyo mgao huu umebadilika kwa sababu kazi hizi zinafanywa na mwanaume katika mfano tunayotoa katika utafiti huu kutoka kwenye hadithi fupi teule.

Katika hadithi ya “Maeko” kwenye diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, Hamduni anadhihirisha kuwa kazi hii ya kuosha nguo pia inaweza kufanywa na mwanaume.  Kama inavyojitokeza katika hadithi hii, mwanaume anafanya kazi hii kwa hiari yake na kwa uangalifu zaidi. Haya yanabainika kupitia kwa maneno yafuatayo:

> Duni akazikunjakunja nguo chafu zote ndani ya nyumba, nyingi zikiwa ni zile za mkewe, na kuenda nazo uwani.  Akazitenganisha nguo za rangi pake na zile nyeupe pake kisha akaziroweka katika mabeseni tofauti.  uk. 55

Maneno ambayo tumenukuu hapo juu yanaonyesha kuwa mwanaume sasa anaweza kushiriki kazi ya kuosha nguo kwa ustadi mkubwa.  Duni anaonekana kuwa na ujuzi wa kuosha nguo kwa vile anavyozitenganisha kulingana na rangi ili kuweza kuziosha kwa uangalifu.

Pia katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* kwenye hadithi ya “Mke Wangu“, kuna mhusika wa kiume anayeosha nguo ili kupata riziki.  Mhusika huyu anayejulikana kama Mapanya ameajiriwa pale nyumbani kwa msimulizi kufanya kazi za nyumba kama vile kupika na kuosha nguo.  Mapanya ndiye anayeosha

nguo za Aziza na mumewe.  Kwa hivyo, inaonekana kuwa mwanaume pia anaweza kufanya kazi ambazo awali zilichukuliwa kuwa za wanawake hasa katika jamii ya Waswahili ili kufidia mahitaji yake ya kiuchumi.

**2.2.5 Kuosha Vyombo**

Kazi ya kuosha vyombo inahusishwa na wanawake kama jukumu lao la kimsingi pale nyumbani.  Parson (2004) anasema kuwa kazi za nyumbani hapo awali zilikuwa kazi za kimsingi za mwanamke.  Kazi hizi ni pamoja na hii ya kuosha vyombo.  Salim (1978) anasema kuwa wanawake walifanya kazi ya kunadhifisha boma, kupika, kuosha vyombo, kuosha nguo, kusaga nafaka na kufuma mikeka. Kulingana na wahakiki hawa, Kazi hii ya kuosha vyombo ni kazi asili ya mwanamke.  Inapofanywa na mwanaume inakuwa kinyume cha mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume na kwa njia hii kuonyesha mabadiliko katika mgao huu wa kazi.

Katika hadithi ya “Mayai Waziri wa Maradhi” kazi ya kuosha vyombo pia inafanywa na wanaume.  Kwenye hadithi hii ya “Mayai Waziri wa Maradhi”, wahusika wa kiume kama vile Ukombozi na wenzake wanashiriki kazi hii ya kuosha vyombo:  “Walisimama kwa pamoja wakaenda jikoni kuosha vyombo walivyovitumia” (uk 69).  Maneno haya yanaashiria kuwa wanaume sasa wanashiriki kazi za nyumbani ikiwemo ya kuosha vyombo kwa hiari yao huku wakivunja mifumo ya jamii ambayo ilitambua kazi hii kama ya kike.  Isitoshe,

wanaume na wanawake wanaweza kufanya kazi ambazo zilikuwa za jinsia tofauti kwa kushirikiana.

### 2.3.0 Mgao wa Kazi za Mwanaume kwa Kuzingatia Ushirikiano

Katika sehemu hii, mtafiti alibainisha kazi ambazo mwanaume anafanya kwa ushirikiano na mwanamke bila kuzingatia tofauti za kijinsia. Mgao wa kazi za mwanaume ulioshughulikiwa hapa ni ule ambao unaonyesha kuwa mwanaume na mwanamke wanafanya kazi kwa kuungana ili kufanikisha mambo mbalimbali katika maisha yao. Baxter na Montgomery (1998) walitambua misingi miwili ya upembuzi; ukinzano na utaratibu wa mambo. Katika muktadha huu, ukinzano ni ushindani wa vitu viwili kama vile mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume na mgao mpya wa kazi za mwanaume. Utaratibu wa mambo unashikilia kuwa upembuzi unaendelea na unakua. Kwa hivyo mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume yanaendelea kutokea kama ilivyobainika katika hadithi tulizoteua.

Baxter na Montgomery (1998) wanaendelea kusema kuwa majukumu ya kiuana ni kitu kinachosababisha mume na mke kufanya kazi pamoja. Hivyo, mwanaume na mwanamke wanaweza kushirikiana katika kufanya kazi mbalimbali. Kwa kuegemea mawazo haya ya Baxter na Montgomery (1998) tunaweza kusema kuwa mgao wa kazi za mwanaume unabadilika ili kuafiki mabadiliko ya kiwakati ambapo mwanaume na mwanamke wanafanya kazi pamoja bila kuzingatia tofauti za kijinsia.

Kama tulivyosema awali kwenye utafiti huu, katika miaka ya karibuni, kumekuwa na mikataba mbalimbali inayotetea usawa wa kijinsia kupitia kwa mashirika kama vile shirika la Umoja wa Kimataifa na Jumuia ya Madola. Mikataba hiyo pia ilitetea haki za wanawake na kuhimiza usawa wa kijinsia katika nyanja zote za maisha. Ushawishi wa mikataba hii ulizaa mabadiliko ya falsafa za watu kuhusu mgao wa kazi ukiwemo mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Spence na Hahn (1997) wanasema kuwa majukumu ya kiuana yanabadilika na imani za wanajamii sasa zimekuwa za kisasa huku wakichuja baadhi ya tamaduni zikiwemo za mgao wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi. Ina maana kuwa mwanaume na mwanamke wanashirikiana katika mgao wa kazi huku wakikamilishana katika kutekeleza baadhi ya kazi. Tulibainisha kazi ambazo mwanaume anafanya kwa msingi wa ushirikiano na mwanamke katika hadithi tulizoteua.

### 2.3.1 Kazi ya Kutoa Suluhisho

Kwa mujibu wa TUKI (2013) suluhisho ni jambo linaloleta mapatano au uhusiano mwema baina ya watu. Pia ni njia ya kutatulia matatizo. Kwa mujibu wa utafiti huu, suluhisho ni njia ya kutatulia matatizo au masuala nyeti katkia familia ili kuleta uhusiano mwema. Parson (2004) anasema kuwa katika mgao wa kazi za kitamaduni, suluhisho lilitolewa na mwanaume hasa utata ukitokea katika familia. Lakini, katika mgao mpya wa kazi, kazi hii inafanywa na mwanaume na mwanamke kwa kushirikiana. Kama anavyosema Parson, hakuna mhusika katika

familia anayepewa kipaumbele katika kutoa suluhisho na maamuzi katika jamii. Kwa sababu hii basi, mwanaume au mwanmke anaweza kutoa suluhisho la jambo fulani katika familia.

Katika jamii za Kiafrika, mwanaume huhitajika kuwa mstari wa mbele katika kutoa suluhisho la jambo ambalo linaoneka kuwa gumu. Masinjila (1997) anasema kuwa mfumo wa kuumeni ni mfumo wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ambao huhakikisha, huhifadhi na kuendeleza mamlaka ya mwanaume katika nyanja zote za maisha. Katika kuhifadhi na kudumisha mamlaka ya mwanaume mfumo wa kuumeni humpa mwanaume kazi ya kutoa uamuzi kuhusu masuala nyeti katika familia yake. *Beijing Declaration and Platform for Action 1995 Chap. IV* walisisitiza wanawake wahusishwe katika kufanya maamuzi muhimu katika familia. Kauli hii ilinuia kuleta usawa wa kijinsia hasa katika familia na shughuli za kiuchumi. Kwa hivyo, kazi ambazo wanaume wanafanya ikiwemo ile ya kutoa suluhu katika masuala tata kwenye familia inatarajiwa kuhusisha wanawake ili kuafiki usawa wa kijinsia.

Parson (2004) alilinganisha tofauti za majukumu ya kiuana na mwingiliano wa majukumu hayo. Utafiti wake ulibainisha kuwa maamuzi katika familia za hapo awali katika tamaduni za Marekani yalifanywa na mwanaume. Lakini sasa hakuna mhusika katika familia anayepewa kipaumbele kutoa suluhisho na maamuzi katika katika familia. Wanaume na wanawake wanashirikiana katika kutoa suluhisho kuhusu jambo lolote linaloleta utata katika familia na maisha kwa jumla. Katika

utafiti wetu tulibainisha jinsi wanaume katika hadithi zilizoteuliwa wamedhihirisha mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume kwa kushirikiana na mwanamke.

Katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* kwenye hadithi ya "Kikaza", Bwana Pima na Bi. Cherehani wanashirikiana katika kutoa suluhisho kuhusu kitendawili cha kikaza.  Kikaza ni nguo ya uongozi ambayo hushonewa viongozi kwa ushirikiano wa umma kama anavyosema mwandishi wa hadithi hii katika ukurasa wa 42: "Kikaza hushonewa kiongozi kwa ushirikiano wa umma." Maitaria (2012) anasema kuwa kikaza ni makubaliano au maafikiano yanayobainisha na kudhibiti nguvu za watawala.  Kupitia udurusu wa kina wa hadithi hii, ilibainika kuwa kikaza hiki ndicho kinachotumika katika kuingoza nchi.  Aidha kikaza kina masharti yanayopaswa kutimizwa na kila kiongozi.  Robert Oduori, mwandishi wa hadithi hii anatueleza:

> Iwapo kiongozi ni mwanamke, wanawake wangempima wanaume nao wangeshona.  Wakati huu, kiongozi alikuwa mwanamume na kwa hivyo wanaume ndio waliopima nao wanawake wakashona (Uk 42).

Kikaza cha Watekede ambao ndio jamii tawaliwa katika hadithi hii kilizingirwa na kitendawili ambacho kilipaswa kuteguliwa ili kuwapa suluhu kuhusu uongozi wao. Kutokana na maelezo haya tunaweza kusema kuwa mwanaume na mwanamke wanafanya kazi pamoja kwani wanashirikina kutoa suluhisho.  Wanaume wakipima wanawake wanashona kikaza.

Kulingana na maelezo katika hadihi hii ya "Kikaza" Bwana Pima akichukua vipimo vya kikaza Bi. Cherehani naye anakishona kulingana na kipimo alichopewa. Kila mmoja ni mshirika muhimu katika kushona kikaza. Ithibati ya haya inaonyeshwa na mwandishi hivi: "Bi. Cherehani na Bwana Pima walikuwepo kutoa suluhisho na kusaidia kutegua kitendawili" (uk 42). Maneno haya yana maana kuwa mwanaume anashirikiana na mwanamke ili waweze kufanya kazi muhimu ya kutoa suluhisho kuhusu masuala yenye utata katika jamii zao tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo mwanaume pekee alitafuta suluhisho la mambo yenye utata.

Aidha kuna Mzee Kadiri katika hadithi ya "Ndoa ya Samani", diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* anayeshirikiana na mkewe kutafuta suluhu kuhusu arusi ya binti yao. Anapoletewa posa anawaomba wenye ujumbe kumpa muda ili aweze kumuuliza mkewe uamuzi wake. Anayoamua Mama Zena, Mzee Kadiri anayaunga mkono. Haya yanadhihirika kupitia kwa kauli ifuatayo, "Baba yake Amali akaingia jikoni kushauriana na mkewe" (uk 86). Kupitia maneno haya mwandishi ameonyesha kuwa babake Amali, Mzee Kadiri alishirikiana na mkewe, Mama Zena ili kutoa suluhu kuhusu kupokea au kukataa posa la Abu kwa binti yao. Kwa hivyo, mwanaume katika muktadha huu anashirikiana na mwanamke katika kutoa suluhisho kuhusu mambo muhimu katika familia zao.

Hadithi ambazo tumehakiki hapo nyuma zimeandikwa na waandashi wa kiume. Omar Babu ameandika hadithi ya "Ndoa ya Samani" huku Robert Oduori

akiandika hadithi ya "Kikaza". Waandishi hawa wamesawiri wahusika wa kiume ambao wameukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume. Mandy (2011) anasema kuwa zaidi ya miaka hamsini iliyopita kumekuwa na mabadiliko yanayoegemea mitazamo ya usawa katika majukumu ya kiuana. Matokeo ya utafiti wa Mandy ni kuwa, watu wenye elimu ya juu hukubali mabadiliko katika mgao wa kazi unaoafiki usawa wa kijinsia. Waandishi wa hadithi hizi ni wasomi na kwa sababu hii elimu imewashawishi kusawiri wahusika ambao wanakaribisha mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume.

### 2.3.2 Kazi ya Kukimu Mahitaji ya Familia

Ndungo (1998) alitambua kazi ya kukimu familia kama kazi ya kimsingi ya mwanaume. Anasema kuwa wanaume Waswahili kama vichwa vya familia walihusishwa na kazi ya kukimu mahitaji ya wake zao na watoto wao. Walitarajiwa kuhakikisha kuwa mahitaji yote ya kimsingi ya familia zao yametimizwa. Anaendelea kusema kuwa wanawake hawakupaswa kutoka nje ya boma isipokuwa walipowatembelea marafiki au kununua kitu sokoni. Hii ina maana kuwa mwanamke alipaswa kukaa nyumbani huku akifanya kazi ambazo zimo pale nyumbani.

Mbaabu (1985) anasema kuwa wanawake Waswahili hawakutwikwa mzigo wa utafutaji chakula cha familia bali kazi yao muhimu ilikuwa ni upishi na kazi zingine za nyumbani. Maneno haya ya Mbaabu yanadokeza kuwa mwanaume ndiye aliyekuwa na jukumu la kufanya kazi ya kukimu mahitaji ya familia.

Mwanaume huyu angetafuta chakula naye mwanamke angekipika. Kwa hivyo, kazi yoyote ile iliyohitaji mtu kutoka nje ya boma na kutafuta riziki ilifanywa na mwanaume.

Moser (1999) anasema kuwa katika boma kuna mgao wazi wa kazi kwa misingi ya jinsia. Mwanaume kama mkimu familia alifanya kazi za nje naye mwanamke kama mke-nyumbani alifanya kazi zote za nyumbani. Kulingana na kauli hii ya Moser, mwanamke alitarajiwa kufanya kazi za kunadhifisha boma huku kazi za nje kama vile biashara na kazi zingine ambazo zinahusisha utafutaji wa riziki zikifanywa na mwanaume. Mwanamke anaposhiriki kazi kama hizi za nje atakuwa amechukua mgao mpya wa kazi. Baadhi ya hadithi ambazo ziliteuliwa katika utafiti huu zimesawiri wanaume ambao wanashabihiana na wanaume Waswahili ambao walifanya kazi ya kukimu mahitaji ya familia.

Biashara inahusisha mtu kutoka nje ya boma ili kutafuta bidhaa za kuuza na pia kuwapelekea wateja bidhaa hizo. Kazi hii katika muktadha wa kauli ya Ndungo na ya Mbaabu hapo nyuma inapaswa kufanywa na mwanaume kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa na ruhusa ya kutoka nje na uwezo wa kuitafutia famila yake riziki. Mwandishi anaonyesha mabadiliko katika kazi hii kupitia kwa mhusika wa kike, mkewe Atanasi katika hadithi ya “Fumbo la Mwana” katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Mwanamke huyu alikuwa akitoka nje ya boma kufanya biashara ya kuuza samaki. Mapato aliyopata ndiyo yaliyotumiwa kukimu mahitaji ya familia yao. Mzee Atanasi naye anashiriki kazi ya kulima

huko shambani ili kusaidiana na mke wake kuhakikisha kuwa mahitaji ya familia yao yametimizwa.

Katika kipindi cha sasa cha baada ya majilio ya elimu rasmi na utetezi wa usawa wa kijinsia, wanawake wanashiriki katika kazi za viwandani na kupata ujira ambao unawawezesha kushiriki katika kazi ya kukimu familia. Kwa sababu hii, wanaume na wanawake wanasaidiana katika kazi mbalimbali ikiwemo kazi ya kukimu mahitaji ya familia. Perry na wengine (1990) wanasema kuwa miaka kumi na mitano iliyopita kumekuwa na ongezeko kubwa la wanawake walioolewa viwandani wakifanya kazi ya ajira huku idadi ya wanawake wanaoshiriki kazi ya kukimu mahitaji ya familia ikiongezeka.

Katika hadithi ya "Fumbo La Mwana", iliyomo katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, Mzee Atanasi anashirikiana na mkewe kutekeleza kazi hii ya kukimu mahitaji ya familia yao. Kila mmoja wao amekubali mgao mpya wa kazi za mwwanaume. Mzee Atanasi anasema:

> Ninadamka kila siku majogoo ninakwenda kulima vitangaa vyangu … Nikitoka huko mimi huyo vichakani kuwalisha mifugo…Mama yao hushinda marikiti huko Lureko akichuuza samaki ( uk 92- 93).

Kama inavyojitokeza katika maneno ya Atanasi kwenye maneno yaliyonukuliwa hapo nyuma, mkewe Atanasi ni mshirika katika kazi ya kukimu familia yao. Kwa sababu hii tunaweza kusema kuwa kazi hii imechukua mkondo mpya kwa vile mwanaume anamshirikisha mkewe katika kuitekeleza.

Butler (1990) katika kazi yake ya kuumbuua jinsia anasema kuwa kila mwanajamii anatarajiwa kudhihirisha tabia fulani na kutekeleza majukumu mbalimbali ambayo yametegewa jinsia yake na jamii yake. Kwa hivyo, majukumu ya kiuana ni mkururo wa matarajio ambayo mwanaume au mwanamke anapaswa kudhihirisha katika jamii ili kuafiki jinsia yake. Pia, Bever (1999) anasema kuwa kazi ya mwanaume ni kutimiza mahitaji ya kimsingi ya familia yake. Uhakiki wa Ndungo (1998), Mbaabu (1985) na Bever (1999) unabainisha kazi ya kukimu mahitaji ya familia kama kazi ya kitamaduni ya mwanaume.

Kwa mujibu wa Brittan (1997) majukumu ya kiuana hayapatikani nje ya historia na tamaduni za jamii husika. Kwa hivyo, uanaume na unauke unahitaji kufasiliwa upya. Jinsi mabadiliko ya kihistoria, kitamaduni, kiuchumi na kisiasa yanavyotokea, ndivyo mgao wa kazi za mwanaume unavyopaswa kufasiliwa upya ili kuafiki mabadiliko haya. Katika mpwito wa wakati kazi ya kukimu mahitaji ya familia imebadilika kwani inafanywa na wanawake wakishirikiana na wanaume ili wasaidiane katika kukimu mahitaji ya familia zao.

Katika *Diwani ya Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* hadithi ya "Kachukua Hatua Nyingine" inaonyesha kwamba mzee Mavitu anaandamana na mkewe, Sakina kufanya kazi ya vibarua ili kukimu mahitaji ya familia yao. Mwandishi anatubainishia haya kwa kusema, "Njia ya pekee ilikuwa moja sasa: kushiriki katika kazi za vibarua. Mara hii ilimlazimu kuandamana na mkewe" (uk 47). Usemi wa mwandishi katika nukuu la ukurasa wa arubaini na saba

unamaanisha kuwa Mavitu anamshirikisha mkewe katika kazi ya kukimu familia. Wawili hawa wanafanya kazi za vibarua ili kusaidiana katika kufanikisha familia yao kazi ambayo awali ilikuwa ya mwanaume katika jamii nyingi za Afrika.

Isitoshe, hadithi ya "Uganga wa Pete" katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine,* mwandishi ameonyesha mhusika wa kike anayefahamika kama Mama Vitumbua ambaye anafanya biashara ya kuuza vitumbua sokoni. Kusudi la kufanya biashara hii ni kukimu mahitaji ya familia yake. Msimulizi wa hadithi hii anasema, "Alijua kuwa vyovyote viwavyo Mama Vitumbua atatoka kwenda kuchuuza vitumbua vyake" (uk 99). Kauli hii inamaanisha kuwa, mwanamke huyu anafanya biashara ambayo inakusudia kutekeleza kazi ya kukimu mahitaji ya familia. Hiii ni kazi ya kimapokeo ya mwanaume. Kwa hivyo mwanamke huyu ameukaribisha na kuukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume.

### 2.3.3 Kazi ya Kushauri

Kazi hii ya kushauri inajitokeza mara mbili katika utafiti huu: kwanza, kama mgao wa kazi za mwanaume ambao unaonyesha kinyume cha mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Pili, kazi hii inajitokeza katika mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa kuzingatia ushirikiano na mwanamke. Hii ni kusema kuwa mtafiti alihakiki hadithi zinazoonyesha wanaume ambao wanawashirikisha wake zao katika kazi hii ya kushauri kwa ufanisi wa familia zao.

Kama tulivyosema awali, kushauri ni dhana inayotokana na neno "shauri". Kulingana na Ahmed na Wengine (2013) neno shauri linamaanisha kutoa maoni,

mawaidha, nasaha au rai.  Shauri ni jambo aghalabu linalohitaji kuzungumzwa au kujadiliwa.  Kushauri katika utafiti huu ni kutoa mwelekeo kuhusu jinsi ya kufanya jambo fulani.  Kimani (2003) anasema kuwa mwanamke hakuwa na uwezo wa kutoa maoni wala kueleza hisia zake kuhusu jambo lolote katika familia.  Angefanya hivyo angechukuliwa kuwa mtovu wa nidhamu.  Kauli hii ina maana kuwa mwelekeo wa kufanya mambo mbalimbali katika familia ulitolewa na mwanaume huku mwanamke akibaki kuwa mtu wa kufuata yale ameelekezwa afanye.  Kama ilivyotajwa awali katika utafiti huu, katika jamii nyingi za Kiafrika, tamaduni nyingi zina misingi yake katika mfumo wa ubabedume na hutawaliwa kutokana na mielekeo ya wanaume huku wanawake wakibaki kuwa watekelezaji tu.  Kwa hivyo, kazi ya kushauri katika muktadha huu ni kazi asili ya mwanaume.

Kwa mujibu wa Fenistermaker (2002) majukumu ya jinsia fulani hujenga taswira kuwa tofauti za kijinsia hujidhihirisha kama kiungo muhimu cha tabia za kijinsia.  Kwa hivyo, majukiumu ya mwanaume yanatarajiwa kudhihirsha tabia za kiume kama vile ujasiri, kuwa kichwa cha familia na kutoa mwelekeo katika masuala nyeti.  Mwanaume Mswahili kama tulivyosema awali, ndiye kichwa cha familia ambaye anatarajiwa kutoa ushauri katika familia yake.  Ili kuipa familia mwelekeo katika masuala nyeti ya maisha mwanaume alitarajiwa kuwashuari watu wa familia yake.

Parson (2004) alilinganisha tofauti za majukumu ya kiuana na mwingiliano wa majukumu hayo.  Utafiti wake ulibainisha kuwa maamuzi katika familia za hapo

awali katika tamaduni za Marekani yalifanywa na mwanaume. Lakini katika familia za sasa, alisema kuwa hakuna mhusika katika familia anayepewa kipaumbele kutoa suluhisho na maamuzi katika katika familia. Kwa hivyo, wanaume na wanawake wanashirikiana katika kutoa suluhisho la jambo lolote linaloleta utata katika familia na maisha kwa jumla.

Mandy (2011) anasema kuwa zaidi ya miaka hamsini iliyopita kumekuwa na mabadiliko kuhusu usawa wa majukumu ya kiuana katika jamii za kisasa. Jamii za kisasa katika muktadha huu ni zile ambazo zimeathirika na elimu, madiliko ya kiuchumi, kisiasa na kihistoria zikiwemo jamii za Afrika. Wanaume na wanawake wamepata ushawishi wa elimu na wa kisiasa katika kubadili kazi zao. Mwandishi wa hadithi ya "Dr. Strese" ambaye ni mwafrika ameonyesha kuwa wahusika ambao wamesoma kama vile Daktari Strese na mume wa Hamnazo wameukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume. Tunaweza kusema kuwa mgao wa kazi za mwanaume umebadilika kwani badala ya mwanaume kuwa tegemeo la kutoa suluhisho, anashirikisha mwanamke katika kutoa suluhisho.

Hadithi ya "Kachukua Hatua Nyingine" iliyomo katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* inaonyesha kuwa mama na baba ya Sakina wanashirikiana kumpa ushauri binti yao. Hadithi hii inashughulikia kipindi cha miaka ya sitini. Katika kipindi hiki Afrika ilipiga hatua ya elimu rasmi huku kazi ya kushauri ikifanywa na mwanaume kwa ushirikiano na mwanamke. Kauli ifuatayo inadhihirisha haya: "Sakina aliacha kazi yake ghairi ya ushauri wa

mamake na babake. Wote walimshauri kwa kila nia…" (uk 41). Usemi huu unaashiria kuwa wazazi wa Sakina walifahamu umuhimu wa kufanya kazi na kumshauri ingawa alipuuza ushauri wao. Ushauri huu wanaufanya kwa ushirikiano ili kumsadia binti yao kuendelea kufanya kazi ambayo ni jambo muhimu hasa kwa mwanamke ambaye amesoma.

### 2.3.4 Kazi ya Kulima

Neno kulima ni kitenzi-jina kinachotokana na kitenzi lima. Longhorn (2013) wanasema kuwa lima ni kutayarisha shamba kwa kufyeka na kutifua ardhi kwa jembe. Kulima katika utafiti huu ni kuandaa shamba na kupanda mbegu ili kupata chakula. Ndungo (1998) anasema kuwa majukumu ya kiuana yalibainishwa wazi kutoka utotoni huku kila mwanajamii akifunzwa kazi anazopaswa kufanya kama mke au mume. Kazi za kiuna kwa hivyo zilibainika kuanzia utotoni. Wanaume walipaswa kuwa kichwa cha familia huku wakitarajiwa kukimu mahitaji ya famila zao. Ndungo anaendelea kusema kuwa ili wanaume waweze kutimiza na kukimu mahitaji ya familia walifanya kazi ya kulima na kuvua samaki huku wakitoa maamuzi katika familia.

Brittan (1997) anasema kuwa majukumu ya kiuana hayawezi kuwepo bila historia na tamaduni za jamii kujidhihirisha ndani yake. Kwa hivyo, kazi wanazozifanya wanaume na wanawake zinaweza kufasiriwa kivingine katika mpwito wa wakati. Kazi ya kulima sasa inafanywa na wanawake na wanaume wakishirikiana kama anavyoonyesha mwandishi katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi*

*Nyingine* katika hadithi ya "Kachukua Hatua Nyingine" Mzee Mavitu anaacha kazi ya kuuza cherehani na kujiunga na mkewe katika kilimo. Wanashirikiana kufanya kazi hii ya kilimo ili kuyakimu mahitaji ya pale nyumbani kwao. Msimulizi wa hadithi anasema, "Miaka miwili baadaye, Mavitu aliamua kuacha kazi ya kuuza cherehani huko mjini na kuja kijijini kupanda mahindi na maharage pamoja na mkewe" (uk 42). Upandaji wa mahindi na maharage ulimwezesha Mavitu kusaidiana na mkewe kuhakikisha kuwa wameyakimu mahitaji ya familia yao.

**2. 4 Hitimisho**

Katika sura hii tumeonyesha jinsi suala la mgao mpya wa kazi za mwanaume limeshughulikiwa na kuainishwa katika hadithi fupi teule. Maadamu kazi za mwanaume zimebadilika na kufikia sasa tumeona wanaume wanaoshiriki kazi ambazo awali zilikuwa zinafanywa na wanawake.

Kazi ya kulima ambayo ilitambuliwa na Ndungo (1998) kama kazi ya kitamaduni ya mwanaume katika utafiti huu inafanywa na mwanaume kwa ushirikiano na mwanamke. Mzee Mavitu kwenye hadithi ya "Kachukua Hatua Nyingine" anashirikiana na mkewe katika kilimo cha mahindi na maharage. Mgao mpya wa kazi za mwanaume unadhihirika hapa kwa sababu mwanamke pia anahusishwa katika kazi hii huku wakishirikiana na mwanaume.

Mwandishi wa hadithi ya "Dr. Strese" ameonyesha kuwa waahusika ambao wamesoma kama vile Daktari Strese na mume wa Hamnazo wameukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Mbaabu (1985) alitambua kazi ya kupika kama kazi ya kitamaduni ya mwanamke. Katika hadithi ya "Maeko", "Mke Wangu", na "Mayai Waziri wa Maradhi" kazi hii inafanywa na wanaume. Mapanya na Hamduni wanafanya kazi hii ya upishi ili wapate riziki na hatimaye kuwa wapishi bora. Kazi hii inapofanywa na mwanaume inaashiria mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume kwa sababu katika mgao wa kitamaduni, kazi hii ilifanywa na mwanamke.

Kama tulivyosema awali, Salim (1978) alitambua kazi za kuosha nguo na vyombo kama kazi za kitamaduni za mwanamke. Katika utafiti huu tumeonyesha kuwa kazi hii sasa inafanywa na wanaume. Kwa mfano, Hamduni kwenye hadithi ya "Maeko" anaosha nguo zake na za mkewe kwa hiari huku akifurahia kazi hiyo. Huu ni ushahidi kuwa mgao wa kazi za mwanaume umebadilika kwani kazi ambazo kitamaduni zilikuwa za mwanamke zinafanywa pia na mwanaume.

Imebanika katika utafiti huu kuwa waandishi wa hadithi ambazo tumehakiki ni wasomi ambao wameshawishiwa na elimu na mabadiliko ya kiwakati kusawiri wahusika ambao wameuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume. Baadhi ya wahusika katika hadithi fupi teule wamedhihirisha ukubalifu wa mgao huu mpya.

Hadithi ambazo tumechambua zimeonyesha kuwa mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume umebadilika na kuwa mpya. Hii ni kwa sababu hadithi hizi

zimeonyesha wahusika wa kiume na wa kike wanaofanya kazi za nyumbani kama vile kuosha nguo, vyombo na kupika bila kuzingatia tofauti za kijinsia.

Sura ya tatu imeonyesha sifa za wanaume ambao wanachukua mgao wa kazi mpya na mambo ambayo yamewasukuma kuuchukua.

# SURA YA TATU

## Sifa za Wanaume Wanaochukua Mgao Mpya wa Kazi

### 3.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia ilionyesha jinsi suala la mgao mpya wa kazi za mwanaume limeshughulikiwa na kuanishwa katika hadithi fupi teule. Sura hii ililenga kuchanganua sifa za wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Kwa mujibu wa TUKI (2013) sifa ni nomino inayomaanisha uzuri au ubaya wa mtu au kitu. Utafiti huu uliegemea fasili ya uzuri ili kuonyesha hulka za wanaume ambao wameuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Parson (2004) alifafanua mipaka ya majukumu ya kiuana. Alitofautisha majukumu ya kike na ya kiume na pia akaonyesha uvunjaji wa majukumu ya kiuana. Katika kielelezo chake, Parson (2004) alisema kuwa kazi za nyumbani hufanywa na mume na mke katika familia huku wakigawa shughuli za nyumbani bila kuzingatia jinsia. Kutokana na maelezo haya ya Parson (2004), yaonekana kuwa mgao huu wa kazi ni wenye usawa kwa sababu mwanaume anaweza kufanya ya mwanamke na mwanamke pia kufanya ya mwanaume.

Nadharia ya upembuzi ilisaidia katika kuonyesha sifa za wanaume ambao wameukubali na kuuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume. Woods (1997) alisema kuwa upembuzi ni njia tunayoathirika na kitu na kukipokea. Anaendelea

kusema kuwa nadharia ya upembuzi inachukulia mabadiliko kama jambo la kawaida na linalopatikana kila mara katika uhusiano wowote kama vile mgao wa kazi za kiuana. Kutokana na kauli ya Woods (1997) inabainika kuwa baadhi ya wanaume katika hadithi zilizochambuliwa wameathirika na mgao mpya wa kazi na kuupokea kwa njia chanya huku wakifanya kazi ambazo awali zilichukuliwa kuwa za kike. Sifa za wanaume hawa ambao wameathirika na kuupokea mgao mpya wa kazi kwa njia chanya zimebainishwa na kufafanuliwa hapa chini.

### 3.1 Ni Wasomi

Longhorn (2013) wanasema kuwa msomi ni mtu mwenye elimu kubwa hususan ya chuo kikuu. Kwa mujibu wa utafiti huu, msomi ni mtu ambaye amepata elimu rasmi. Baadhi ya wahusika ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume wamesoma. Mtu anapopata elimu, hutarajiwa kuonyesha mabadiliko katika maisha yake hasa jinsi anavyofanya mambo yake ukiwemo mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Mandy (2011) anasema kuwa, kwa miaka hamsini iliyopita majukumu mengi yenye usawa yameshuhudiwa katika jamii za kisasa. Akitumia utafiti linganishi alibainisha kuwa mabadiliko katika mgao wa kazi za kiuana yaliegemea usawa wa majukumu. Mabadiliko hayo yalisababishwa na upataji elimu, usuli wa mtu na uzoefu wa kibinafsi. Anaendelea kusema kuwa watu ambao wamesoma wanapaswa kuonyesha mtazamo wazi kuhusu kazi na suala la jinsia. Utafiti wa Mandy ulidhihirisha kuwa wanaume ambao wana elimu ya juu wanapendelea kazi

zenye usawa wakilinganishwa na wenzao ambao hawana elimu ya juu. Kutokana na maelezo ya Mandy (2011), kazi zenye usawa ni zile ambazo zinaegemea usawa wa majukumu hivi kwamba mwanaume anaweza kufanya kazi ambazo awali zilikuwa za kike kama vile kupika na kuosha vyombo.

Kama alivyosema Mandy (2011) mabadiliko ambayo yametokea katika mgao wa kazi katika miaka ya hamsini yamesababishwa na upataji elimu na uzoefu wa mtu. Kwa hivyo watu ambao wamesoma wanapaswa kuonyesha mtazamo wazi kuhusu kazi na uana. Utafiti wa Mandy ulidhihirisha kuwa wanaume ambao wana elimu ya juu wanapendelea kazi zenye usawa wakilinganishwa na wenzao ambao hawana elimu ya juu. Kulingana na matokeo ya utafiti huu wa Mandy tunaweza kusema kuwa elimu na uzoefu ni vigezo muhimu katika utekelezaji wa mgao mpya wa kazi za mwanaume. Aidha, Hamduni alipata uzoefu wa kazi ya upishi alipokuwa akifanya kazi kwenye hoteli. Hamduni alichukua mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa njia chanya kwa sababu anapika na kufua nguo pale nyumbani kwake. Mumewe Hamnazo amesoma na ni mwalimu mkuu wa shule ya upili.

Kutokana na ufafanuzi wa Mandy (2011) inabainika kuwa Hamduni amepata elimu na uzoefu kwa sababu anafanya kazi ambazo zilichukuliwa kuwa za kike. Hii ni kwa sababu mabadiliko katika mgao wa kazi yamesababiswa na upataji elimu na uzoefu kama alivyosema Mandy. Pia mwandishi wa hadithi ya "Maeko" anadhihirisha uzoefu wa Hamduni wa kufanya kazi ya kupika anapoonyesha jinsi Mhusika huyu alivyopata uzoefu wa upishi alipokuwa akifanya kazi kwenye

hoteli. Kwa sababu ya uzoefu huu, upishi na uandaaji wa vyakula haukuwa jambo geni kwa Hamduni. Dondoo lifuatalo linadhihirisha ukweli wa kauli hii;

> Alimradi baada ya muda usio kuwa mrefu, Duni alikuwa ameshaandika mezani herufi zote tamutamu, kalikali na kengakenga alimudu kuzitayarisha asubuhi ile. Kwani hii haikuwa kazi ngumu kwake, hasa ikitiliwa maanani uzoefu wake aliokuwa nao kama mpishi wa hoteli (uk 55).

Kauli ambayo tumenukuu hapo nyuma inaonyesha kuwa uzoefu ni mojawapo ya sababu ambazo zilimfanya Hamduni kufanya kazi za nyumbani kama vile kupika miongoni mwa zingine. Aidha, Hamduni aliupata uzoefu huu alipokuwa akifanya kazi ya upishi kwenye hoteli kama alivyosimulia mwandishi.

Kwenye hadithi ya "Dr. Strese" mwandishi ameonyesha mhusika wa kiume ambaye anaonekana kukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume. Mumewe Hamnazo amesoma hadi kufikia kuwa mwalimu mkuu wa shule ya upili. Mwanaume huyu amedhirihirisha ukubalifu wa mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa sababu anaichukua kazi ya kukimu mahitaji ya familia kama kazi ya mke na mume. Mkewe pia amesoma kwa sababu ni mwalimu wa shule ya msingi. Hata hivyo, mkewe angali anashikilia jadi za mgao wa kazi ambapo mwanaume ndiye anayehitajika kukimu mahitaji ya mke na watoto wake. Haya yanadhihirishwa na kauli ifuatayo kutoka kwenye hadithi ya "Dr. Strese" "Hamnazo alikuwa na ufahamu kwamba mume kazi yake ilikuwa kumkimu mkewe…" (uk42). Kauli hii

inaonyesha kuwa Hamnazo hajauchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume kwani angali anashikilia jadi za mgao wa kazi.

Ingawa Hamnazo hajashawishika na elimu rasmi ambayo ameipata kuchukua mgao mpya wa kazi, mumewe ameukubali mgao huu. Kwenye hadithi ya "Dr. Strese", msimulizi anasimulia, "Kwa sababu Hamnazo alikuwa mwalimu wa shule ya msingi, mumewe naye, hakutarajia kwamba hela yake pekee ndiyo ambayo ingewatekelezea mahitaji yao wote wawili" (uk 42). Hivyo basi, mumewe Hamnazo anaona ni vyema mkewe kushirikiana naye kutekeleza kazi ya kukimu mahitaji ya familia yao kwa sababu yeye pia anapata mshahara. Hata hivyo, Hamnazo alidinda kutekeleza kazi hiyo jambo ambalo lilisababisha mtafaruku baina yake na mumewe hadi wakatengana. Sura hii imejikita katika kuonyesha sifa za wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume. Hata hivyo, Hamnazo ni mhusika wa kike ambaye anatusaidia kujenga taswira ya mwanaume msomi ambaye anatekeleza mgao mpya wa kazi.

Isitoshe, katika hadithi hii ya "Dr. Strese" kuna mhusika mwingine ambaye amesoma. Mhusika huyu anaitwa Daktari Strese. Usomi wa Daktari Strese ulibainishwa na mwandishi aliposema, "Wakati dada zake wakiwa wamepata watoto na kuwalea pale nyumbani, Strese alikuwa amemaliza shule ya upili na hata kuingia chuo kikuu alikosomea kazi ya udaktari" (uk 43-44). Mtu ambaye amesoma hadi chuo kikuu anaafiki jina la msomi kama tulivyosema mwanzoni mwa sura hii. Daktari strese hapo awali alidhihirisha mgao wa kitamaduni wa kazi

za mwanaume kwa sababu yeye ndiye aliyekuwa mshauri na mpatanishi pale nyumbani kwao. Baada ya kifo cha babake alichukua usukani wa kuingoza familia. Mwishoni mwa hadithi, Daktari Strese anaukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume na kufuata ushauri wa mkewe kinyume na ilivyokuwa katika mgao wa kitamaduni

Utafiti huu umeteua hadithi kumi ambazo zimesaidia kufanikisha malengo ya utafiti. Kwenye sehemu hii, baadhi ya wanaume hawakudhihirisha sifa hii ya usomi. Usomi wa wahusika kama vile Maskini, Atanasi, Mzee Kadiri, Mavitu, Mapanya, Ukombozi na Sikujua haukujitokeza wazi. Hata hivyo, Daktari Strese, mumewe Hamnazo na Hamduni wamedhihirisha sifa hii ya usomi. Kwa sababu hii, hawa wametumika kufafanua sifa ya usomi huku wale wengine wakitumika kufafanua sifa zingine.

### 3.2 Ni Watambuzi wa Mantiki ya Mgao Mpya wa Kazi za Mwanaume

Mtambuzi ni nomino inayotokana na kitenzi tambua. Kwa mujibu wa Longhorn (2013) kutambua ni kufahamu kitu. Kadhalika, mantiki ni mtiririko wa fikra zilizopangwa ili kujenga hoja yenye kukubalika. Katika utafiti huu watambuzi wa mantiki ya mgao mpya wa kazi za mwanaume ni wahusika ambao wanafahamu na kushawishika na mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Kwa mujibu wa TUKI (2013) kushawishi ni kumpa mtu maelezo ili kutaka kumfanya akubali kufuata fikira au maelezo yako. Pia ni kumfanya mtu avutike kutenda jambo fulani. Utafiti huu uliegemea sana kwenye maana ya pili.

Wanaume wanaochukua mgao mpya wa kazi za mwanaume ni wale ambao wanavutika kwa urahisi kufanya kazi ambazo awali zilichukuliwa kuwa za kike. Mtu ambaye anashawishika kwa urahisi anaweza kukubaliana na mabadiliko bila utata. Mabadiliko ambayo yamejitokeza katika mgao wa kazi za mwanaume yanahitaji mhusika ambaye anaweza kukubaliana na ushawishi wenye mashiko kwa haraka kuyatekeleza.

Cherlin (1992) anasema kuwa kuibuka tena kwa ufeministi miaka ya sabini na mabadiliko katika elimu na mgao wa kazi za mwanamke ambazo zilifuata, kulisababisha mabadiliko katika mtazamo wa kila mwanajamii kuhusu mgao wa kazi. Kwa sababu hii, mgao wa kitamaduni unafifia na mgao mpya kukita mizizi katika jamii. Kulingana na kauli hii ya Cherlin, mgao mpya wa kazi za mwanaume pia umekita mizizi katika jamii inayoangaziwa na hadithi fupi teule. Pia, kutokana na maelezo haya ya Cherlin (1992) inabainika kuwa wanaume ambao wanafanya kazi zilizochukuliwa kuwa za kike wameshawishika na ufeministi kuchukua mgao mpya wa kazi ambao unaafiki usawa wa kijinsia.

Sikujua ni mwepesi wa kushawishiwa. Huyu ni mhusika wa kiume aliyesawiriwa na mwandishi wa hadithi ya “Macheo Mengine” iliyomo katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine.* Mwanzoni mwa hadithi hii, Sikujua alionekana kushika na kufuata mila na desturi za jamii yake. Kulingana na mila zao, mwana anapozaliwa na ulemavu angeuliwa kabla ya siku ya kumi tangu kuzaliwa kwake. Mkewe alipojifungua mtoto wa kiume, aliondokea kuwa

mlemavu. Wazee waliamuru mila yao itekelezwe na kwa hivyo maisha ya mtoto huyo yakawa hatarini.

Ingawa Sikujua hakutaka kukiuka mila zao, jambo hilo lilimuia gumu. Mkewe alishika usukani wa ulinzi na kumshauri mumewe wamlinde mtoto wao kwa kutumia sheria za katiba mpya. Alishawishika na kufuata ushauri wa mkewe na ndio maana alisema.”Ni macheo mengine” (uk 36). Maana ya maneno haya ni kuwa, wakati mwingine umefika ambapo Sikujua amekubaliana na ushauri wa mkewe wa kutoa ulinzi kwa mwanao aliyelemaa.

Kadhalika katika hadithi ya “Dr. Strese”, Daktari Strese anashawishiwa na mkewe kuukubali ushauri wake. Kwenye hadithi hii tunaelezwa kuwa Daktari Strese aliathirika sana na imani zake za jadi kwamba mwanaume kazi yake ni kukimu mahitaji ya familia na kwamba mtoto wa kwanza wa kiume ndiye hushika nafasi ya babake anapoondoka duniani. Imani hizi zilimpelekea yeye kujitwika mzigo mzito wa kuwalea dada zake na makinda wao hadi akakosa wakati wa kuanzisha familia yake mwenyewe.

Daktari Strese alitumia muda wake mwingi na hela zake kuwatimizia dada zake na makinda wao mahitaji yao ya kimsingi. Makinda hao walipofanikiwa kupata ajira waligura na kuwachukua mama zao huku wakimwacha Daktari Strese kwa upweke. Hatimaye aliingilia ulevi uliodhoofisha afya yake. Hata hivyo, alipata mke wa uzeeni ambaye alimwauni upweke na kumshauri kuacha ulevi. Ushawishi wa mkewe ulimfaa kisha akaacha ulevi na kurudia uwajibikaji kazini.

### 3.3 Wakubalifu

Kulingana na Longhorn (2013) kubali ni kitenzi kinachomaanisha pokea fikira, wito au tendo la mtu mwingine; kiri, ridhika, ungama na afiki . Mtu mkubalifu ni yule ambaye hupokea wazo au kuafiki jambo fulani kama vile mgao mpya wa kazi za mwanaume. Baadhi ya wahusika ambao wamepokea mgao mpya wa kazi za mwanaume ni wakubalifu kwani wameukaribisha mgao huu mpya kwa hiari yao wenyewe.

Wahusika wa kiume kama vile Hamduni kwenye hadithi ya "Maeko" katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* ni wakubalifu. Hii ni kwa sababu Hamduni aliuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa hiari yake mwenye. Katika ukurasa wa 55 alisema, "Hizi nitazifua jioni." Hamduni alikuwa akijisemea mwenyewe kuwa angezifua nguo ambazo aliziloweka kwenye mabeseni. Kauli hii inadhihirisha kuwa Hamduni aliamua mwenyewe kufanya kazi za nyumbani ambazo awali zilichukuliwa kuwa za wanawake. Haya yanamaanisha kuwa Hamduni ni mkubalifu.

Mhusika mwingine ambaye ameonyesha ukubalifu ni Sikujua. Huyu ni mhusika wa kiume ambaye amesawiriwa katika hadithi ya "Macheo mengine" iliyomo kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine.* Sikujua aliposhauriwa na Mwakwetu, mkewe kuungana naye katika kutumia sheria za katiba mpya kumlinda mwana wao, anaunga hatua hiyo huku akifurahi. Kinachomfurahisha Sikujua ni ile hali ya kujua kuwa Mwakwetu amemuani mzigo

ambao kwake ulikuwa mzito kama nanga. Hatimaye wanashikana mikono na mkewe huku akimwambia mkewe, “Ni macheo mengine” (uk 36). Hapa, Sikujua anamaanisha kuwa ni wakati mwingine ambapo amekubali ushauri wa mkewe na kwamba watatumia sheria za katiba mpya kumuokoa mwanawe asiuliwe.

Ukombozi pia alionyesha sifa hii ya ukubalifu. Hii ni kwa sababu yeye mwenyewe alijipangia kufanya kazi ambazo katika mgao wa kazi za kitamaduni tulitambua kuwa za jinsia ya kike. Ukombozi anafanya kazi ya kuandaa meza na kuosha vyombo pale jikoni. Kule kujitolea kufanya kazi hizi kunaonyesha kuwa amekubali mgao mpya wa kazi za mwanaume ambao unasisitiza ugawaji na utendaji kazi bila kuzingatia jinsia ya wahusika kama alivyosema Parson (2004). Ukubalifu wa Ukombozi unadhihirika katika hadithi ya “Mayai Waziri wa Maradhi” kupitia kwa kauli ifuatayo:

> Ukombozi alikuwa amesimama akiwapakia wenzake jamu na siagi kwenye mkate…Ukombozi aliwawekea chai kwenye vikombe na sukari. Walipomaliza kula walisimama kwa pamoja wakaenda jikoni kuosha vyombo walivyotumia (uk 69).

Mzee Atanasi, mhusika katika hadithi ya “Fumbo la Mwana” ameukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa sababu amemruhusu mkewe kufanya kazi ya biashara ili wasaidiane kutimiza mahitaji ya familia yao. Mwandishi alionyesha kuwa Atanasi ni mkubalifu kupitia kwa maneno ya Atanasi mwenyewe aliposema,

> Ninadamka kila siku majogoo ninakwenda kulima vikataa vyangu. Nikitoka huko mimi huyo vichakani kuwalisha mifugo. Mama yao hushinda marikiti huko Lukero; akichuuza samaki (uk 92-93).

Maneno ya Atanasi kwenye nukuu la hapo nyuma yanaonyesha kuwa hachukulii kazi hii ya kukimu mahitaji ya familia kama kazi ya mwanaume pekee bali amekubali kushirikiana na mkewe kutekeleza kazi hiyo.

### 3.4 Waadilifu

Ahmed na Wengine (2013) wanashikilia kuwa mtu mwadilifu ni mwenye maadili. Maadili ni wingi wa nomino adili. Kwa mujibu wa Ahmed na Wengine (2013) neno adili linamaanisha lililo jema. Kwa hivyo, mtu mwadilifu hutenda mambo ambayo yanaafiki maadili ya jamii yake. TUKI (2013) wanasema kuwa maadili ni mwendo mwema. Mwendo mwema hujumuisha kufanya kazi ili kukimu mahitaji ya kimsingi ya kila mwanajamii. Baadhi ya wahusika ambao wameuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume wameonyesha sifa hii ya uadilifu. Katika hadithi ya "Mke Wangu" mwandishi ameonyesha kuwa mtu mwadilifu ni mtu ambaye anafanya kazi ili kukimu mahitaji yake. Kwa mujibu wa mwandishi wa hadithi hii, mtu anayefanya kazi ndiye binadamu kamili. Anabainisha ukweli huu kupitia kwa mhusika wa kike aitwaye Aziza anaposema:

> Huyu ni binadamu kamili, kwani huyu ni mkulima, tena ni mfanyikazi. Yeye daima anafikiri kazi tu, maana kazi ndiyo maisha bora na jambo moja pekee tuliloumbiwa kulifanya hapa duniani (uk 9).

Tukirejelea maneno ya Aziza kwenye nukuu ambalo tumenukuu awali, binadamu kamili ni yule anayethamini kazi huku akifanya kazi yoyote ile ili kukimu mahitaji

yake. Huyu ndiye mtu mwadilifu kwa sababu anaafiki maadili ya jamii inayorejelewa katika hadithi hii. Mapanya ambaye ni mfanyikazi wa Aziza na Msimulizi ni mtu mwadilifu. Hii ni kwa sababu anafanya kazi ya kufua nguo pale nyumbani kwa msimulizi ili aweze kupata riziki yake.

Hadithi ya Maeko imeonyesha mwanaume kwa jina Hamduni ambaye alikuwa akifanya kazi ya upishi kwenye hoteli. Ni katika mazingira haya ya hotelini ambamo Hamduni alipata tajriba ya upishi bora. Hamduni aliishia kuipenda kazi hii na kuifanya pia pale nyumbani kwake kwa ustadi mkubwa. Mwandishi anaonyesha kuwa Hamduni alikuwa mpishi wa hoteli hivi:

> Aliwasha buli la umeme akateleka chai nzito ya maziwa, akaoka jiko la makaa na kutayarisha supu ya pweza na penye jiko la utambi akakaanga mayai. Alifungua jiko la kuhifadhia chakula, akatoa mandazi na chapati alizozipika jana yake. Vitu vyote hivi akaviwasilisha mezani. Baada ya muda usio mrefu, Duni alikuwa ameshaandika mezani herufi zote tamutamu, kalikali na kengakenga alizomudu kuzitayarisha asubuhi ile. Kwani hii haikuwa kazi ngumu kwake, hasa ukitilia maanani uzoefu wake aliokuwa nao kama mpishi wa hoteli (uk 55).

Baxter na Montgomery (1998) wanasema kuwa majukumu ya kiuana ni kitu kinachobadilika na kusababisha mume na mke kufanya kazi pamoja. Mabadiliko ambayo yameletwa na elimu rasmi na ushawishi wa kiuchumi na kisiasa yameleta ushirikiano katika utendaji kazi za kiuana. Mwanaume na mwanamke wanaposhirikiana kufanya kazi ya kukimu mahitaji ya familia, kushauriana na kufanya kazi za nyumbani pamoja wanadhihirisha uadilifu. Ushirikiano katika familia ni kipengele muhimu cha uadilifu.

Wahusika kama vile Mzee Atanasi katika hadithi ya "Fumbo la Mwana", diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* wanashirikiana na wake zao kutekeleza kazi ya kukimu mahitaji ya familia. Mkewe Atanasi anafanya kazi ya kuchuuza samaki huku Atanasi akilisha mifugo na kulima pale shambani. Yote haya yanachangia mapato ya familia ya Atanasi. Kwa hivyo, Atanasi anaafiki kigezo cha uadilifu kwa sababu anashirikiana na mkewe kukimu mahitaji ya familia yake.

Hadithi ya "Macheo Mengine" imeonyesha kuwa ushirikiano katika utafutaji suluhisho la masuala nyeti ni jambo muhimu. Mwakwetu, mkewe Sikujua alitumia hekima yake kumshirikisha mumewe kumlinda mwana wao dhidi ya mauaji kwa kutumia sheria za katiba mpya kama tulivyoonyesha katika sura ya pili. Mwanamke huyu ambaye ametwaa jukumu la kufanya kazi ya ulinzi wa mtoto wake ni mwadilifu kwa sababu alitumia mafunzo ya katiba mpya kumsadia mumewe kutatua suala gumu ambalo limkabili. Mwandishi ameonyesha uzito uliomkabili Sikujua kumlinda mwanawe kupitia kwa usemi wa Sikujua mwenyewe:

> Naelewa kwamba lazima auawe kabla ya siku ya kumi tangu kuzaliwa kwake. Kuhusu mahali, wakati na mbinu ya kumwulia mwanangu sijafanya uamuzi wa mwisho. Kama ujuavyo, sio rahisi kamwe kwangu kufanya uamuzi huu japo natambua sina njia ya kuikwepa mila hii yetu jadi. Kwa sasa najiona kutapatapa kama mfa maji (uk 31).

Usemi ambao tumenukuu hapo nyuma ulisemwa na Sikujua alipokuwa akizungumza na Majaliwa, mzee mwenzake kuhusu kuuliwa kwa mtoto wao mlemavu. Sikujua hakupendelea mila hiyo yao ya jadi. Kulingana na mila yao, alitakiwa kuamua jinsi ya kumwangamiza mtoto wao aliyelemaa lakini mwenyewe anasema kuwa hakuwa na njia ya kuikwepa mila hiyo. Bila shaka hili likuwa suala nyeti na zito kwake. Mwakwetu alimsaidia kutatua suala hilo kwa kumshauri kuhusu njia ya kukwepa mila hiyo yao ya jadi. Kushirikiana kwa Sikujua na mkewe kumlinda mwana wao dhidi ya mauaji kunaonyesha uadilifu kwa sababu wanahimiza ushirikiano huku wakilinda uai wa binadamu.

Mzee Kadiri katika hadithi ya "Ndoa ya Samani" alionyesha uadilifu aliposhirikisha mkewe katika kufanya uamuzi kuhusu posa la binti yao. Kama ilivyojitokeza katika hadithi hii, mzee huyu hakufanya uamuzi peke yake bali alimhusisha mkewe. Hii ni ishara ya ushirikiano katika familia katika kufanya maamuzi yanayowahusu watu wa familia hiyo. Mzee huyu alimshirikisha mkewe ili waweze kusema kwa usemi sawa. Msimulizi alieleza hili kupitia kwa Abu ambaye ni kijana wa kiume aliyepeleka posa kwa mzee Kadiri. Abu anasema, "Tulipowasili, mjomba wangu alimweleza baba yake Amali lengo la ujumbe wetu. Baba yake Amali akaingia jikoni kushauriana na mkewe" (uk 86). Kwa hivyo tunaweza kusema kuwa mzee Kadiri, babake Amali ni mwadilifu.

Uadilifu pia ulijitokeza kupitia kwa mhusika anayefahimika kama Ukombozi katika hadithi ya "Mayai Waziri wa Maradhi". Ukombozi ni mwadilifu kwa

sababu baada ya kuandaa kiamsha kinywa, anakusanya vyombo vyote na kuviosha. Kitendo hiki kinaonyesha uwajibikaji unaochangiwa na uadilifu. Mwandishi wa hadithi hii anaipa kauli hii mashiko anaposema,

> Ukombozi aliwapakia wenzake jamu na siagi kwenye mikate, akaweka chai kwenye vikombe na sukari. Wakala wakamaliza. Walipomaliza walisimama kwa pamoja wakaenda jikoni kuosha vyombo walivyotumia (uk 69).

Kutokana na maneno haya ya mwandishi, inabainika kuwa Ukombozi amewajibika katika kudumisha usafi pale nyumbani. Uwajibikaji ni kipengele cha uadalifu.

Bi. Cherehani na Bwana Pima ni waadilifu. Wahusika hawa ambao wameangaziwa katika hadithi ya “Kikaza” waliungana kutoa suluhu ya tatizo la Watekede kuhusu kikaza. Utatuzi wa shida zinazoikumba jamii fulani ni ishara ya uadilifu. Uadilifu ni dhana inayotokana na kitenzi adili chenye ya kutenda wema. TUKI (2013) wanasema kuwa adili ni kutenda haki na wema. Mtu mwadilifu ni mtu ambaye ana tabia ya kutenda haki na wema. Bi. Cherehani na Bwana Pima ambao mwandishi amesawiri kama washirika wakuu katika ushonaji wa kikaza walishirikiana katika kuwaeleza Watekede matatizo yaliyotokea katika ushonaji wa kikaza. Kwenye hadithi hii, mwandisi anaonyesha uadilifu wa Bwana Pima kwa kusema:

> Bwana Pima aligundua namna ukweli unavyoweza kuumiza, kuchoma, kukandamiza na hata kunyonga. Alipigana na nafsi kuumeza ukweli alioujua lakini haukumezeka, ulijisukuma nje. Pima alijizoazoa, akapata

> nguvu, ama ni kutokana na uzito wa mambo ambayo yangepasua moyo wake. Bwana Pima alilenga walivyotaka na kuuliza, "Mwakumbuka miaka miwili ilyopita? Bwana Mtajika alivunja masharti ya kikaza nasi tukafanya hisani na huruma (uk 45).

Haya yalikuwa maneno ya mwandishi akimrejelea Bwana Pima ambaye alikuwa akiwaeleza Watekede kitendawili cha kikaza. Kulingana na hadithi hii, kikaza kilikuwa na masharti kwamba ikiwa kiongozi ni mwanamke, mumewe hakuruhusiwa kukishika na ikiwa kiongozi ni mwanaume mkewe hakuruhusiwa kukishika. Pia kikaza hiki kilipaswa kuhifadhiwa kwa namna safi. Kiongozi wa Watekede alikuwa amevunja masharti haya kwa kumruhusu mwenzake kukishika kikaza. Haya yote Bwana Pima na Bi. Cherehani waliyafahamu ndiposa wakaamua kuwafahimisha Watekede ambao hatimaye wanamuondoa kiongozi huyo uongozini. Kushirikiana kwa Bwana Pima na Bi. Cherehani kufichua siri inayowaathiri Watekede ni kitendo kinachoonyesha uadilifu.

## 3.5 Wenye Mapenzi ya Dhati

Kwa mujibu wa Longhorn (2013) dhati ni nia thabiti ya kutenda jambo. Kwa hivyo, mtu ambaye ana mapenzi ya dhati huwa na nia thabiti ya kupenda na kwa hivyo hujitolea kwa vyovyote vile ili kudumisha mapenzi yake kwa mwenzake. Lipman (1961) anasema kuwa wanaume wanaoshiriki katika kazi za nyumbani huongeza mapenzi na urafiki katika uhusiano wao (ndoa). Kazi za nyumbani katika muktadha wa utafiti huu ni mgao mpya wa kazi za mwanaume ambao unajumuisha mwanaume kupika na kuosha nguo miongoni mwa mengine.

Wanaochukua mgao mpya wa kazi za mwanaume ni wenye mapenzi ya dhati kwa wenzao kama inavyojitokeza katika hadithi teule.

Wahusika kama vile Hamduni katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine,* hadithi ya "Maeko" ni wenye mapenzi ya dhati. Hamduni alimpenda mkewe kwa dhati. Anashiriki kazi za nyumbani kama vile kupika na kufua nguo ili aweze kudumisha mapenzi yake kwa mkewe. Hamduni anatekeleza kazi za nyumbani kama vile kuosha nguo, kupika na kuandaa meza. Kulingana na kauli ya Lipman (1961) hapo nyuma, wanaume wanaoshiriki katika kazi za nyumbani huongeza mapenzi na urafiki katika ndoa. Hivyo, inabainika kuwa Hamduni anaongeza mapenzi ya mkewe kwake kwa kufanya kazi za nyumbani huku akidhihirisha mapenzi ya dhati. Jamila, mkewe Hamduni pia anathibitisha haya kwa sababu alifurahishwa na upishi wa mumewe huku akimpenda zaidi. Mwandishi anadhihirisha mapenzi ya Jamila kwa Hamduni kwa kusema:

> Basi baada ya yote haya, Jamila alijikuta kila siku akiyahesabu maisha ya ndoa yake na Duni na akichelea kuyakosa. Si kwamba hakusimanzika kwa shida azipatazo ndani ya ndoa hii lakini alikuwa akijipa moyo kwamba ni wanawake wangapi wa aina yake ambao wanafanyiwa anayofanyiwa na mume wake? Hakuwa na hakika ikiwa wanawake wenzake walioolewa walikuwa na shida kama zake lakini alijua kwamba wengi wao hawazipati starehe azipatazo (uk 56).

Maneno ya msimulizi katika nukuu la hapo juu yanadokeza kwamba Jamila alimpenda mumewe na kufurahia kazi za nyumbani ambazo mumewe alikuwa akifanya.

Mzee Mavitu pia ana mapenzi ya dhati kwa mkewe. Mavitu alipoamua kuchukua hatua yoyote ambayo ingeathiri maisha ya familia yake kwa njia moja au nyingine alimshawishi mkewe kwa upendo. Mwandishi anadhihirisha haya kwa kusema;

> Mwanzoni Sakina alipingapinga laikini Mavitu akashikilia maneno yake aliyoyatomea vito vya mapenzi hapa na pale ili kumshawishi ( uk 41). Aliamua kuacha kazi ya kuuza cherehani huko mjini na kuja kijijini kupanda mahindi na maharage pamoja na mkewe (uk 42).

Maneno haya ya mwandishi, yanadokeza mapenzi ya dhati ya Mavitu kwa mkewe kwa sababu alishinikiza ushawishi wake na vito vya mapenzi. Pia, yaonekana kuwa mapenzi haya ndiyo yanayomfanya kuacha kazi ya kuuza cherehani huko mjini na kuungana na mkewe kupanda mahindi na maharage kijijini. Kwa hivyo, inabainaka hapa kuwa Mavitu alitaka kukaa karibu na mkewe huku wakisaidiana katika shughuli za kutafuta riziki kwa sababu alimpenda kwa dhati.

### 3.6 Wanyenyekevu

Kwa mujibu wa Ahmed na wengine (2013) mtu mnyenyekevu ni mtu afuataye maelekezo anayopewa bila matata; mtu aliye na tabia ya utiifu. Katika utafiti huu, mtu mnyenyekevu ni yule ambaye anadhihirisha tabia ya kutii na kufuata mgao mpya wa kazi za mwanaume. Baadhi ya wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume ni wanyenyekevu.

Mhusika wa kiume kwa jina Maskini katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*, hadithi ya “Uganga Wa Pete”, ananyenyekea kwa mkewe ili aweze kumfaa kwa ushauri aliohitaji zaidi. Pia, mwandishi wa hadithi hiyo ametudhihirishia kuwa Maskini alinyenyekea kila mara kwa mkewe ili ampe

ushauri hasa alipokuwa anakabiliwa na masuala nyeti yaliyohitaji uamuzi wa busara.

Katika hadithi ya "Maeko" Hamduni anaonekana kuwa mnyenyekevu. Alipomaliza shughuli za upishi na kuroweka nguo kwenye mabeseni, kwa hatua za unyenyekevu kabisa alinyatianyatia chumbani kumwamsha mkewe ili wapate kiamsha kinywa pamoja. Ile hali ya Hamduni ya kujitolea kwa hiari yake kuandaa vyakula vya kila aina na kuosha nguo zake na za mkewe inaashiria unyenyekevu mkubwa. Hii ni kwa sababu katika mfumo wa kibabedume ambao ulifuatwa na tamaduni nyingi za Kiafrika si rahisi mwanaume kufanya kazi kama hizi.

Wamitila (2003) anasema kuwa ubabedume ni mfumo wa kijamii unaomtukuza mwanaume huku ukimdhalilisha au kumdunisha mwanamke. Utukuzaji wa mwanaume huegemea mfumo wa kuumeni. Masinjila (1997) anasema kuwa mfume wa kuumeni ni mfumo wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ambao huhakikisha, huhifadhi na kuendeleza mamlaka ya mwanaume katika nyanja zote za maisha. Kauli ya Wamitila (2003) na Masinjila (1997) zinadokeza kuwa mwanaume amewekwa mbele na kutukuzwa katika jamii nyingi za Kiafrika. Kazi anazozifanya ni kazi za hadhi ili awze kudumisha hadhi na heshima katika familia yake.

Salim (1978) anasema kuwa katika familia ya Waswahili wanawake walitumia muda wao mwingi katika mazingira ya nyumbani huku wakifanya kazi za nyumbani. Kazi hizi zilijumuisha kufagia, kupika, kuosha nguo na vyombo,

kusaga unga, kusuka nywele na kufuma mikeka. Inabainika hapa kuwa kazi ya kupika, kuosha vyombo na nguo ni kazi za kitamaduni za mwanamke. Kwa hivyo, kazi hizi zinapofanywa na mwanaume zinaashiria mabadiliko. Awali katika hadithi hii, Hamduni alitawaliwa na ubabedume kwa sababu alikuwa akimchapa mkewe. uchapaji wa mke ni udhalilishaji wa mwanamke. TUKI (2013) wanasema kuwa chapa ni kupiga kwa kutia adabu au kuumiza. Hamduni alikuwa akimpiga mkewe na kumtia makovu. Hii ni ishara ya kumdhalilisha mwanamke ili kudumisha mamlaka yake kama mume. Lakini sasa, Hamduni amebadilika na kuuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume huku akimpenda mkewe na kumheshimu.

Aidha, hadithi ya "Ndoa ya Samani" imemsawiri mzee Kadiri kama mtu mnyenyekevu. Mzee huyu ni mnyenyekevu kwa sababu anafuata uamuzi wa mkewe bila kupinga. Ukweli huu unabainika kupitia kwa maneno yafuatayo, "Mzee Kadiri hakutaka kubishana na mkewe wala kujitia katika mipango yote ya arusi. Mshika usukani alikuwa Mama Zena" (uk 88). Maneno haya yanaashiria kuwa unyenyekevu wa Mzee Kadiri ulimfanya kumruhusu mkewe kushika usukani wa kuendesha familia yake. Yote yaliyoamuliwa na mkewe yeye alifuata bila pingamizi. Inagharimu unyenyekevu kwa mwanaume kufuata uamuzi wa mkewe na kumpa ruhusa ya kushika usukani katika mambo mbalimbali kwenye familia.

### 3.7 Waliopata Uzindushi wa Kiuchumi

Uzindushi ni nomino inayotokana na kitenzi zinduka. Kulingana na Longhorn (2013), kitenzi zinduka kinamaanisha toka katika hali ya kutoelewa jambo. Uchumi ni mfumo wa mapato na matumizi ya watu katika nchi (TUKI 2013). Katika utafiti huu, wanaume ambao wamezinduka kiuchumi ni wale ambao wametoka katika hali ya kutoelewa mgao mpya wa kazi za mwanaume. Pia, wanaume hawa wameukumbatia mfumo wa kiuchumi ambapo mwanaume anaweza kufanya kazi za kike ili kupata riziki kama inavyojitokeza katika fasili za maneno "uzindushi" na "uchumi. Baadhi ya wahusika wamepata uzindushi wa kiuchumi na kufahamu kuwa kitu muhimu cha kufuata si utamaduni wa kibabedume bali ni nguvu-hela za kuendeleza maisha. Hawa wametambua kuwa mwanaume anaweza kufanya kazi ambazo awali zilifanywa na wanawake ili kupata riziki.

Wahusika kama vile Mapanya katika hadithi ya "Mke Wangu" kwenye diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* wanafanya kazi za nyumbani kama vile kufua nguo na kupika ili kujipatia riziki. Woods (1997) anasema kuwa nadharia ya upembuzi inachukulia mabadiliko kama jambo la kawaida na linalopatikana kila mara katika uhusiano wowote kama vile mgao wa kazi za kiuana. Humwezeshe mtu kuyachukulia na kuyashughulikia mabadiliko kwa njia chanya. Pia, mtu huweza kushughulikia mikinzano kwa mtazamo bora. Mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume unakinzana na mgao mpya wa kazi za mwanaume. Hii ni kwa

sababu kazi ambazo mwanaume alifanya awali ni tofauti na zile anazofanya sasa katika mgao mpya. Kama ilivyobainika awali katika utafiti huu, katika mgao mpya wa kazi za mwanaume, wanaume wanafanya kazi ambazo katika mgao wa kitamaduni zilifanywa na wanawake.

Kadhalika, Conell (1987) alichanganua jinsi nadharia ya uana na vipengele vya ushawishi wa kijamii vinavyoweza kusababisha mabadiliko. Kumaanisha kuwa ikiwa ushawishi wa kijamii unaweza kubadili mgao wa kazi za mwanaume na mwanamke, kazi wanazofanya zinaweza kuchukua mkondo tofauti mpya. Kwa Conell, mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume yanasababishwa na ushawishi wa jamiii ambayo imepitia mabadiliko ya kiuchumi. Baadhi ya jamii zinazosawiriwa na waandishi wa hadithi ambazo zimehakikiwa katika utafiti huu zimeonyesha mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume. Hii ni kwa sababu hadithi zilizohakikiwa zimesawiri wanaume ambao wanafanya kazi tofauti na kazi zao za mgao wa kitamaduni.

Perry na Crouter (1990) wanasema kuwa kwa miaka kumi na mitano iliyopita, kumekuwa na ongezeko kubwa la wanawake walioolewa kwenye viwanda wakifanya kazi za ajira. Kutokana na ongezeko la wanawake kwenye viwanda, idadi ya wanawake wanaoshiriki jukumu la kukimu familia imeongezeka. Haya yamesababisha mabadiliko ya kiuchumi kwa sababu wanaume na wanawake wanafanya kazi sawa ili kukimu mahitaji ya familia.

Nukuu lifuatalo linadhihirisha kuwa Mapanya alikuwa akishiriki kazi za nyumbani ili kukimu mahitaji yake; "Nguo zake Aziza, Mapanya alikuwa akija kumchukulia kuenda kumfulia" (uk 5). Kwa kuzingatia maneno ya msimulizi tunaweza kusema kwamba mwanaume huyu alikuwa akifanya kazi za nyumbani kama kitegauchumi chake. Kwa hivyo, Mapanya amezinduka kiuchumi na kuupokea mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa njia chanya unaompa nguvu- hela za kukidhia mahitaji yake ya kimsingi.

Mhusika mwingine ambaye amezinduka kiuchumi ni Hamduni katika hadithi ya "Maeko", diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.* Hamduni alifanya kazi ya upishi katika hoteli moja aliyoajiriwa. Mhusika huyu alifanya kazi hii ili kukimu mahitaji yake. Kwa hivyo, ameukaribisha mgao huu mpya wa kazi za mwanaume baada ya kuzinduka kiuchumi. Vilevile amefahamu kuwa kazi ambazo awali zilionekana kuwa za jinsia ya kike pia zinaweza kumsadia mwanaume kupata riziki. Mwandishi anathibitisha kuwa Duni alikuwa ameajiriwa kama mpishi hotelini anaposema:

> Baada ya muda usio mrefu, Duni alikuwa ameshaandika herufi zote tamutamu, kali na kengakenga alizomudu kuzitayarisha asubuhi ile. Kwani hii haikuwa kazi ngumu kwake, hasa ukitilia maanani uzoefu wake aliokuwa nao kama mpishi wa hoteli"(uk 55).

Haya ni maneno ya mwandishi akimrejelea Hamduni. Hamduni alikuwa nyumbani kwake akiandaa chakula kazi ambayo alipata uzoefu wake alipokuwa akifanya kazi hoteni. Maneno haya ni ithabati tosha kuwa Hamduni aliweza

kuuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume kutokana na uzindushi wa kiuchumi kwa sababu awali aliifanya kazi hii ili kupata riziki. Hatimaye Hamduni aliendelea kufanya kazi ya upishi nyumbani kwake bila kuzingatia jinsia yake kama mwanaume na matarajio ya jamii nyingi za Kiafrika kuhusu majukumu ya kiuana.

Katika hadithi ya "Fumbo la Mwana", kwenye diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* Mzee Atanasi anamruhusu mkewe kwenda kuchuuza samaki marikiti huku naye akijihusisha na kilimo na ufugaji. Atanasi anaonekana kugundua kuwa kipato cha mkewe kikiunganishwa na chake kinaweza kuwasaidia katika kazi ya kukimu mahitaji ya kimsingi ya familia yao.

Mzee Mavitu pia amezinduka kiuchumi na kufahamu umuhimu wa kushirikiana na mkewe katika kutafuta riziki. Huyu ni mhusika wa kiume katika hadithi ya "Kachukua Hatua Nyingine", diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine.* Mwanaume huyu aliungana na mkewe kufanya kazi ya kilimo cha mahindi na maharage. Pia anamshirikisha mkewe katika kazi ya kukimu mahitaji ya familia kwa kuandamana naye kufanya kazi ya vibarua. Hii ni kwa sababu alifahamu kuwa mchango wa hela za mkewe unaweza kumfaa kutimiza mahitaji ya pale nyumbani. Mwandishi anasema, "Njia pekee ilikuwa moja sasa: kushiriki katika kazi za vibarua. Mara hii alilazimika kuandamana na mkewe" (uk 47). Kwa mujibu wa maneno haya, njia pekee ya kukimu mahitaji ya familia ya mzee Mavitu ni kushirikiana na mkewe kufanya kazi ya kukimu mahitaji ya familia hii.

### 3.8 Wenye Mwamko wa Usawa wa Kijinsia

Neno mwamko linatokana na kitenzi amka ambacho Ahmed na wengine (2013) wanasema kuwa ni kutoka katika hali ya kutoelewa jambo. Kwa mujibu wa TUKI (2013) mwamko ni ari au hamasa ya kutenda jambo. Kulingana na fasili hizi mbili, mwamko wa usawa wa kijinsia ni hali ya mhusika kutoka katika hali ya kutoelewa usawa wa kijinsia na kupata ari ya kufanya kazi zinazoafiki usawa wa kijinsia. Kwa hivyo, wahusika ambao wana mwamko wa usawa wa kijinsia ni wale ambao wamekumbatia usawa wa kijinsia na kuutilia maanani katika mgao wa kazi hasa kazi za mwanaume.

Parson (2004) kwenye muundo wa mfumo wa familia ambao ulipendelewa na jamii nyingi za Marekani miaka ya 1995 alilinganisha mielekeo na mitazamo ya jamii kuhusu majukumu ya kiuana na mipaka ya majukumu hayo. Alitumia miundo miwili ya mifumo ya familia ambapo muundo wa kwanza ulionyesha tofauti baina ya majukumu ya kike na ya kiume. Muundo wa pili ulieleza uvunjaji wa majukumu ya kiuana. Katika uvunjaji wa majukumu ya kiuana Parson alionyesha kuwa wanaume na wanawake wanagawa kazi bila kuzingatia jinsia. Kulingana na Parson, wanaume na wanawake hugawa kazi kwa kuzingatia usawa na kwa sababu hii, kazi zote za nyumbani hufanywa na mwanaume na mwanamke bila kuzingatia jinsia. Kauli hii inamaanisha kuwa wahusika katika mgao mpya wa kazi za mwanaume, wamepata mwamko wa usawa wa kijinsia. Kwa hivyo, wanagawa kazi kwa kuongozwa na usawa huku wakivunja imani za kitamaduni

kuhusu mgao wa kazi za mwanaume. Mwanaume na mwanamke sasa wanabadilishana kazi.

Katika hadithi ya “Macheo Mengine” kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine,* mkewe Sikujua ndiye anayetatua suala nyeti kuhusu ulinzi wa mwana wao. Baada ya kupata uzindushi wa kikatiba, Mwakwetu anamshirikisha mumewe kuchukua hatua za kikatiba za kumlinda mwana wao. Ushirikiano huu unawawezesha kutatua suala nyeti la kumuokoa mwana wao dhidi ya maangamizi ya jamii ya Wajadi. Pia Sikujua anafuata ushauri wa mkewe. Mwanaume kufuata ushauri wa mkewe ni ishara kuwa amepata mwamko wa usawa wa kijinsia.

Bever (1999) anasema kuwa kazi ya mwanaume ni kutimiza mahitaji ya kimsingi ya familia yake na kufanya maamuzi katika familia. Bever alikuwa akichunguza jinsi majukumu ya kiuana yamebadilika. Matokeo ya utafiti wake ni kuwa majukumu ya kiuana na mitazamo ya jamii kuhusu mgao wa kazi yamebadilika. Hii ni kwa sababu wanaume na wanawake hujadiliana juu ya majukumu ya kiuna katika familia tofauti na ilivyokuwa awali. Pia, wanaume na wanawake hujadiliana kuhusu jukumu la kufanya maamuzi katika familia. Isitoshe, utafiti wa Bever ulibaini kuwa, ingawa mgao wa kazi za wanawake unabadilika mitazamo ya kitamaduni kuhusu mgao wa kazi ingali inashikiliwa na wanaume na wanawake. Kazi ya kutoa ushauri kwa hivyo, ni ya mwanaume. Mwanaume anayekubali kufuata ushauri wa mkewe ni yule ambaye ameathirika na usawa wa kijinsia huku akikaribisha mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Mhusika mwingine ambaye anaonekana kupata mwamko wa usawa wa kijinsia ni mzee Atanasi. Huyu ni mhusika katika hadithi ya "Fumbo la Mwana" iliyomo katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*. Atanasi anadhihirisha mwamko wa usawa wa kijinsia kwa sababu ameukaribisha mgao mpya wa kazi za mwanaume. Katika mgao huu mpya, mwanamke ni mshirika katika kazi ya kukimu mahitaji ya familia yake.

Mbaabu (1985) anasema kuwa wanawake Waswahili hawakutwikwa mzigo wa kufanya kazi ya kuchumia familia bali kazi yao muhimu ni kupika na kufanya kazi zingine za nyumbani. Sinjiri Mukuba ambaye ndiye mwandishi wa hadithi ya "Fumbo la Mwana" naye amesawiri mwanamke ambaye anafanya shughuli za kibiashara huku akishiriki katika jukumu la kuchumia familia yao kinyume na Mbaabu. Kwa hivyo, uchukuzi wa majukumu ya wanawake na wanaume unaegemea itikadi za jamii mbalimbali za Kiafrika. Mabadiliko ambayo yametokea katika jamii kiuchumi na kiasiasa yamewaweka wanaawake sawia na wanaume huku vigezo vya kitamaduni vya mgao wa kazi za mwanaume vikikiukwa. Atanasi amekiuka vigezo hivi vya kitamaduni vya mgao wa kazi kwa sababu anamruhusu mkewe kufanya biashara ili kumsaidia kuichumia familia yake. Pia, yaelekea kuwa Atanasi anafuata usawa wa kijinsia. Hii ni kwa sababu kwake mwanaume na mwanamke wanashirikiana kufanya kazi zozote zile na hivyo kuukumbatia usawa wa kijinsia katika mgao wa kazi.

Mwandishi wa hadithi ya “Dr. Strese”” iliyomo katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* ameonyesha mumewe Hamnazo kama mhusika ambaye tayari amepata mwamko wa usawa wa kijinsia kwa kusema hivi:

> Kwa sababu Hamnazo alikuwa mwalimu wa shule ya msingi, mumewe naye hakutarajia kwamba hela yake pekee ndiyo ambayo ingewatekelezea mahitaji yao wote wawili (uk 42).

Kama inavyojitokeza katika maneno ya mwandishi hapo juu, mumewe Hamnazo alikuwa na matarajio kuwa Hamnazo angechangia katika shughuli za kukimu mahitaji ya familia yao. Hii ni kwa sababu Hamnazo pia alikuwa akifanya kazi ya malipo kama mwalimu wa shule ya msingi. Hata hivyo, Hamnazo alidinda kutimiza matarajio ya mumewe. Kama inavyojitokeza hapa mume wa Hamnzo amepata uzindushi wa usawa wa kijinsia na kwa sababu hii kutarajia mkewe kuwa mshirika katika kazi ya kukimu mahitaji ya familia. Woods (1997) anasema kuwa upembuzi ni jinsi tunavyoathirika na kitu na kukipokea. Mumewe Hamnazo anaonekana kubadili jadi za mgao wa kazi za mwanaume na kuuchukua mgao mpya ambao unasisitiza usawa katika utendaji kazi wa kila mwanajamii. Kwake mwanamke ambaye anafanya kazi ya ujira kama vile mkewe, anapaswa kuchangia katika kukimu mahitaji ya familia. Huo ndio usawa ambao anatarajia kwa mkewe.

Pia Maskini katika hadithi ya “Uganga wa Pete”, diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* anabainisha mwamko wa usawa wa kijinsia. Maskini anaomba ushauri kwa mkewe kuhusu masuala yaliyomzunguka. Kama tulivyoonyesha

katika sura ya pili, Maskini hangefanya jambo lolote bila kumshirikisha mkewe na kumuomba ushauri. Pia, Maskini hakuwa na kazi bali alitegemea kipato cha mkewe baada ya kufanya kazi ya kijungujiko. Maelezo haya yanadokeza kuwa Maskini ameukubali mgao wa kazi mpya za mwanaume huku akijua kuwa hata mwanamke anaweza kutoa ushauri na mwelekeo wenye busara.

Scanzoni (1979) anasema kuwa mwanaume anayekubali mabadiliko katika kazi za kiuana hufaidika kwa sababu hatalazimika kutimiza mahitaji ya kimsingi ya familia peke yake. Mwanaume huyu atasaidiwa na mkewe kutimiza mahitaji hayo. Mavitu katika hadithi ya "Kachukua Hatua Nyingine" anaonyesha kuwa ameukaribisha usawa wa kijinsia kwa sababu anamhusisha mkewe katika kazi ya utafutaji riziki. Jambo hili linamfaa kwa sababu wanasaidiana na mkewe kutekeleza kazi ya kuichumia familia ambayo ni kazi ya kitamaduni ya mwanaume.

### 3.9 Hitimisho

Katika sura hii sifa za wanaume ambao wameukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume zimebainishwa na kuchanganuliwa. Hadithi ambazo zimechanganuliwa hapa zimedhihirisha sifa nane za wanaume wanaoukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume. Utafiti huu umebainisha kuwa wanaume wanaoukubali na kuutekeleza mgao mpya wa kazi za mwanaume ni wasomi. Wanaume hawa wamepata ushawishi wa elimu ambao umewasukuma kuchukua

mgao huu wa kazi kwa njia chanya. Wale ambao wamepata msukumo wa elimu ni kama vile muwe wa Hamnzo na Daktari Strese.

Mgao wa kitamaduni ulibainisha kazi ya kupika kama kazi ya mwanamke. Hata hivyo, katika utafiti huu tumeonyesha kuwa kazi hii pia inafanywa na wanaume ambao wamepata uzindushi wa nguvu-hela. Pia inafanywa na wanaume ambao ni waadilifu na wangependa kuongeza mapenzi katika ndoa zao kama vile Hamduni.

Hali kadhalika, utafiti huu umeonyesha kuwa wanaume ambao wameukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume wameathirika na mwamko wa usawa wa kijinsia. Wahusika kama vile mume wa Hamnazo wanaoneka kuathirika na mwamko wa usawa wa kijinsia. Hii ni kwa sababu mwanaume huyu anatarajia kwamba mkewe pia angeshiriki kazi ya kukimu mahitaji ya familia kwa sababu yeye pia alikuwa anapata mshahara kama alivyokuwa akipata.

Sura hii pia imebainisha kuwa wanaume ambao wameukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume ni wakubalifu na wanyenyekevu. Sifa ya ukubalifu imedhihirishwa na wanaume ambao wanafanya kazi zilizokuwa za wanawake kwa hiari yao huku wakizipenda kazi hizo. Isitoshe, wanaochukua mgao mpya wa kazi wamedhihirisha unyenyekevu. Kwa hivyo, unyenyekevu na ukubalifu ni vipengele muhimu katika kuukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Sura ambayo inafuata imechunguza athari za kuchukua mgao mpya kazi za mwanaume.

# SURA YA NNE

## Athari za Kuchukua Mgao Mpya wa Kazi za Mwanaume

### 4.0 Utangulizi

Sura ya tatu ilibainisha sifa za wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume na mambo ambayo yamewasukuma kuuchukua mgao huo. Sura hii ililenga kuchunguza athari za kuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa mhusika mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili.

Kulingana na TUKI (2013) athari ni matokeo au alama inayobakia kwa muda baada ya mtu au kitu kufikwa na jambo fulani. Pia athari ni hali inayomwambukiza mtu tabia au mazoea yake. Ahmed na wengine (2013) wanasema kuwa athari ni hali imwambukizayo mtu tabia ama mazoea aliyonayo. Fasili zote mbili zinaangazia athari kama hali inayomkumba mtu baada ya kufikwa na jambo fulani kama vile mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume. Katika utafiti huu, athari ni alama inayobakia baada ya mwanaume kuukubali mgao mpya wa kazi.

Dunleavy (2007) anasema kuwa sasa mpaka asilimia 48% ya wafanyikazi wa Marekani ni akina mama. Pia, anasema kuwa thuluthi moja ya wanawake hupata mapato makubwa kuliko waume zao. Wanawake hawa hushiriki katika kazi ya kukimu mahitaji ya familia zao au wao ndio hutegemewa na familia zao. Utafiti huu wa Dunleavy unaonyesha kuwa kazi ya kukimu mahitaji ya familia

imebadilika kwa sababu wanawake pia wanashiriki kazi hii. Katika hadithi ambazo tuliteua, mabadiliko katika kazi hii yalibainishwa huku athari zake zikijitokeza.

Kwa mujibu wa Gitau (2005; 24) jamii za Kiafrika zimebadilika. Anaendelea kusema kuwa mojawapo ya mabadiliko ya kijamii, kiuchumi, kisiasa na kisheria yaliyotokea katika jamii za kisasa yanahusu mabadiliko ya majukumu na hadhi ya wanawake. Kazi wanazofanya wanawake na wanaume zinabadilika ili kuafiki mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa. Utafiti huu wa Gitau ulidokeza mabadiliko katika kazi za wanawake. Ikiwa kazi za wanawake zimebadilika ili kuafiki mabadiliko ya kijamii, kiuchumi na kisiasa, mgao wa kazi za mwanaume nao umebadilika kama ilivyojitokeza katika utafiti huu. Kutokana na mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume, sura hii ilijikita katika kuonyesha athari ambazo zilitokana na mabadiliko hayo.

Katika sura hii mtafiti alijadili athari za mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa kuziweka katika makundi yenye sifa zinazofanana. Katika kila kundi, mtafiti alijadili hadithi ambazo zimedhihirisha athari fulani mahsusi kwa mwanaume katika uchukuzi na utekelezaji wa mgao huu mpya wa kazi za mwanaume. Mgao mpya wa kazi za mwanaume umeleta athari zinazobainishwa hapa chini.

## 4.1 Huongeza Mapenzi

Wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume wameweza kuongeza mapenzi katika ndoa zao kama ilivyojitokeza katika utafiti huu. Keith

na Brubaker (1979) wakimnukuu Lipman (1969), wanasema kuwa wanaume hujihisi kuwa wa maana na wenye umuhimu wanaposhiriki majukumu ya nyumbani na pia husisitiza mapenzi katika uhusiano. Hamduni katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*, hadithi ya "Maeko", alikuwa anaongeza mapenzi kwa ndoa yake kwa kumpikia mkewe, Jamila vyakula vya kila nui. Kama inavyojitokeza katika hadithi hii, Jamila alifurahia sana upishi wa mumewe. Hamduni pia alionekana kushiriki kazi ya kuosha nguo kwa ustadi mkubwa. Mwandishi ameonyesha kuwa Jamila aliwekwa kwenye ndoa hiyo na matendo ya mumewe ya kumpikia na kumuoshea nguo kupitia kwa maneno yafuatayo:

> Mapishi ya Duni siku zote yalimfurahisha Jamila na mara zote alikuwa anajisahau kula kiasi chake…baada ya yote haya, Jamila alijikuta kila siku akiyastahabu maisha ya ndoa yake na Duni na kuchelea kuyakosa. Alijua kwamba wanawake wenzake walioolewa hawazipati starehe azipatazo (uk 56).

Kama anavyodokeza mwandishi katika kauli yake hapo juu, Jamila alipendezwa na mapishi ya mumewe na kuyafurahia maisha yake ya ndoa. Pia, mwandishi amebainisha kuwa wanawake wengine ambao walikuwa wameolewa hawakupata starehe ambazo Jamila alikuwa akipata kwa mumewe. Jamila mwenyewe, pia anakiri kuwa si wanawake wengi waliolewa wanaozipata starehe anazozipata kwa mumewe. Starehe hizi ni kama vile kupikiwa vyakula vya kila nui na kuoshewa nguo. Maelezo ya msimulizi katika dondoo la hapo nyuma yanaonyesha kwamba matendo ya Hamduni ya kumpikia na kumwoshea nguo mkewe yaliweza

kumweka kwenye ndoa hiyo. Hii ni kwa sababu alifahamu kuwa si wanawake wengi walioolewa hufanyiwa kazi hizo na waume zao.

Isitoshe, baada ya Duni kumaliza upishi na kulowesha nguo kwenye mabeseni anaenda kwenye chumba cha malazi ambako anaamwamsha mkewe aliyekuwa amelala. Wawili hao wanashikana nyonga kuelekea bafuni. Hii ni ishara ya mapenzi yanayodhihirishwa na maneno yafuatayo ya mwandishi, "Huko bafuni nao, walitumia muda mwingi wakichezea maji na kurushiana mapovu, hata walipotoka bado vicheko vyao na matani viliweza kusikika hadi ukumbuni" (uk 56). Kulingana na kauli ya Keith na Brubaker (1979) wanasema kuwa wanaume wanaposhiriki majukumu ya nyumbani husisitiza mapenzi katika uhusiano. Kulingana na kauli hii ya Keith na Brubaker pamoja na maelezo ya msimulizi wa hadithi ya "Maeko" kuhusu Jamila na mumewe, inabainika kuwa mwanaume ambaye amechukua mgao mpya huweza kuongeza mapenzi kwa ndoa yake.

**4. 2 Huleta Ushirikiano baina ya Mwanaume na Mwanawake**

Kwa mujibu wa Longhorn (2013) ushirikiano ni hali au tendo la watu wawili au zaidi kuungana na kusaidiana katika shughuli. Katika ushirikiano, wanaume na wanawake wanaungana kufanya kazi au mwanaume anamhusisha mkewe katika utendaji kazi ambazo kitamaduni zilikuwa za mwanaume. Wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume wamedhihirisha ushirikiano baina yao na wenzao wa kike hasa katika familia.

Baxter na Montgomery (1998) wanasema kuwa majukumu ya kiuana ni kitu kinachobadilika na husababisha mume na mke kufanya kazi pamoja. Kwa mujibu wa maneno haya ya Baxter na Montgomery na fasili ya ushirikiano hapo juu, inabainika kuwa mume na mke wanapofanya kazi pamoja wanaonyesha ushirikiano. Utafiti huu umewachukulia wanaume ambao wanawashirikisha wake zao kufanya kazi za kike au za kiume kama ambao wamechukua mgao mpya wa kazi huku wakidhihirisha ushirikiano.

Parson (2004) anasema kuwa, katika familia za sasa, hakuna mhusika katika familia anayepewa kipaumbele kutoa suluhisho na maamuzi katika familia. Wanaume na wanawake wanashirikiana katika kutoa suluhisho kuhusu jambo lolote linaloleta utata katika familia na maisha kwa jumla. Kauli hii ya Parson inabainisha kuwa katika familia za sasa badala ya mwanaume kutegemewa katika utoaji suluhu, anamshirikisha mwanamke (mkewe) katika jukumu hilo nyeti. Kwa hivyo, kila mmoja wao anajihisi kuwa wa maana katika familia huku uhusiano wao ukiwa bora zaidi.

Katika hadithi ya “Kachukua Hatua Nyingine”, diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* mama na baba ya Sakina wanashirikiana kumpa ushauri binti yao. Hadithi hii inashughulikia kipindi cha miaka ya sitini. Kipindi hiki kimesheheni upigaji hatua wa elimu rasmi katika nchi za Afrika huku kazi ya kushauri ikifanywa na mwanaume kwa ushirikiano na mwanamke. Kauli ifuatayo inadhihirisha haya: “Sakina aliacha kazi yake ghairi ya ushauri wa mamake na

babake.  Wote walimshauri kwa kila nia…"( uk 41).   Kwa mujibu wa dondoo hili, mwanaume na mwanamke wanaposhirikiana katika kumpa binti yao ushauri huu matokeo yake ni uhusiano mwema na ushirikiano katika familia.

Pia, katika diwani hiyo hiyo ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* hadithi ya "Kachukua Hatua Nyingine" Mzee Mavitu anashirikiana na mkewe kufanya kazi ya kilimo ili kusaidiana kukimu mahitaji ya familia yao.  Ndungo (1998) anasema kuwa kazi ya kulima na kuvua samaki ilikuwa kazi asili ya mwanaume ambayo ilimwezesha kukimu mahitaji ya familia yake.  Katika utafiti huu, kazi hii inafanywa na mwanamke na mwanaume huku ikileta mafanikio na ushirikiano katika familia kwani mahitaji ya familia yanatimizwa na mwanamke kwa kushirikiana na mwanaume.

Katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* kwenye hadithi ya "Kikaza", Bwana Pima na Bi. Cherehani wanashirikiana katika kutoa suluhisho kuhusu kitendawili cha kikaza.  Mwanaume na mwanamke katika hadithi hii wanafanya kazi sawa kwani wote wawili wanakamilishana katika kutoa suluhisho.  Bwana Pima alikuwa akichukua vipimo vya kikaza huku Bi. Cherehani akishona kikaza kulingana na kipimo alichopewa.  Kulingana na maelezo haya yaelekea kuwa kila mmoja wao ni mshirika muhimu katika kushona kikaza.  Ithibati ya haya inapatikana kwenye usemi ufuatao, "Bi. Cherehani na Bwana Pima walikuwepo kutoa suluhisho na kusaidia kutegua kitendawili" (uk 42).  Usemi huu unaashiria kuwa mwanaume anashirikiana na mwanamke ili waweze kufanya kazi muhimu

ya kutoa suluhisho kuhusu masuala yenye utata katika jamii zao tofauti na ilivyokuwa hapo awali ambapo mwanaume pekee ndiye aliyetafuta suluhisho la mambo yenye utata.

Kadhalika, Mzee Kadiri katika hadithi ya “Ndoa ya Samani”, kwenye diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* anashirikiana na mkewe kutafuta suluhu kuhusu arusi ya binti yao. Anapoletewa posa anawaomba wenye ujumbe kumpa muda ili aweze kumuuliza mkewe uamuzi wake. Anayoamua Mama Zena, Mzee Kadiri anayaunga mkono. Mwandishi anaonyesha haya kupitia kwa msimulizi hivi, “Tulipowasili, mjomba wangu alimweleza baba yake Amali lengo la ujumbe wetu. Baba yake Amali akaingia jikoni kushauriana na mkewe" (uk 86). Kama inavyojitokeza hapa, Mzee Kadiri alimhusisha mkewe katika kutoa uamuzi kuhusu masuala muhimu kwenye familia yao. Haya ni kinyume na familia zilizotawaliwa na ubabedume. Hii ni kwa sababu mwanaume pekee ndiye aliyekuwa na uwezo wa kufanya maamuzi katika familia yake lakini hapa Mzee Kadiri anamhususha mkewe katika shughuli hiyo.

### 4.3 Mgao Mpya wa Kazi za Mwaanaume Husababisha Utoshelevu wa Moyoni

Utoshelevu ni nomino inyotokana na kitenzi tosheka kinachomaanisha ridhika. Kwa mujibu wa Ahmed na wengine (2013) neno tosheka linamaanisha ridhika na maelezo yaliyotolewa ama kiasi ulichopata; ridhika. Katika utafiti huu utoshelevu wa moyoni ni hali ya mtu kutosheka, kuridhika na kupata utulivu wa moyo anapofanya kazi ambazo awali zilichukuliwa kuwa za kike kwa hiari yake. Katika

hadithi ya “Maeko” kwenye diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi* Nyingine, msimulizi wa hadithi anadhihirisha utoshelevu kwa kusema,

> Duni akazikunjakunja nguo chafu zote ndani ya nyumba, nyingi zikiwa ni zile za mkewe, na kwenda nazo uwani. Akazitenganisha nguo za rangi pake kisha akaziroweka katika mabeseni tofauti. “Hizi nitazifua jioni”, alijiambia mwenyewe (uk 55).

Maneno ambayo yamenukuliwa hapo nyuma yanaonyesha jinsi Hamduni (Duni) alivyojitolea kufanya kazi za pale nyumbani. Pia anafanya kazi ya kuosha nguo kwa kutumia utaratibu bora kwani anazitenganisha kulingana na rangi zake. Kadhalika, anajisemea mwenyewe kuwa angezifua nguo hizo jioni hiyo. Kule kujisemea mwenyewe ni ishara kuwa mwenyewe aliamua kufanya kazi hii kwa sababu aliridhika kuosha nguo zake na mkewe. Pia, Hamduni alionekana kufurahia kazi hii na kuifanya kwa ustadi mkubwa. Anaporidhika kufanya kazi ya kuosha nguo na kuifurahia anapata utulivu wa moyo.

Fauka ya haya, diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine,* hadithi ya “Uganga wa Pete”, maskini anapata utulivu wa moyo baada ya kushauriwa na mkewe kwa sababu masuala yaliyomkabili yalikuwa nyeti huku akilemewa kufanya uamuzi. Kwa hivyo, mkewe anapomsadia kufanya uamuzi wa busara anapata suluhu na hivyo basi kupata utulivu wa moyo. Mwandishi anadokeza kuwa mkewe Maskini alikuwa mtatuzi wa masuala sugu ambayo yalimlemea yeye. Haya yanajitokeza kwenye kauli ifuatayo;

> Mfalme akaamua kumwita tena Maskini aje aseme vile vilivyoibwa vimefichwa wapi. Jukumu hili lilikuwa gumu na zito na lilimfadhaisha

> sana Maskini… Kwa mara nyingine akaomba arudi nyumbani kwake mpaka keshoye… Kule kufika nyumbani aliomba ushauri kutoka kwa mkewe (uk 104).

Kama inavyojtokeza katika usemi wa msimulizi wa hadithi ya “Uganga wa Pete” hapo juu, Maskini aliona jukumu la kutoa suluhisho kama ambalo lilikuwa gumu na zito kwake. Alifadhaika sana ndiposa akaamua kuomba ushauri wa mkewe kama ilivyokuwa desturi yake. Hivyo, inabainika kuwa Maskini alipata utulivu wa moyo kwa kumshirikisha mkewe katika kazi ya kumshauri katika masuala nyeti. Ugumu na uzito wa jukumu lililomkabili Maskini ulimpa mfadhaiko wa moyo kama inavyojitokeza kwenye dondoo lilonukuliwa awali. Kupatikana kwa suluhu kwa hivyo, kulimpa utulivu moyoni kwa sababu ushauri wa mkewe uliridhisha.

Kulingana na kauli ambazo zimeangaziwa hapo juu, imebainika kuwa baadhi ya wanaume ambao huchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume hupata utulivu wa moyo. Hii ni kwa sababu baadhi ya kazi ambazo wanashiriki sasa huweza kuwaauni mzigo ambao peke yao wangehisi kuwa mzito. Phillips (2008) anasema kuwa jinsi mtu anavyoishi na kuchukua mgao tarajiwa wa kazi huathiri afya yake. Kauli hii inamaanisha kuwa mgao wa kazi za mwanaume unaweza kusababisha athari chanya au hasi katika maisha ya mwanaume.

Dr. Strese katika Hadithi ya “Dr. Strese” kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* anapitia mateso mengi ya moyoni kwa kushikilia mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume ambao humtaka mwanaume kuwa kichwa cha familia na kubeba mizigo yote ya familia. Kichwa cha familia kiliandamana na

majukumu mengi aliyopewa mwanaume na jamii yake. Osore (2008) anasema kuwa kutoka utotoni mafunzo katika jamii yalijikita katika uana. Wanaume walichukuliwa kuwa vichwa vya familia huku wakipewa majukumu ya kutimiza mahitaji ya wake na watoto wao. Mgao wa kazi za kitamaduni uliegemea mfumo wa kuumeni.

Masinjila (1997) anasema kuwa mfumo wa kuumeni ni mfumo wa kijamii, kisiasa na kiuchumi ambao huhakikisha, huhifadhi na kuendeleza mamlaka ya mwanaume. Mfumo huu humpa mwanaume jukumu la kutoa uamuzi kuhusu masuala nyeti katika familia yake. Hii ni kwa sababu yeye ndiye kichwa cha familia. Kauli hii ya Masinjila inadokeza kuwa mfumo uliotumiwa kugawa kazi za kitamaduni ulimpa mwanaume heshima na kuhakikisha kuwa mamlaka ya mwanaume yamedumishwa. Kazi ambazo mwanaume angefanya zilikuwa kazi za hadhi ikiwemo kazi ya kuwa kichwa cha familia. Ingawa katika mgao wa kitamaduni kazi ya kuwa kichwa ilichukuliwa kama ambayo ina hadhi, kazi hii ni nzito. Uzito wa kazi hii unatokana na ukweli kwamba, mwanaume atalazimika kufanya juu chini kutimiza mahitaji ya familia yake.

Daktari Strese alichukua usukani wa kuwa kichwa cha familia ya baba yake na kusadia dada zake kulelea watoto wao. Hatua hii ya Daktari Strese inaonekana kama kujitwika mzigo mzito kama ilivyodhihirika katika hadithi ya "Dr. Strese". Maneno yafuatayo yanadhihirisha kuwa Daktari Strese alijitwika mzigo mzito;

> Strese alipoanza kufanya kazi tu, ilimbidi achukue majukumu ya babake pale nyumbani. Aliazimia kutotafuta nyumba yake binafsi katika eneo

> lililokuwa karibu na sipitali, bali abaki pale nyumbani ili asaidie (uk44). Miaka mitatu baada ya kifo cha wazazi wake, Daktari Strese alijikuta akilea watoto watano, kuwakimu kwa karo na mahitaji yao yote. Yeye mwenyewe alikuwa na umri wa miaka 35 na alikuwa hajafikiria kuanzisha familia yake mwenyewe. Mawazo yake yalikuwa kuwakimu dada zake na wapwaze (uk 46).

Dondoo la hapo juu linaonyesha kuwa Daktari Strese aliuchukua mgao wa kitamaduni wa kazi ambapo kichwa cha familia kilikuwa cha mwanaume. Yeye kama kifungua mimba wa wazazi wake alilazimika kuchukua usukani baada ya wazazi wake kuzeeka na kufariki mtawalia. Kama inavyoonekana kwenye kauli zilizonukuliwa hapo nyuma, Daktari Strese alilichukulia jukumu hili kwa uzito hadi akachelewa kuanzisha familia yake. Alitumia wakati na mali yake yote kuwalelea wapwa zake mpaka akakosa wakati wa kuoa na kuanzisha familia yake. Kama ilivyobainika katika utafiti huu, hatimaye dada zake na wapwa zake waligura baada ya kuwalea na kuwasomesha huku wakimwachia upweke. Upweke huu ulimsababishia ulevi wa kupindukia kwa sababu hakuwa na yeyote wa kuishi naye pale nyumbani.

Daktari Strese alitwikwa mzigo wa malezi eti kwa sababu alivaa kofia ya babake kama anavyosema dadake Daktari Strese. Pia, yeye mwenyewe alikwamilia mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Haya yalimsababishia Daktari Strese sononeko la moyoni. Dadake Daktari Strese anasema, “Ni kweli kaka twashukuru lakini hilo lilikuwa jukumu lako. Wewe ndiwe uliovaa kofia ya baba”. Maneno haya yanamaanisha kuwa Daktari Strese alichukua usukani wa kuindeleza familia

ya babake na kwa hivyo kulingana na dada zake, ilimbidi kuwalelea pamoja na watoto wao. Anapoacha mgao huo wa kitamaduni na kuukaribisha mgao mpya wa kazi za mwanaume, anapata afueni kiafya.

Daktari Strese alikuwa ameathirika kiafya lakini anapopewa ushauri na nasaha na mkewe anabadili mwelekeo wake wa kutamauka na kujizoazoa tena ili kuishi maisha bora. Dondoo lifuatalo linathibitisha haya. "Daktari Strese aliweza kumskiza mkewe na kurekebisha maisha. Alipunguza ulevi na kurudia juhudi kazini kwake" (uk.50). Kwa mujibu wa dondoo hili, Daktari Strese aliweza kufaidika na kuendeleza maisha yake kwa njia bora zaidi baada ya kuuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume. Daktari Strese aliweza kupewa ushauri nasaha na mkewe na kubadili maisha yake.

Isitoshe, katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine,* hadithi ya "Macheo Mengine", Sikujua ambaye ni mhusika wa kiume anapata afueni katika suala nyeti lililomkabili baada ya mkewe kumsadia katika uamuzi kuhusu mwana wao ambaye alikuwa mlemavu. Mwakwetu alimshauri watafute msaada wa sheria ili kumlinda mwana wao asiuliwe kwa sababu ya ulemavu. Sikujua ameshachukua mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa sababu hashikilii utamaduni unaombebesha yeye mzigo mzito wa kutoa suluhu na mwelekeo katika masuala nyeti. Kwa hivyo anapata utulivu wa moyo kwa sababu wanatafuta suluhisho la suala nyeti kwa ushirikiano na mkewe. Mzigo wa kutoa suluhu na

ulinzi wa familia uliokuwa mzito kwake sasa umerahisishwa kwa kuchuja tamaduni za mgao wa kazi za mwanaume na kuchukua mgao mpya wa kazi.

**4. 4 Mgao Mpya wa Kazi Huleta Ufanisi Katika Maisha ya Mwanaume**

Kwa mujibu wa Scanzoni (1979) mwanaume hubadili majukumu yake kwa sababu atafaidika kutokana na mabadiliko hayo. Kulingana na Scanzoni, wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi wamefanya hivyo kwa sababu wanafaidika na mgao mpya kwa njia moja au nyingine. Kimani (2003) anasema kuwa mwanamke hakuwa na uwezo wa kutoa maoni yake kuhusu jambo lolote katika familia. Kauli hii ya Kimani inamaanisha kuwa mwelekeo kuhusu jinsi ya kufanya mambo mbalimbali katika familia ulitolewa na mwanaume. Kwa hivyo, kazi ya kushauri ni jukumu la kitamaduni la mwanaume na inapofanywa na mwanaume kwa kushirikiana na mwanamke inakuwa jukumu katika mgao mpya wa kazi za mwanaume. Kama tulivyodhihirisha katika sura ya pili, kazi hii sasa inafanywa na mwanaume na mwanamke kwa ajili ya ufanisi wa familia.

Spence na Hahn (1997) wanasema kuwa majukumu ya kiuana yanabadilika na imani za wanajamii sasa zimekuwa za kisasa. Wanajamii hawa wamechuja baadhi ya tamaduni zikiwemo za mgao wa kazi za mwanaume na kuumbua mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Wilbon na Simpson (2009) wanashikilia kuwa kupitia kwa ufasili barabara wa kitu, kitu hicho hupata maana yake na umahiri. Wanaendelea kusema kuwa jinsi jamii inavyofasili na kutoa maana ya kitu fulani,

kitu hicho hupata maana kulingana na muktadha husika. Wilbon na Simpson walisisitiza utoaji maana mpya wa majukumu ya mwanaume.

Spence na Hahn (1997) na Wilbon na Simpson (2009) wanadhihirisha mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume ambao sasa umechukua mkondo mpya. Mwanaume ambaye ameukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume haoni ugumu wa kuomba ushauri wa mkewe katika mambo nyeti bali huchukulia ushauri huo kwa njia chanya. Matokeo yake huwa ni ufanisi katika mambo mbalimbali kwenye maisha ya mwanaume na familia yake kwa jumla. Ili kudhihirisha ukweli wa kauli hii, mifano kadha imetolewa kutoka kwenye hadithi tulizoteua.

Katika hadithi ya "Uganga wa Pete" kwenye diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine,* mhusika wa kiume kwa jina Maskini alikuwa akiomba ushauri kwa mkewe katika mambo yaliyomlemea kusuluhisha huku yakimpa wasiwasi mwingi kama tulivyoonyesha kwenye sura ya pili. Ushauri huu wa mkewe uliweza kumfaa kila mara na kumpa fursa ya kuendeleza maisha yake vilivyo. Maneno yafuatayo yanadhihirisha ukweli wa kauli hii:

> Jukumu hili lilikuwa gumu na zito na lilimfadhaisha sana Maskini. Hakujua kama ajitoe vipi. Kwa mara nyingine, akaomba arudi nyumbani kwake mpaka keshoye… Kule kufika nyumbani aliomba ushauri kutoka kwa mkewe. (uk 104.)

Maneno ambayo tumenukuu awali yanamaanisha kuwa Maskini alifahamu fika kuwa mkewe angeweza kumkwamua katika masuala nyeti ambayo yalimlemea na hatimaye kufanikiwa maishani. Pia yaonekanaka kuwa hii haikuwa mara ya

kwanza kuomba ushauri wa mkewe katika masuala nyeti. Kutokana na maelezo haya inabainika kuwa Maskini amechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume. Maskini anapochukua mgao mpya wa kazi na kumshirikisha mkewe katika kumshauri anapata wadhifa mkubwa serikalini katika nchi yao. Hatimaye Maskini aliishia kuwa tajiri mtajika na mwenye heshima kuu nchini kwao. Huu ni ufanisi katika maisha yake na mkewe. Haya yanadhihirishwa na maneno yafuatayo ya msimulizi wa hadithi ya "Uganga wa Pete" "Mfalme akampa Maskini wadhifa mkubwa serikarini… Maskini aliinukia kuwa tajiri mwenye heshima kuu nchini kwao." (uk.109)

Maneno ya msimulizi kwenye nukuu la awali yanasaidia kuonyesha kuwa Maskini alipata ufanisi baada ya kuchukua ushauri wa mkewe kusuluhisha masuala yaliyomkabili mfalme. Baada ya Maskini kumsaidia mfalme, mfalme alimpa wadhifa mkubwa serikalini na mwishowe akawa tajiri mtajika. Huu ni ufanisi katika maisha ya Maskini na mkewe. kulingana na maelezo haya, tunaweza kusema kuwa mwanaume anapokaribisha mgao mpya wa kazi za mwanaume huwa anapata ufanisi wa maisha. Hii ni kwa sababu mambo ambayo ni magumu yanatatuliwa kwa kumhusisha mkewe katika utoaji wa ushauri. Kila mmoja anashiriki katika kutoa suluhu na kuyafanya mambo kuwa mepesi katika familia yao. Katika mgao huu mpya wa kazi hakuna mhusika anayeachiwa mzigo wa kutatua masuala nyeti peke yake bali mwanaume na mwanamke wanashirikiana kwa hayo.

Aidha, kazi ya kuosha nguo ambayo ni kazi ya kitamaduni ya mwanamke katika jamii nyingi za Kiafrika sasa inafanywa hata na wanaume. Kwa mujibu wa utafiti huu, huu ni mgao mpya wa kazi za mwanaume ambao unampa ufanisi katika maisha yake na ya familia yake kwa jumla. Wanaume ambao wamevuliwa ubabedume na mabadiliko ya kiuchumi wamechukulia jukumu hili kama kazi ambayo inaweza kuwasaidia kupata riziki. Mapanya ambaye ameajiriwa kufanya kazi ya nyumba anachangamkia kazi hii kama ambayo inafanikisha maisha yake kwa kumpa ujira wa kila mwezi. Ujira huo humwezesha kukimu mahitaji yake ya kimsingi na kwa hivyo kufaidika na kazi hii ambayo kitamaduni huchukuliwa kuwa ya wanawake.

**4 .5 Humfanya Mwanaume Kujihisi kuwa wa Maana katika Familia yake**

Lipman (1961) anasema kuwa mwanaume anaposhiriki majukumu ya nyumbani na kugawa kazi za pale nyumbani na mkewe hujihisi kuwa wa maana. Inaamanisha kuwa mwanaume huyu anapata kitulizo fulani kwa kuhusika moja kwa moja katika kazi ambazo awali zilichukuliwa kuwa za mwanamke. Katika hadithi ya “Maeko”, diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* Hamduni ambaye ni mhusika wa kiume anaonekana kujihisi kuwa mtu wa maana anaposhiriki kazi ya kuosha nguo za mkewe na pia kupika vyakula vya kila aina pale nyumbani mwao. Yeye mwenyewe anajituma kufanya kazi hizi. Pia anaoneka kuwa na uzoefu wa kufanya kazi hizi. Msimulizi wa hadithi ya “Maeko” katika ukurasa wa 55 alisema kuwa Duni alichukua muda mfupi kuandalia mkewe meza na kuiremba na kila aina ya chakula kwa sababu kazi hiyo

haikuwa ngumu kwake. Pia, msimulizi alisema kuwa Duni alipata uzoefu wa kazi ya upishi alipokuwa akifanya kazi kwenye hoteli. Msimulizi anasema, "… hii haikuwa kazi ngumu kwake, hasa ukitilia maanani uzoefu wake aliokuwa nao kama mpishi wa hoteli" (uk 55).

Kulingana na kauli ambayo tumenukuu hapo juu, Duni anaonekana kujihisi kuwa mtu wa maana sana anapompikia mkewe. Hii ndiyo sababu anaandika herufi zote pale mezani ili kuonyesha ustadi wake katika upishi. Vilevile mwandishi anaonyesha haya kwa kusema, "Mapishi ya Duni siku zote yalimfurahisha Jamila na mara zote alikuwa anajisahau kula kiasi chake, ni lazima avimbiwe tu" (uk.56). Kauli hizi mbili zinaonyesha kuwa Duni aliweza kumfurahisha mkewe katika mapishi yake na kwa sababu hii anaishia kujihisi kuwa mume bora kwa Jamila.

**4. 6 Wanaume Wanaochukua Mgao Mpya wa Kazi za Mwanaume Hufaidika**

Scanzoni (1979) anasema kuwa mwanaume hubadili majukumu yake kwa sababu atafaidika kutokana na mabadiliko hayo. Maneno haya ya Scanzoni yanadokeza kuwa mwanaume anaweza kukubali kubadili majukumu ambayo anayafanya ikiwa atapata faida kwa kufanya hivyo. Vivyo hivyo katika utafiti huu, mwanaume ambaye anaukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume anaweza kuukubali kwa sababu atafaidika na mgao huo mpya. Hii ni kwa sababu hatalazimika kujisumbua sana ili kufaulu katika maisha na pia kujiweka juu kihadhi. Kadhalika, Scanzoni (1979) anaendelea kusema kuwa mwanaume huyu huweza kupunguziwa mahitaji yasiyo ya kimsingi. Ina maana kuwa mwanaume ambaye anamshirikisha

mwanamke katika utekelezaji wa baadhi ya kazi kama vile kukimu familia hupumzishwa kwa kusaidiana na mkewe kwenye shughuli za kukimu familia. Kwa hivyo mwanaume hatakuwa na mzigo mzito wa kuhakikisha ameikimu familia yake kwani mkewe pia atashiriki katika kazi hii ya kukimu familia.

Ukweli kuwa mwanaume ambaye ameukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume hufaidika unathibitishwa katika hadithi ya "Fumbo la Mwana" kwenye diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine".* Mzee Atanasi anafaidika kwa kuukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa sababu wanashirikiana na mkewe kutafuta mbinu za kukimu mahitaji ya familia yao. Kazi ya kukimu mahitaji ya familia ni kazi ya kitamaduni ya mwanaume kama anavyosema Bever (1999). Kwa hivyo, mwanamke hakuwa na shinikizo la kutimiza mahitaji ya kimsingi ya familia.

Mwanamke anaposhiriki kazi ya kukimu familia, inaashiria mabadiliko katika mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Mabadiliko haya ni bora zaidi kwani mwanaume anasaidiwa na mkewe kukimu mahitaji ya familia yao. Atanasi anasema kuwa alidamka kila asubuhi kulima na kulisha mifugo huku mkewe akichuuza samaki marikiti (uk.92-93). Maneno haya ya Atanasi yanamaanisha kuwa Atanasi na mkewe walisaidiana kukimu mahitaji ya famila. Kutokana na maelezo haya, mkewe Atanasi pia anashiriki kazi ya kukimu mahitaji ya familia yao kwa kufanya biashara ya kuchuuza samaki. Anaposhiriki kazi hii anamtua mumewe mzigo mzito wa kukimu mahitaji ya familia peke yake. Matokeo ya

ushirikiano wa Atanasi na mkewe katika kazi ya kukimu mahitaji ya familia ni kwamba Atanasi anafaidika kwani kazi hii sasa inakuwa nafuu kwake kwa sababu anasaidiwa.

**4. 7 Husabisha mikinzano**

Baxter na Montgomery (1998) walitambua misingi miwili ya upembuzi ambayo ni ukinzano na utaratibu wa mambo. Ukinzano ni ushindani wa vitu viwili kama vile mgao wa kitamaduni na mgao mpya wa kazi za mwanaume. Msingi wa pili ni utaratibu wa mambo unaoshikilia kuwa upembuzi unaendelea na unakua. Wanaendelea kusema kuwa majukumu ya kiuana ni kitu kinachobadilika na husababisha mume na mke kufanya kazi pamoja. Kulingana na maelezo haya ya Baxter na Montgomery, hali ya ukinzano hutokea baina ya mgao wa kitamaduni na mgao mpya wa kazi za mwanaume wakati mume anachukua mgao mpya wa kazi huku mke akigandama kwenye mgao wa kitamaduni wa kazi. Hamnazo alionekana kukataa katakata kuchukua mgao mpya wa kazi ambapo mwanamke pia ni mshirika katika kukimu mahitaji ya familia. Mawazo ya Hamnazo yangali kwenye mgao wa kitamaduni ambapo mwanaume peke yake ndiye aliyekuwa na jukumu hili zito la kukimu mahitaji ya familia yake.

Kama tulivyosema awali katika utafiti huu, jamii nyingi za Kiafrika zilifuata mfumo wa ubabedume ambapo mwanaume ndiye aliyekuwa na mamlaka ya kutoa uamuzi katika familia yake. Wanawake walibaki kuwa watekelezaji wa yale ambayo yaliamuliwa na wanaume. Katika utafiti huu, imebainika kuwa jukumu

hili la kutoa uamuzi pia linafanywa na wanawake huku wanaume wakifuata yote yaliyoamuliwa na wake zao. Haya hayakukubalika katika mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Kwa hivyo, haya ni mabadiliko yanayoleta mkinzano baina ya mgao wa kitamaduni wa kazi na mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Pia, jukumu la kuwa kichwa cha familia ni jukumu asili la mwanaume, jukumu hili liliendana na utafutaji wa riziki ili kukimu mahitaji ya familia. Kama ilivyojitokeza katika hadithi ya "Dr. Strese", Daktari Strese alichukua jukumu hili na kujitwika mzigo wa kuwalelea dada zake na watoto wao jambo ambalo lilimsababishia sononeko la moyo na pia kuchelewa kuanziasha familia yake mwenyewe. Jukumu hili lilisababisha ukinzani wa ndani kwa ndani kwa sababu Daktari Strese ndiye aliyekuwa akitoa ushauri kwa dada zake lakini baada ya mambo kumwendea mrama ilibidi afuate ushauri wa mkewe na akapata afueni kiafya.

Kanogo (2005) anasema kuwa katika jamii ya Wakikuyu, kubadilika kwa mgao wa majukumu kati ya wanawake na wanaume kulichangiwa na ukoloni. Vita vya Mau Mau vilifanya wanaume kwenda msituni kupigana nao wanawake wakabaki wakifanya majukumu ya kike na kiume hali ambayo iliendelea hata baada ya uhuru kupatikana. Maelezo haya ya Kanogo yanaonyesha kuwa wanawake walianza kufanya kazi ambazo zilifanywa na wanaume kama vile kufanya uamuzi katika familia na kukimu mahitaji ya familia. Mgao huu mpya unakinzana na mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume.

Kazi za nyumbani kama vile kuosha nguo na kupika zilitambuliwa na baadhi ya wahakiki kama vile Ndungo (1998), Osore (2008) na Salim (1978) kama kazi ya kitamaduni ya mwanamke. Katia utafiti huu, imebainika kuwa kazi hizi pia zinafanywa na wanaume. Ile hali ya wanaume kufanya kazi ambazo awali zilifanywa na wanawake inazua mkinzano wa mgao mpya wa kazi za mwanaume na mgao wa kitamaduni.

Kuna athari hasi ambazo zinaletwa na mgao huu mpya wa kazi za mwanaume. Mojawapo wa athari hizi ni kusababisha migogoro katika ndoa. Kazi ya kukimu familia ilitambuliwa na baadhi ya wahakiki kama vile Ndungo (1998) kuwa kazi ya asili ya mwanaume. Kutokana na upataji wa elimu, mabadiliko ya kiuchumi na kisiasa, wanawake pia wanashiriki kazi hii. Wanaume ambao wamekubali mabadiliko katika kazi hii wanapata afueni ya maisha kwa sababu wanasaidiwa kukimu familia zao. Wanawake ambao wangali wanashikilia kuwa kazi ya mume ni kukimu mke wanaondokea kuzozana katika familia. Katika hadithi ya "Dr.Strese" mhusika wa kiume ambaye ni mumewe Hamnazo anaonekana kukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume lakini mkewe angali anashikilia mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume.

Kama tulivyoona katika hadithi hii ya "Dr. Strese", mumewe Hamnazo amesoma huku akishikilia kuwa mwanamke pia anapaswa kushiriki katika kukimu mahitaji ya familia hasa ikizingatiwa kuwa mwanamke huyo anafanya kazi ya ujira. Kwa

upande mwingine mwandishi amesawiri mhusika wa kike, Hamnazo kama ambaye anadhihirisha mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Katika mgao huu, mwanaume ndiye mkimu wa mke na watoto wake. Kwa Hamnazo, mwanaume anapaswa kukimu mahitaji ya mke na watoto wake. Tofauti hizi zilisababisha mkinzano uliosababisha mgogoro wa ndoa ya Hamnazo na mumewe. Hatimaye, mgogoro huo unasabisha kusambaratika kwa ndoa hiyo.

**4. 8 Hitimisho**

Sura hii ililenga kuchunguza athari za mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa mhusika mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Hadithi teule kutoka kwenye diwani za *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine*, *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* na *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* zimetumika kudhihirisha athari za mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Sura hii ilibainisha kuwa mwanaume ambaye ameukaribisha mgao mpya wa kazi za mwanaume huongeza mapenzi katika ndoa yake. Kama tulivyoonyesha katika sura hii, Hamduni aliweza kuongeza mapenzi katika ndoa yake na Jamila kwa kuukaribisha mgao mpya wa kazi za mwanaume. Hamduni alikuwa akimpikia Jamila vyakula vya kila aina jambo ambalo lilimfurahisha Jamila sana. Upishi wa Hamduni na kumwoshea Jamila nguo ulimfurahisha Jamila na kumfanya ampende zaidi. Kwa hivyo, mgao huu umeongeza mapenzi ya Hamduni kwa mkewe.

Pia, sura hii ilionyesha kuwa mgao mpya wa kazi za mwanaume huleta ushirikiano baina ya mwanaume na mwanamke. Mavitu na Sakina walishirikiana kufanya kazi ya kilimo ili kusaidiana kukimu mahitaji ya kimsimgi ya familia yao. Isitoshe, mgao mpya wa kazi za mwanaume huleta utoshelevu wa moyoni. Wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume hupata utoshelevu wa moyo kwa sababu baadhi ya kazi ambazo anashiriki huweza kumwauni mzigo ambao peke yake atahisi kuwa mzito. Dr. Strese ambaye awali aliteseka kwa kuukwamilia mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume alipata afueni baada ya kuukaribisha mgao mpya.

Aidha, ilibainika katika sura hii kuwa mgao mpya wa kazi za mwanaume huleta ufanisi katika maisha ya mwanaume na familia yake kwa jumla. Hii ni kwa sababu mwanaume ambaye ameukaribisha mgao mpya wa kazi za mwanaume haoni ugumu wa kuomba ushauri wa mkewe katika mambo nyeti bali huchukulia ushauri wa mkewe kwa njia chanya. Matokeo ya kuuchukulia ushauri wa mkewe kwa njia chanya huwa ni ufanisi katika mambo mbalimbali katika maisha ya mwanaume huyo na familia yake kwa jumla. Maskini alionekana kuomba ushauri wa mkewe kila mara mambo yalipomwia magumu na matokeo yake yakawa ya manufaa kwake na mkewe.

Mgao mpya wa kazi za mwanaume pia humfanya mwanaume kujihisi kuwa mtu wa maana sana katika familia yake. Kama tulivyosema awali katika sura hii,

mwanaume ambaye ameuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume hupata kitulizo fulani anaposhiriki kazi ambazo awali zilichukuliwa kuwa za kike. Hamduni anajihisi kuwa mtu wa maana anapompikia Jamila vyakula vya kila aina na kumfanya ale zaidi ya kiwango chake. Kwa mujibu wa msimulizi wa hadithi ya "Maeko" upishi wa Hamduni daima ulimfurahisha Jamila. Jambo hili lilimfanya Hamduni kujihisi kuwa mtu wa maana kwa sababu alifahamu kuwa upishi wake uliweza kumpendeza mkewe.

Hali kadhalika, mwanaume ambaye ameuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume hufaidika kwa kufanya hivyo. Baadhi ya kazi kama vile ya kukimu mahitaji ya familia zinapofanywa na wanawake huweza kumfaidi mwanaume kwa sababu atapumzishwa kwa kusaidiana na mkewe kufanya kazi hii. Atanasi alifaidika kwa kuukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume hasa alipomshirikisha mkewe katika kutafuta riziki ili kukimu mahitaji ya familia yao. Pia, mgao mpya wa kazi za mwanaume husababisha mikinzano. Mgao wa kitamaduni na mgao mpya wa kazi za mwanaume unakinzana kwa sababu yale mwanaume anafanya sasa ni tofauti na yale alikuwa akifanya katika mgao wa kitamaduni. Kwa mfano, mwanaume kufuata yote anayoagiziwa na mkewe hayakukubalika katika mgao wa kazi wa kitamaduni ambao uliegemea mfumo wa ubabedume.

Hata hivyo, imebainika katika utafiti huu kuwa mgao mpya wa kazi za mwanaume husababisha mgogoro na kusambaratisha ndoa hasa pale ambapo mwanaume

ameuchukua mgao mpya lakini mkewe amekwamilia mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume.

Sura inayofuata inatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti na kujibu maswali ya utafiti kulingana na malengo ya utafiti na uchambuzi wa diwani zilizoteuliwa. Hatimaye, sura hii imetoa mapendekezo ya utafiti zaidi.

# SURA YA TANO

## Muhtasari, Matokeo, Mchango na Mapendekezo

### 5 .0 Utangulizi

Utafiti huu ulihusu mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi za Kiswahili. Utafiti huu ulikuwa na madhumuni ya kubainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili kutoka kwenye diwani tatu teule za hadithi fupi.

Kutoka katika diwani ya *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine* hadithi tatu zilichanganuliwa. Katika diwani ya *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine* hadithi nne zilihakikiwa. Kadhalika, kutoka kwenye diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine* hadithi tatu ziliteuliwa. Kwa jumla, mtafiti alihakiki hadithi kumi. Hadithi zilizohakikiwa ni zile ambazo ziliafiki malengo ya utafitli huu.

Pamoja na haya, utafiti huu ulikuwa na malengo matatu. Lengo la kwanza lilikuwa kubainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi za *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine, Damu Myeusi na Hadithi Nyingine* na *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine*. Lengo la pili lilikuwa kuchanganua sifa za wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili na tajriba ambazo zimewafanya kuuchukua. Lengo la tatu lilikuwa kuchunguza athari za kuchukua mgao mpya wa

kazi za mwanaume kwa mhusika mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili.

Katika kushughulikia malengo haya, utafiti huu uliongozwa na nadharia ya uana na nadharia ya upembuzi. Mihimili minne ya nadharia ya uana ilitumiwa kuonyesha jinsi jamii inavyomkuza mwanaume kuanzia utotoni hadi anapoelewa anayopaswa kutekeleza kama mwanaume. Pia, utafiti huu uliweza kutambua mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume kwa kuegemea mihimili ya nadharia ya uana. Nadharia hii iliwezesha utafiti huu kudhihirisha kuwa kazi ya kupika, kuosha vyombo, kunadhifisha boma na kuosha nguo ni kazi za kitamaduni za kike katika jamii nyingi za Kiafrika.

Fauka ya haya, mihimili mitatu ya nadharia ya upembuzi ilitumiwa kuonyesha mabadiliko ya mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume na mikinzano baina ya mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume na mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili.

Ilibainika katika utafiti huu kuwa mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume ambao unakinzana na mgao mpya wa kazi za mwanaume umechukua mkondo mpya. Kazi wanazofanya wanaume katika hadithi zilizoteuliwa ni tofauti na kazi walizokuwa wakifanya awali. Utafiti huu umegendua kuwa mgao mpya wa kazi za mwanaume ni bora zaidi kuliko mgao wa kitamaduni kwa sababu unaleta ushirikiano, kuongeza mapenzi katika ndoa, kuleta ufanisi wa familia na kuleta utoshelevu wa moyoni miongoni mwa athari zingine. Kwa jumla, mihimili ya

nadharia ya upembuzi imewezesha utafiti huu kugundua kuwa baada ya mikinzano ya mgao wa kitamaduni na mabadiliko ya kiwakati, mgao mpya wa kazi za mwanaume umepatikana na ndicho kitu bora na kikamilifu zaidi.

Kadhalika sura hii imetoa muhtasari wa matokeo ya utafiti sura baada ya nyingine na kujibu maswali ya utafiti kulingana na malengo ya utafiti na uhakiki wa diwani zilizoteuliwa. Hatimaye, sura hii imeeleza mchango wa utafti na kutoa mapendekezo ya utafiti zaidi.

**5. 1 Muhtasari**

Utafiti huu ulilenga kubainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Tasnifu hii imewasilishwa katika sura tano. Sura ya kwanza ambayo ndiyo utangulizi wa utafiti imeshughulikia mada ya utafiti, maswali na malengo ya utafiti na kueleza sababu ambazo zilimfanya mtafiti kufanya utafiti huu. Hali kadhalika, sura hii imeshughulikia usuli wa utafiti na kujadili nadharia zilizoongoza utafiti huu. Pia, maelezo kuhusu yaliyoandikwa kuhusu mada yametolewa. Hatimaye, mbinu za utafiti alizotumia mtafiti kufanikisha utafiti huu zimefafanuliwa.

Sura ya pili ililenga kubainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Katika sura hii, mtafiti aliweka msingi wa mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa kujadili mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Hapa, mtafiti alifafanua kazi za kitamaduni za mwanaume. Aidha, alijadili mgao wa kazi za mwanaume ambao ni kinyume cha mgao wa kitamaduni. Tulionyesha

kazi ambazo mwanaume anafanya sasa kinyume na ilivyokuwa katika mgao wa kitamaduni na zile ambazo anafanya kwa kushirikiana na mwanamke.

Sura ya tatu ililenga kuchanganua sifa za wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili na tajriba ambazo ziliwafanya kuuchukua. Sifa hizi zilifafanuliwa kwa kina katika sura hii. Utafiti huu ulibaini kuwa wanaume ambao wameuchukua mgao mpya wa kazi ni wasomi, wepesi wa kushawishiwa, wakubalifu, waadilifu, wenye mapenzi ya dhati, wanyenyekevu, waliopata uzindushi wa kiuchumi na wenye mwamko wa usawa wa kijinsia. Wanaume hawa huchukulia mgao mpya wa kazi kwa njia chanya na kufanya kazi ambazo kitamaduni zilichukuliwa kuwa za kike kwa hiari yao.

Sura ya nne ililenga kuchunguza athari za kuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume. Katika sehemu hii, tulionyesha jinsi ambavyo mgao mpya wa kazi za mwanaume umeathiri maisha ya wanaume ambao wameuchukua na jamii zao kwa jumla. Wanaume hawa wameweza kuongeza mapenzi katika ndoa zao, kujihisi kuwa watu wa maana katika familia zao, kufaidika na mgao huo, kupata utoshelevu wa moyoni, kupata ufanisi wa maisha, ushirikiano baina ya mwanaume na mwanamke. Hata hivyo, mgao huu mpya wa kazi umeweza kusababisha mikinzano baina ya mgao huu mpya na mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume. Hali hii ya mikinzano pia imesababisha migogoro ya ndoa na hatimaye kuchangia katika kuvunjika kwa ndoa kama vile Hamnazo na mumewe

walivyotengana baada ya mumewe Hamnazo kushikilia mgao mpya wa kazi za mwanaume huku Hamnazo akikwamilia mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume.

Sura ya tano ni hitimisho la tasnifu. Sura hii imetoa utangulizi wa sura na muhtasari wa kila sura kulingana na malengo ya sura hizo. Maelezo yametolewa kulingana na malengo ya utafiti wetu. Sura hii pia imeeleza matokeo ya utafiti na mchango wa ufati. Hatimaye, sura hii imetoa mapendekezo ya utafiti ambao unaweza kufanywa baadaye. Sehemu inayofuata ya sura hii inaeleza matokeo ya utafiti.

**5. 2 Matokeo ya Utafiti**

Utafiti huu ulilenga kuyatimiza malengo matatu. Lengo la kwanza lilinuia kubainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Utafiti huu uligundua kuwa mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume umebadilika na kuwa mpya kwa sababu ya mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na ya kijamii. Hali kadhalika utafiti huu ulibaini kuwa mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume yamechangiwa pakubwa na mikataba mbalimbali inayotetea usawa wa kijinsia kupitia kwa mashirika mbalimbali. Mikutano mbalimbali ya kimataifa imefanyika kuanzia mwaka wa 1975 hadi mwaka wa 1995 kutetea haki za wanawake na kuhimiza usawa wa kijinsia katika nyanja zote za maisha. Kwa hivyo, mikutano hii ilisababisha mabadiliko ya falsafa za watu kuhusu mgao wa kazi.

Isitoshe, utafiti huu uligundua kuwa mabadiliko ya kiuchumi yaliyotokea baada ya majilio ya enzi ya ukoloni katika jamii nyingi za Kiafrika yamebadilisha majukumu na hadhi ya wanawake kwani sasa wamekuwa na wajibu wa kukimu na kuitunza familia sawia na wanaume. Katika hadithi zilizochanganuliwa kazi ambazo zimechukua mkondo mpya ni pamoja na kazi ya kushauri, ulinzi, upishi, kuosha nguo, kuosha vyombo, kutoa suluhisho, kukimu mahitaji ya familia, kazi ya kulima na kazi ya kuwa kichwa/kiongozi katika familia. Mkondo huu mpya umedhihirika kuwa bora zaidi kwa sababu mwanaume na mwanamke wanaweza kushirikiana kuiendeleza familia kwa kusaidiana katika baadhi ya kazi kwa ufanisi wa familia.

Aidha, mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume yamebainika wanapofanya kazi ambazo ni kinyume na mgao wa kitamaduni na pia kushirikiana na wanawake kufanya kazi ambazo awali zilifanywa na wanaume peke yao. Kazi hizi ni pamoja na kazi ya kushauri. Ilibainika kuwa kazi hii awali ilikuwa ikifanywa na wanaume lakini sasa wanaume wanawashirikisha wanawake katika kutoa mielekeo ya kufanya mambo mbalimbali katika familia zao.

Kazi nyingine ambayo imebadilika ni ile ya ulinzi. Kama tulivyosema katika sura ya pili, ulinzi ni mikakati ambayo inawekwa ili kuhakikisha usalama wa familia. Katika mgao wa kazi wa kitamaduni mikakati hii iliwekwa na wanaume. Ilibainika katika utafiti huu kuwa kazi hii inafanywa na mwanamke hasa katika hadithi ya “Macheo Mengine”. Mwakwetu anamsaidia mumewe kulinda mtoto

wao dhidi ya maangamizi kwa sababu ya ulemavu wake. Pia, wanaume wanafanya kazi ya kupika ambayo kitamaduni ilikuwa kazi ya wanawake. Kazi hii inapofanywa na mwanaume ni ishara ya mgao mpya. Katika utafiti huu pia imebainika kuwa wanaume wanafanya kazi ya kuosha nguo na kuosha vyombo.

Mgao mpya wa kazi za mwanaume pia umebainishwa kwa kuegemea ushirikiano. Kuna baadhi ya kazi ambazo katika mgao wa kitamaduni zilifanywa na wanaume. Hata hivyo, kazi hizi zimechukua mkondo mpya kwa sababu wanaume wanawashirikisha wanawake katika kufanya kazi hizi. Imebainika kuwa wanaume wanaowashirikisha wanawake katika kufanya kazi hizi hufanya hivyo kwa sababu wanafaidika kwa njia moja au nyingine. Kazi hizi ni pamoja na; kutoa suluhisho katika mambo magumu, kukimu mahitaji ya familia, kazi ya kushauri na kazi ya kulima.

Lengo la pili lilikuwa kuchanganua sifa za wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili na tajriba ambazo zimewafanya kuuchukua. Hadithi kumi ambazo zimechanganuliwa katika utafiti huu zimedhihirisha sifa nane za wanaume wanaoukubali mgao mpya wa kazi za mwanaume. Imebainika kuwa wanaume hawa ni wasomi. Wamepata uzindushi wa elimu ambao umewasukuma kuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa njia chanya. Aidha, wamepata uzindushi wa nguvu-hela. Uzindushi huu unawafanya wanaume kufanya kazi ambazo kitamaduni zilifanywa

na wanawake. Hii ni kwa sababu wamegundua kuwa kazi hizi zinaweza kuwasaidia kupata riziki.

Mgao mpya wa kazi za mwanaume umechukuliwa na wanaume ambao wameathirika na mwamko wa usawa wa kijinsia. Pia, wanaume hawa ni wakubalifu na wanyenyekevu. Sifa ya ukubalifu ilidhihirishwa na wanaume ambao wanafanya kazi zilizokuwa za wanawake kwa hiari yao huku wakizipenda kazi hizo.

Lengo la tatu lilikuwa, kuchunguza athari za kuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa mhusika mwanaume katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Ilibainika kuwa mwanaume ambaye ameukaribisha mgao mpya wa kazi za mwanaume huongeza mapenzi katika ndoa yake. Wahusika kama vile Hamduni waliweza kuongeza mapenzi katika ndoa zao kwa kuukaribisha na kuutekeleza mgao mpya wa kazi za mwanaume.

Pia, ilibainika kuwa mgao mpya wa kazi za mwanaume huleta ushirikiano baina ya mwanaume na mwanamke. Katika diwani ya *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine,* hadithi ya "Kachukua Hatua Nyingine" Mzee Mavitu wanashirikiana na mkewe kufanya kazi ya kilimo ili kusaidiana kukimu mahitaji ya familia yao. Kazi hii ya kulima awali ilifanywa na mwanaume kama tulivyoelezea katika sura ya pili. Ndungo (1998) alitambua kazi hii kama kazi ya kitamaduni ya mwanaume. Mwanaume alifanya kazi hii ili kukimu mahitaji ya

familia yake. Utafiti huu uligundua kuwa sasa kazi hii inafanywa na mwanamke na mwanaume huku ikileta mafanikio na ushirikiano katika familia kwani mahitaji ya familia yanatimizwa na mwanamke kwa kushirikiana na mwanaume.

Kadhalika, ilibainika kuwa wanaume wanaotekeleza mgao mpya wa kazi za mwanaume huleta ushirikiano katika familia. Baadhi ya wanaume katika hadithi zilizochanganuliwa wanashirikiana na wake zao kutafuta suluhu kuhusu mambo nyeti katika familia. Utafiti huu umegundua kuwa baadhi ya wanaume, wanawahusisha wake zao katika utoaji wa suluhisho na matokeo yake ni ushirikiano.

Utafiti huu pia ulibaini kuwa mgao mpya wa kazi za mwanaume huleta utoshelevu wa moyoni. Wanaume ambao wamechukua mgao mpya wa kazi za mwanaume hupata utoshelevu wa moyo kwa sababu baadhi ya kazi ambazo wanashiriki huweza kuwaauni mzigo ambao peke yao watahisi kuwa mzito. Dr. Strese ambaye awali aliteseka kwa kuukwamilia mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume alipata afueni baada ya kuukaribisha mgao mpya.

Aidha, ilibainika kuwa mgao mpya wa kazi za mwanaume huleta ufanisi katika maisha ya mwanaume. Hii ni kwa sababu mwanaume ambaye ameukaribisha mgao mpya wa kazi za mwanaume haoni ugumu wa kuomba ushauri wa mkewe katika mambo nyeti bali huchukulia ushauri wa mkewe kwa njia chanya. Matokeo ya kuuchukulia ushauri wa mkewe kwa njia chanya huwa ni ufanisi katika mambo mbalimbali katika maisha ya mwanaume huyo na familia yake kwa jumla.

Maskini alionekana kuomba ushauri wa mkewe kila mara mambo yalipomwia magumu na matokeo yake yakawa ya manufaa kwake na mkewe.

Hali kadhalika, utafiti huu ulibaini kuwa mgao mpya wa kazi za mwanaume pia humfanya mwanaume kujihisi kuwa mtu wa maana sana katika familia yake. Aidha, mwanaume ambaye ameuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume hupata kitulizo fulani anaposhiriki kazi ambazo awali zilichukuliwa kuwa za kike.

Isitoshe, imebainika kuwa mwanaume ambaye ameuchukua mgao mpya wa kazi za mwanaume hufaidika kwa kufanya hivyo. Utafiti huu umegendua kuwa Kazi kama vile ya kukimu mahitaji ya familia zinapofanywa na wanawake huweza kumfaidi mwanaume kwa sababu atapumzishwa kwa kusaidiana na mkewe kufanya kazi hii.

**5. 3 Mchango wa Utafiti**

Utafiti huu utakuwa na mchango mkubwa kwa tafiti ambazo zimeshughulikia masuala ya wanawake. Hii ni kwa sababu umebainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume ambao unaafiki usawa wa kijinsia katika hadithi fupi teule za Kiswahili. Utafiti huu unaweza kuwawezesha wasomi wa fasihi andishi hususan hadithi fupi za Kiswahili kutambua sifa za wanaume wanaopokea mgao mpya wa kazi. Fauka ya haya, utafiti huu utaongeza tahakiki ambazo zimeshughulikia masuala ya kijinsia katika fasihi ya Kiswahili.

Tumeonyesha kuwa mgao wa kitamaduni wa kazi za mwanaume umechukua mkondo mwingine na kuwa mpya. Kazi ambazo wanaume wanafanya katika hadithi zilizoteuliwa zimedhihirika kuwa tofauti na kazi walizokuwa wakifanya awali. Utafiti huu unaweza kuwahamasisha waandishi kufanikisha sifa ya usasa ya hadithi fupi kwa kusawiri wanaume zaidi wanaobadilishana kazi na wanawake.

Isitoshe, mgao mpya wa kazi za mwanaume umeainishwa, kuchanganuliwa na kuelezwa kulingana na malengo ya utafiti huu. Kwa hivyo, utafiti huu unaweza kuleta mwongozo mwafaka kwa wasomi wa fasihi andishi ya Kiswahili katika kuangazia suala zima la mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume. Ugawaji wa nyadhifa mbalimbali katika hadithi fupi za Kiswahili utachukua mwelekeo mpya wa kuafiki uswa wa kijinsia. Kazi atakazopewa mhusika wa kiume zitaafiki matakwa ya usawa wa kijinsia.

Pia, utafiti huu unahimiza wanaume kuchukua mgao mpya wa kazi kwa sababu wakishirikiana na wanawake na kubadilishana majukumu watasaidiana kuimarisha familia yao na jamii kwa jumla. Utafiti huu umeonyesha mabadiliko katika mgao wa kazi za mwanaume na sifa za wanaume wanaouchukua mgao huo. Mabadiliko haya yameonyesha taswira ya mwanaume anayewakilisha kizazi kipya kinachokaribisha mabadiliko katika mgao wa kazi na usawa wa kijinsia.

## 5.4 Mapendekezo

Utafiti huu ulilenga kubainisha mgao mpya wa kazi za mwanaume katika diwani za *Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine, Damu Myeusi na Hadithi*

*Nyingine* na *Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine.* Kuna mambo kadha ambayo utafiti huu haukushughulikia na ambayo watafiti wengine wanaweza kuyashughulikia.

Utafiti unaweza kufanywa kuhusu athari za kisaikolojia za mgao mpya wa kazi za mwanaume kwa wanaume ambao wanafuata mfumo wa kibabedume.

Vilevile, utafiti mwingine unaweza kufanywa kuchunguza jinsi wanawake wanavyowachukulia wanaume wanaouchukua mgao mpya wa kazi.

Hatimaye, utafiti mwingine unaweza kufanywa kuhusu mitazamo ya watu kuhusu mgao mpya wa kazi za mwanaume katika hadithi fupi ili kutathmini ikiwa utanzu wa hadithi fupi umefanikiwa kusawiri wahusika wenye hulka za kisasa.

## MAREJELEO


Adler, M.J. (1993). *The Difference of Man and The Difference It Makes.* Fordham University Press.

Ahmed, E.N, Hamisi, B na Suleiman, A.M. (2013). *Kamusi Teule ya Kiswahili.* Nairobi: East African PublishersbLtd.

Anderson, A.R na Jack, S (2002). *The Articulation of Entrepreneurial.* Social capital: content process Entrepreneurship and regional Development. 14 (13); 193-210

Baxter, L. A. na Montgomery B.M (1998). *Dialectical Approaches to Studying Personal Relationships.* L. Erlbaum Associates. Mahwah.

Bem, S. L. (July 1981). "Gender schema theory: A cognitive Account of Sex Typing". Katika Psychological Review 88 (4): 354–364. doi:10.1037/0033-295X.88.4.354.

Benjamin, S. (1976). *Baby Care.* (4th edition),New York City: pocket Books Publishers.
.

Bever, S.W. (1999). Migration, Household Economy and Gender: a comparative Study of Household in a Rural Yucatan Maya Community, Ph.D. Desertation, Department of Anthropology. Southern Methodist University, Dallas.

Brittan, A. (1997). "Masculinity and Power" in Gould, C. (ed). Gender, New Jersy: Humanities Press. Pp 113/119.

Butler, J. (1990). *Gender Trouble: Feminism and The Subversion of Identity.* New York: Routledge.

Carney,T.F. (1969) Content Analysis for classicists.*Acta Classica, Vol.12 pp151-168.* South Africa: Classical Association of south Africa.

Cherlin, A. J. (1992). *Marriage, divorce, remarriage revised and enlarged ed.* Cambrige: M.A: Havard University Press.

Connell, R. W. (1987). *Gender and Power*. Cambridge: Cambridge University Press.

Dunleavy, M. P. (2007*). American Progress* (Oktoba 2009). “The Shriver Report: A Woman’s Nation Changes Everything.”

Eagly, A.H na Kite, M.E (1987). “Are Sterotypes of Nationality applied to both women and men?” Journal of Personality and psychology, 53, 451-462.

Eagly, A.H; Beall, A; Sternber, R.S. (eds) (2004). *The Psychology of Gender* 2nd ed. New York: Guilford Press.

Elishopher, N.G. (2013). “Factors Affecting Women Leadership In The Public Primary Schools.” Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Engels, F. (1972). *The Origin Of The Family, Private Property and the state.* New York: Pathfinder Press.

Fenistermaker, S.(2002). *Doing Gender, Doing Differences. Inequality, Power, and Instituitional Change.* New York: Routledge.

Foucault, M.(1978). *History of Sexuality.* France, Edition Gallimard.

Gitau, E. N. (2005). “ Unyanyasaji Dhidi ya Wanaume katika Fasihi Andishi ya Kiswahili.” Tasnifu ya M.A, Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Goldbery, H. (1976). *The Hazards of Being Male* buy-online: Surviving the Myth of Masculine Priviledge.

Good, G.E. na Wood, P.K. (1995). Male Gender Role, conflict, depression, and help seeking: Do college men face double jeopardy? *Journal of Counselling and Development,74,70-75.*

Kanogo, T. (2005). *African Womanhood in Colonial Kenya, 1900-1950.* United States: Ohio University Press.

Keith, P.M na Brubaker, T.H. (1979). Male Household Roles in Later Life. A Look at Masculinity and Marital Relationships. *A Journal of National Council on Family Relations.*

Ken, W. na Said A.M (Wah) (2007). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Moran (E.A.) Publishers Limited.

Kibutu, S.W. (2013) "Maudhui na Mitindo ya Lugha Inayotumiwa Kuwasilisha Mafunzo ya Kukuza Vijana Katika Misingi ya Kiuana. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

Kimani, C.W. (2003). "Dhuluma Dhidi ya Wanawake Katika Fasihi ya Kiswahili." Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

King'ei, K. (2000). *Miale ya Uzalendo*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Kurian, G. (2007). Family and Gender in the Transformation of countryside. *Journal of comparative Family Studies. Vol.38. No. 3.*

Lipman, A. (1961). Role Conceptions and Morale of Couples in Retirement. *Journal of Gerontology. 1961, 18, 267-271.*

Longhorn (2011). *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja.* Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Longhorn (2013). *Kamusi ya Karne ya Ishirini na Moja.* Nairobi: Longhorn Publishers (K) Limited.

Maitaria, J. N. (2012). *Mwongozo wa Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Longhorn Publishers Limited.

Mandy, B (2011). Special focus: social stratification studiesnin east Asia. *Asian Journal of Social Science*. Vol. 39. No.1. pg 57-74. Brill Stable.

Masinde, E. W. (2003). "Ushairi wa Kiswahili; Maendeleo na Mabadiliko ya Maudhui." Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Masinjila, M. (1997). Patriachy and Women's participation in Kenya. Publication of the collaborative centre for Gender and Development. Gender Responsive Politics. Nairobi: The Fredrick Ebert Foundation.

Marx, K. na Engels, F. (2020). *The communist Manifesto.* London: Park Publishing House Limited.

Marx, K. (2004). *Capital* Vol. 1, Afterword to the Second German Edition. [4] (http://www. Marxist. Org/archive/marx/works/1867-cl/p3.htm)

Mbaabu, I. (1985). *New Horizons in Kiswahili.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Mbuthia, E.M. (2010). *A Thematic and Stylistic Analysis of Kiswahili Short Stories.* Deutschaland: VDM Muller.

McOnyango, O. (2006). *Mimba Ingali Mimba Na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Focus publishers Ltd.

Merriam Webster (2003). *Merriam Webster Collegiate Dictionary.* USA: Merriam Webster.

Money, J. (1994). "The Concept of Gender Identity disorder in Childhood and adolescence after 39 years." *A Journal of sex and marital therapy 20(3): 163-77.*

Moser, C.O.N. (1999). *Gender Planning and Development: Theory, Practice and Training.* USA: Routledge.

Mugenda, O.M. na Mugenda A.G. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Mugenda, A.G. (2013). *Qualitative Research Methods:* Introduction. Nairobi: Kijabe Printing Press.

Mukopi,L.M.(2005). "Hadithi Fupi za Kisasa za Kiswahili kama Utanzu Mahuluti.Tasnifu ya MA. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Ndungo, C. M. (1998). " Images of Women in African Oral Literature." Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Osore, M.K.(2008). "Defamiliarization In The Novels Of Kezilahabi And Said Ahmed Mohamed." Tasnifu ya Phd. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijachapishwa)

Parson, T. (2004). Katika Franco – German T. V Station ARTE Karambolage.

Perry, J. M na Crouter, A. C. (1990). Men's Provider- role attitude: implicationfor household work and marital satisfaction. *Journal of Family Issues,11,136-156*

Phillips, S.P. (2008). Theory and Methods: Measuring the health effects of gender. Journal of Epidemiology and Community Health. Vol. 62, No.4 Aprili 2008 pp 368-371.

Salim, I.A. (1978). *People of The Coast.* London: Evans Brothers.

Sanja, L (Mh.) (2011). Mwavyaji wa Roho na Hadithi Nyingine. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Scanzoni, J. (1979). Strategies for Changing Male Family Roles: Research and Practice. *A Journal of National Council on Family Relations.* Vol.28.No. 4. Oct. 1979.

Spence, J. T., & Hahn, E. D. (1997). The Attitudes Toward Women Scale and attitude to change in college students. Psychology of Women Quarterly, 24, 17-34.

TUKI (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Toleo la Tatu. Nairobi: Oxford University Press.

United Nations (1975). *Report of the World Conference of the International Women's Year.* Mexico: United Nations Publication.

Wafula, R. na Njogu, K. (2007). *Nadharia Za Uhakiki Wa Fasihi*. Nairobi: JKF.

Walibora, K. na Mohamed, S.A. (Wh) (2007). *Damu Nyeusi na Hadithi Nyingine*. Nairobi: Moran (E.A) publishers Ltd.

Wamitila, K.W (2002). *Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Phoenix publishers Ltd.

Wamitila K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi*: Istilahi na Nadharia. Nairobi: Focus Publishers Ltd.

Wamitila, K.W (Mh.) (2004). *Mayai Waziri Wa Maradhi na Hadithi Nyingine.* Nairobi: Focus Publishers Ltd

Wamitila, K.W (2008). *Kanzi ya Fasihi.* Nairobi: Vide-Muwa publishers Limited.

Wilbon, R.W na Simpson, G.M (2009) *Black Women, Gender and Families;* Vol. 3, No.2. University of Illinios Press.

Woods, J. T. (1997) *Communication Theories In Action.* Callifonia: Wadsworth Publishing Company.

www.un.org/women watch/beijing/pdf/BDPFA.E. pdf 15/06/2015.12.51pm

www.swwc.org/downloads/Report of WCW 1985 15/06/2015